Релятив в глаголе. Определительное предложение может присоединяться к главному с помощью релятивного форманта, занимающего позицию после показателя времени. Релятивные форманты приведены выше в таблице. В отличие от релятивного союза amba-, который может вводить придаточное предложение с глаголом-сказуемым в любом времени, релятивный формант в глаголе сочетается только с показателями настоящего времени -na-, прошедшего времени -li- и будущего времени -ta- (который в этом случае принимает форму -taka-), например: watoto wa***nao***imba “дети, которые поют”, vitu vi***livyo***nunuliwa jana “купленные вчера вещи”, nyumba zi***takazo***jengwa “дома, которые будут построены”.

Отрицательная форма релятива в глаголе – общая для всех времен, показатели которых заменяются отрицательным формантом -si-, сравните: kitabu kinachosomwa, kilichosomwa, kitakachosomwa “книга читаемая, читавшаяся, которую будут читать” > kitabu kisichosomwa. Перевод отрицательного релятива в глаголе зависит от контекста. Если же надо сохранить точное указание времени действия, употребляется релятивный союз и глагол-сказуемое в требуемом по смыслу времени.

Mazoezi

1. Вставьте союз amba- в следующие словосочетания по образцу:

mtoto anacheza > mtoto ambaye anacheza

kitu ni kizuri > kitu ambacho ni kizuri

mkate upo mezani > mkate ambao upo mezani

picha imechorwa; mabasi yanaondoka; kazi zinatekelezwa; duka litafungwa; dada anajifunza; mgomba unaota; mitihani imepita; mahali panajulikana; visu vinakata; gari litatengenezwa; sheria zinaandikwa; mbu wanauma; chakula kinapikwa; maua ni meupe; njia ni ndefu; wanafunzi ni hodari; babu ni mwembamba; mahali ni pazuri; kamusi iko darasani; watalii wako njiani; bibi yuko jikoni.

2. Заполните пропуски союзом amba-:

1. Barua … niliiandika jana imepotea. 2. Mgeni … unamwona hapa ametoka Urusi. 3. Nyumba … amezijenga zina madirisha makubwa. 4. Hivi ni vyeti … sina budi kuvipeleka kesho. 5. Magazeti … baba anayasoma yameletwa asubuhi. 6. Ugali … dada aliupika umempendeza mgeni. 7. Hii ni milima … nilitaka kuipanda tangu zamani. 8. Hapa ni mahali … mamangu alizaliwa. 9. Nitakupa kitabu … nimemaliza kukisoma.

3. Соедините предложения с помощью союза amba-. Замените единственное число множественным в полученных предложениях. Образец:

Kisu hiki ni kikali. Hiki ni kisu changu > Kisu ambacho ni kikali ni changu > Visu ambavyo ni vikali ni vyangu

1. Mfanya kazi anaumwa. Amekwenda kwa daktari. 2. Basi hili linakwenda mpaka Moshi. Basi hili limeondoka. 3. Kitu kimoja kipo hapa. Kitu hiki ni zawadi yako. 4. Njia imenyooka sana. Njia hii inakwenda mpaka bandari. 5. Huyu ni mkulima. Anauza mazao yake sokoni. 6. Hii ni shule. Imejengwa zamani. 7. Hiki ni kifaa kizuri. Nitachukua kifaa hiki safarini. 8. Huu ni mzigo wa babu. Mzigo huo umeletwa na dereva. 9. Embe kubwa liko mezani. Embe hili ni kutoka bustani yetu. 10. Simba mkali anaishi katika msitu huu. Simba huyu anakula watu. 11. Mmea wa kupendeza unaota

mbele ya nyumba yenu. Huu ni mmea wa aina gani? 12. Chakula ni kizuri. Kimepikwa na dada.

4. Переведите словосочетания, употребив союз amba-:

обещание, данное братом; цветы, которые купит молодой человек; закрывшийся банк; клиенты, ожидающие менеджера; перевозимые грузы; оплаченные долги; дорога, идущая к морю; открывшийся магазин; кашляющий ребенок; неизвестное животное; побежденная болезнь; экзамены, которые начнутся; приехавшие вчера рабочие; овощи, не продающиеся на этом рынке.

5. Замените конструкцию с союзом amba- конструкцией с релятивом в глаголе. Образец:

nyumba ambayo ilijengwa > nyumba iliyojengwa

jibu ambalo lilitolewa; nyani ambao wanaharibu mazao; sauti ambayo inajulikana; mtu ambaye anaongoza; maduka ambayo yatafungwa; urefu ambao ulipimwa; taa ambazo zimewashwa; kisiwa ambacho kinatembelewa; wakati ambao umepita upesi; wenyeji ambao watawinda hapa; mtu ambaye anakula.

6. Замените утвердительную конструкцию отрицательной:

vitabu vilivyosomwa; kalamu zitakazoletwa; vijana wanaoimba; taifa litakalogawanyika; sikukuu iliyosherehekewa; kiongozi anayeheshimiwa; nguo ambazo zitafuliwa; mwaka ambao umeanza; bendera ambayo inapepea; wazazi ambao wamepumzika; kipande cha nyama kilicholiwa; mgeni anayekuja.

7. Соедините предложения с помощью релятивного форманта в подчеркнутом глаголе:

1. Msichana yule <u>anacheka</u>. Ni mwanafunzi wa chuo chetu. 2. Huu ni mkate mzuri. <u>Ulichomwa</u> jana. 3. Nitalifuata shauri hili. <u>Lilitolewa</u> na kaka yangu. 4. Huyu ni paka wangu. Paka huyu <u>hashiki</u> panya. 5. Meli ya kigeni <u>imefika</u> bandarini. Meli hii ni kutoka Ulaya. 6. Hawa ni wanafunzi wangu. <u>Wamemaliza</u> darasa la nne. 7. Mimea hii <u>haioti</u> kaskazini. Inaogopa baridi kali. 8. Maswali mengi <u>yaliulizwa</u> na mwalimu. Maswali hayo ni magumu. 9. Vitu

vyako vilipotea. Kumbe vitu hivi viko chini ya meza. 10. Mtu yule anakwenda kwa haraka. Ni mwalimu wetu.

8. Переведите:

1. Студенты, которые сделали упражнения, могут идти домой. 2. Турист, не знающий дороги, потерялся в городе. 3. Книга, которую я прочитал, переведена с английского языка. 4. Возьми фрукты, которые мы купили вчера. 5. Больной, которого осмотрел врач, отправлен в больницу. 6. Ключ, который находится в столе, не мой. 7. Мясо, которое принес официант, очень жесткое. 8. Я хочу надеть платье, которое сшила бабушка. 9. Пассажиры, которые не успели сесть на поезд, поедут автобусом. 10. Мы съели все булочки, которые испекла тетя. 11. Дети нашли убитую змею. 12. Почти все цветы, растущие в этой долине, белого цвета. 13. Иностранцы, не понимающие по-суахили, остались в гостинице. 14. Заповедник, который называется Микуми, находится недалеко от Дар-эс-Салама.

Maneno mapya

ardhi (-) земля; почва
mchezo (mi-) 1)игра 2)матч
mchezaji (wa-) 1)спортсмен; игрок 2)актер; артист
kikapu (vi-) корзина
mpira wa kikapu баскетбол
wavu (nyavu) 1)сетка 2)рыболовная сеть
mpira wa nyavu волейбол
sinema (-) кино, кинотеатр
filamu (-) фильм, кинофильм
video (-) видеофильм
disko (-) дискотека
dansi/dansa (-) танец
ngoma (-) 1)барабан 2)танец
mashuhuri знаменитый, известный
shuka (ma-) 1)кусок ткани 2)простыня
kiuno (vi-) талия, поясница
zumari (-) флейта, дудка
bega (ma-) плечо
unyoya (ma-) 1)перо 2)шерстинка
njuga (-) колокольчик (у танцора)
vazi (ma-) одежда
ukingo (kingo) край; кромка
nakshi (-) узор, орнамент
-kabili стоять напротив (*чего-л.*), стоять перед (*кем-л.*)

utamaduni (tamaduni) культура
mlio (mi-) 1)плач, крик 2)звук; шум
-tikisa трясти
mdundo (mi-) бой; биение
-kimbia бегать

Burudani

Katika Tanzania kuna burudani za aina mbalimbali. Watu wanaokaa mjini wanapenda michezo kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, mpira wa kikapu au mpira wa wavu. Wengine hupenda kukimbia. Kuna watu ambao wanapenda sinema au video. Vijana hupendelea disko au dansi. Watu wanaokaa pwani wanapenda kuogelea na kuvua samaki. Watu wengi na hasa wageni wanaokuja Tanzania wanapenda sana kupanda milima au kwenda mbuga za wanyama. Watu wa Afrika ya Mashariki wanaoishi vijijini hupenda sana kucheza ngoma. Kati ya ngoma ambazo ni maarufu sana ni ile iitwayo 'sengenya'.

Sengenya ni ngoma ya kabila la Wadigo ambalo linaishi nchini Kenya. Huchezwa wakati maalumu au mahali ambapo pana sherehe za sikukuu au za kumkaribisha mgeni mashuhuri. Ngoma hii huchezwa na wanawake pamoja na wanaume. Wachezaji wanaume huvaa mashuka kiunoni ambayo ni ya rangi nyekundu, nyeupe na nyeusi. Mabegani huvaa manyoya marefu na miguuni hufunga njuga. Njuga hizi hufungwa kwenye mguu moja.

Wanawake nao wana mavazi yao. Wao pia huvaa mashuka na mabegani hufunga nguo ya rangi ya buluu au nyekundu ambayo ukingoni imepambwa nakshi ya shanga nyeusi na nyekundu au nyeupe peke yake.

Sengenya huchezwa uwanjani. Wachezaji wanaume huwakabili wanawake. Wote hutikisa mabega yao, na miguu yao iliyofungwa njuga huipiga juu ya ardhi mara kwa mara kufuatana na mdundo wa ngoma na mlio wa zumari.

Ngoma hii ni moja tu kati ya ngoma mbalimbali za watu wa Afrika ya Mashariki. Kwa jumla ngoma zote ni sehemu ya utamaduni wa Waafrika.

Maelezo

1. Слово mchezo “игра” (во мн. числе michezo) может употребляться в значении “спорт”.

2. Словосочетание -piga ngoma имеет русский эквивалент “играть на барабане” (*букв.* “бить барабан”). -Cheza ngoma переводится как “исполнять танец” (*букв.* “играть танец”). Следует отметить, что это выражение употребляется, в основном, в отношении традиционных танцев, а эквивалентом глагола “танцевать” в его более общем значении является словосочетание -cheza dansi. Сравните: Salum amejifunza kupiga ngoma kwa babu yake “Салюм научился играть на барабане у своего дедушки”; Watalii hupenda kuangalia Waafrika wanapocheza ngoma zao za kienyeji “Туристы любят наблюдать за африканцами, когда те исполняют свои народные танцы”; Sitaki kucheza dansi leo, naumwa kichwa “Я не хочу сегодня танцевать, у меня болит голова”.

3. Существительное unyoya “перо”, “шерстинка” во мн. числе – manyoya может предавать значение “мех”, “шерсть”, например: koti la manyoya “меховое пальто”, “шуба”; manyoya ya paka “кошачья шерсть”.

4. Следует обратить внимание на употребление глагола -kimbia “бегать”, который также имеет значение “убегать (*откуда-л., от кого-л.*)” или “избегать (*кого-л.*)”: Watoto wanakimbia mbele ya nyumba “Дети бегают перед домом”; Mwanafunzi amekimbia shuleni (katika/kutoka shule) “Ученик убежал из школы”; Kwa nini unanikimbia? “Почему ты избегаешь меня (убегаешь от меня)?” При передаче движения в направлении к чему-л. или кому-л. этот глагол употребляется в направительной форме -kimbilia: Mtoto ananikimbilia “Ребенок бежит ко мне”; Mbwa amekimbilia msituni “Собака убежала в лес”;

Mazoezi

9. Дайте русские эквиваленты:
wakati wa burudani; aina za burudani; mpira wa miguu; mpira wa mikono; mchezo wa kienyeji; -maliza mchezo; uwanja wa michezo; mchezaji maarufu; mchezaji mashuhuri wa sinema; filamu ya sinema; -angalia video; -cheza ngoma; -piga ngoma; -kimbia masomoni; -kimbilia mtoni; -vaa shuka begani; -fanya kazi bega kwa bega; manyoya ya ndege; manyoya ya kondoo; mavazi ya kike; vazi la jioni; ukingo wa nguo; ukingo wa barabara; -kabili nyumba; -kabiliwa na shida; -tikisa mti; -tikisa kichwa; mdundo wa saa; mdundo wa ngoma; mlio wa simba; mlio wa kuomba msaada; utamaduni wa kitaifa; -wa sehemu ya utamaduni; -panda mimea katika ardhi; -tia maji kwenye ardhi.

10. Дайте эквиваленты на суахили:
различные виды развлечений; время развлечений; виды спорта; быть спортсменом; начать игру; продолжить игру; известный артист; киноактриса; пойти в кино; национальные танцы; быстро бегать; бежать домой; убегать из леса; избегать преподавателя; меховое пальто; собачья шерсть; мужская одежда; носить национальную одежду; берег реки; берег моря; стоять лицом к площади; стоять перед врачом; трясти плечами; качать головой; барабанный бой; бой часов; звуки колокольчиков, привязанных к ногам; телефонный звонок; плач ребенка; крики людей; вносить (*класть*) удобрения в почву; лежать на земле; изучать национальную культуру других народов; африканская культура.

11. Раскройте скобки, выбрав ответ, соответствующий содержанию текста:
1. Watu wa mjini hupendelea burudani kama (michezo, ngoma, kupanda baisikeli). 2. Michezo mbalimbali hupendwa na (watu wa vijijini, wageni, watu wanaoishi mjini). 3. Vijana hujichagulia burudani kama (kuvua samaki, disko, kuogelea). 4. Wanaopenda kupanda milima ni (Waafrika, wageni, watoto). 5. Ngoma ya sengenya ni mchezo maarufu wa (Wakenya, Warusi, wakulima). 6. Sengenya huchezwa na (vijana wa kiume, wanawake pekee,

wanawake na wanaume). 7. Wachezaji hufungwa njuga (kwenye mguu mmoja, kichwani, mabegani). 8. Manyoya marefu huvaliwa na (wachezaji wa kike, wachezaji wa kiume, watu wanaoangalia mchezo). 9. Wanawake huvaa nguo za rangi (ya buluu, nyekundu, nyeusi). 10. Sengenya huchezwa (ndani ya nyumba, porini, uwanjani). 11. Wachezaji wanaposikiliza midundo ya ngoma (wanapiga miguu juu ya ardhi, huimba, huzungumza). 12. Ngoma za kila aina ni sehemu ya utamaduni wa (Waafrika wote, Watanzania, Wakenya pekee).

12. Перескажите текст на суахили.

13. Переведите:

1. Люди, живущие в городе, предпочитают различные виды спорта. 2. Футбол – это игра, которую любят все африканцы. 3. Самый популярный заповедник, посещаемый туристами, находится на севере Танзании. 4. Вы слышали о танце, который называется 'сенгенья'? 5. В этом танце участвуют (-cheza) мужчины и женщины, одетые в разноцветные наряды. 6. Маленькие колокольчики, привязанные к ногам танцоров, издают приятные звуки. 7. Одежда женщин, украшенная орнаментом из черных бусинок, очень красива. 8. Нам очень понравились местные жители, игравшие на барабанах и флейтах. 9. Все гости, приглашенные на этот праздник, радовались, как дети. 10. На уроке суахили студенты смотрели фильм, рассказывающий об африканской культуре.

* * *

Грамматика

Желательно-побудительное наклонение. Название этого наклонения говорит о его значении побуждения субъекта к действию, оно также выражает косвенное приказание, просьбу, пожелание, указание на цель действия. В отличие от повелительного наклонения, которое имеет всего две формы (для ед. числа: simama! "стой!", для мн. числа: simameni! "стойте!"), желательно-побудительное наклонение может

включать все субъектные и объектные показатели, последние занимают позицию перед корнем/основой глагола. Желательно-побудительное наклонение образуется заменой конечного гласного -а бантуского глагола на -е:

Umwambie asimame hapa "Скажи ему, пусть он стоит здесь"; Tumwombe mama atupikie supu "Давайте попросим маму, чтобы она приготовила нам суп".

Односложные глаголы не требуют употребления слогового расширителя ku-:

Waje mapema, tule chakula cha mchana pamoja "Пусть они приходят пораньше, чтобы нам пообедать вместе".

Заимствованные глаголы, оканчивающиеся не на -а, не изменяют окончания:

Nijibu? "Мне отвечать?"; Arudi "Пусть он возвращается"; Tumsamehe "Давайте простим его".

Субъектный показатель 2-го лица ед. числа может опускаться при том, что сохраняется показатель объекта: [u]mwambie "скажи ему", waletee "принеси им".

Отрицательная форма желательно-побудительного наклонения образуется при помощи отрицательного форманта -si-, занимающего позицию непосредственно за субъектным показателем:

Asitusomee "Пусть он нам не читает"; Nisile nyama "Мне не стоит есть мясо"; Wasirudi "Пусть они не возвращаются".

Глаголы в желательно-побудительном наклонении переводятся на русский язык повелительным наклонением, инфинитивом или при помощи таких слов как "пусть", "давай/давайте", "следует", "надо", "стоит" и др. в зависимости от контекста.

Глаголу в желательно-побудительном наклонении могут предшествовать модальные слова lazima или budi "надо", "нужно", "необходимо": Lazima/budi tumpeleke mtoto kijijini "Нам надо отвезти ребенка в деревню".

Если в предложении есть два однородных глагола-сказуемых в желательно-побудительном наклонении, то второй глагол может включать в свой состав показатель

рассказывательной формы -ka-, занимающий позицию за субъектным согласователем:

Twende tu***ka***tembee "Пойдемте погуляем"; Umwonyeshe chumba u***ka***mletee chai "Покажи ему комнату и принеси ему чай".

Первое однородное сказуемое может быть выражено глаголом в повелительном наклонении:

Nenda ukamwambie mama asipike wali leo "Пойди и скажи маме, пусть она не готовит рис сегодня".

В отрицательной форме глагола в желательно-побудительном наклонении -ka- не употребляется.

Mazoezi

14. Замените повелительное наклонение желательно-побудительным, включая его отрицательную форму. Образец:

Soma! > Usome > Usisome

Simama! Imba! Tafsiri! Fuateni! Fikirini! Badili! Ingia! Fungeni! Lala! Kula! Nenda! Njoo!

15. Образуйте желательно-побудительное наклонение. Замените утвердительную форму отрицательной. Образец:

(yeye) -lima > alime > asilime

(sisi) -pokea; (wao) -tunza; (yeye) -meza; (nyinyi) -kaa; (mimi) -la; (wewe) -omba; (wao) -ja; (nyinyi) -enda; (mimi) -rudi; (sisi) -kutana; (yeye) -samehe; (wewe) -jibu.

16. Переведите, используя желательно-побудительное наклонение:

1. Мне идти вместе с вами? 2. Пусть они подождут нас. 3. Вам следует заплатить ему. 4. Давайте сначала хорошо подумаем. 5. Пусть он снизит цену. 6. Испеки, пожалуйста, хлеб. 7. Закройте ваши учебники. 8. Приходи послезавтра. 9. Пусть он не плачет. 10. Не смотри сюда. 11. Не ешьте фрукты до обеда. 12. Им не следует торопиться. 13. Мне не стоит отказываться. 14. Не будем соглашаться с ними. 15. Мне продолжать работать? 16. Пусть они не садятся на этот автобус.

17. Составьте предложения со следующими словосочетаниями, используя желательно-побудительное наклонение и соответствующие субъектные и объектные согласователи. Образец:

(wewe) -leta chai > Tafadhali, uilete chai ya maziwa

(wewe) -karibisha wageni; (sisi) -tafsiri mazoezi; (yeye) -eleza wazazi; (wewe) -ambia mimi; (wao) -peleka mtoto shuleni; (yeye) -ita daktari; (sisi) -nunua baisikeli; (sisi) -funga dirisha; (wao) -saidia sisi; (mimi) -pika ugali.

18. Переведите:

1. Tafadhali, umwonyeshe mgeni chumba chake ukamletee soda. 2. Uwape Juma na Hamisi kahawa ukawatilie maziwa. 3. Niambie jina lako ukaandike namba yako ya simu. 4. Lazima wampeleke mgonjwa huyu mpaka hospitali wakampime. 5. Tusiende katika uwanja wa ndege, tuwangoje nyumbani. 6. Kesho dadako asichelewe kuamka, lazima aende chuo kikuu mapema. 7. Umwambie mama atupikie wali leo. 8. Uwaombe watoto wasicheze mpira kwenye mlango. 9. Wasilinunue gari hili, ni la kizamani sana. 10. Tumwombe mwenyeji wetu atuwekee televisheni chumbani. 11. Nenda ukamwambie shangazi asikate maua leo.

19. Замените подчеркнутую конструкцию желательно-побудительным наклонением:

1. Tulimwomba mhudumu wa mkahawa <u>kutuletea</u> vyombo. 2. <u>Hana budi kumwandikia</u> bibi barua. 3. <u>Nitakuja</u> ofisini asubuhi <u>na nitasoma</u> vyeti vyote. 4. Wazazi walisema kuwa <u>hawana budi kukutana</u> na mwalimu wa shule. 5. Mnataka <u>kwenda</u> wapi wakati wa likizo? 6. Tafadhali, njoo <u>kunisaidia</u> kazi ya nyumbani. 7. Mtumishi anatakiwa <u>kutufulia</u> nguo <u>na kusafisha</u> jiko. 8. Nendeni katika benki <u>na kuchukua</u> pesa. 9. <u>Hawatakwenda</u> kuwinda katika msitu ule. 10. Tuliamua <u>kuupanda</u> mlima Kilimanjaro <u>na kuziona</u> barafu zake.

20. Переведите, употребив желательно-побудительное наклонение в подчеркнутых глаголах:

1. Давайте пойдем в кафе и выпьем чая. 2. Помоги мне обработать это поле. 3. Что мне делать после работы? 4. Пожалуйста, сходи в аптеку и купи таблетки для дедушки. 5. Не забудьте выучить новые слова и переведите весь текст. 6. С кем я должен поговорить о своей работе? 7. Скажи Амине, чтобы она не приходила завтра. 8. Они не должны заходить в эту комнату. 9. Сотрудники обязательно должны закрыть офис, когда будут уходить. 10. Обязательно покажи туристам то красивое озеро.

Maneno mapya

jumba (ma-) большой дом; дворец
jumba la makumbusho музей
askari (-) солдат; военный
polisi (-) 1)полицейский 2)полиция
-dhuru наносить ущерб; причинять убыток; вредить
kiatu (vi-) туфля, ботинок
kofia (-) головной убор (*шапка, шляпа и т. п.*)
miwani (мн.) очки
tiketi/tikiti (-) билет, талон
nauli (-) плата за проезд

Mazungumzo

Asha: Twende tukatembee, Tatu.
Tatu: Vyema. Unataka twende mahali gani?
Asha: Twende mjini tukatazame Jumba la makumbusho ya taifa na tupite madukani.
Tatu: Sawa, nataka viatu vipya, kofia na miwani ya jua.
Asha: Tuondoke sasa? Uko tayari?
Tatu: Tusiondoke sasa. Nina kazi kidogo kumaliza, lakini haidhuru itangoja. Twende.
Asha: Tupite njia hii?
Tatu: Tusipite njia hii kwani inazunguka kidogo. Bora tupite njia ile.
Asha: Mwulize yule askari njia ya karibu ya kwenda mjini. Na usichelewe, saa zinakwenda.

Tatu anazungumza na askari polisi.

Tatu: Yule polisi alisema kuwa ni mbali na hapa. Lazima tupande gari.

Asha: Utapenda tupande basi au tuchukue teksi?
Tatu: Bora tuchukue teksi, tutafika upesi.
Asha: Mwulize dereva nauli itakuwa kiasi gani?
Tatu: Anasema kuwa nauli ni shilingi elfu moja.
Asha: Mwambie atupunguzie. Atupeleke kwa shilingi 500. Mwambie sisi ni wanafunzi, hatuwezi kulipa zaidi.
Tatu: Kama wewe ni mwanafunzi, basi nenda kwa basi. Tiketi ya basi ni rahisi.

Maelezo

1. vyema (vi+ema) “хорошо”, “ладно”. Сравните синонимичные варианты: vizuri; haya.

2. Слово askari “солдат”, “военный” здесь употреблено как синоним слова polisi “полицейский”. Возможен также вариант askari polisi.

3. Выражение haidhuru - застывшая форма глагола -dhuru “вредить”. Оно употребляется в значении “ничего”, “пустяки”, “неважно”: Haidhuru tumechoka, tutaendelea na safari yetu “Ничего, что мы устали, мы продолжим наш путь”. Это выражение также может употребляться как ответ на выражение благодарности: Asante kwa msaada wako. – Haidhuru “Спасибо за вашу помощь. – Не стоит [благодарности]”.

Mazoezi

21. Ответьте на вопросы по содержанию диалога:
1. Asha na Tatu wanaishi mjini au kijijini? 2. Jumba la makumbusho ya taifa liko wapi? 3. Wasichana hao walitaka kwenda mjini kwa ajili gani? 4. Tatu alihitaji kujinunulia vitu gani? 5. Tatu na Asha walichagua njia gani ya kwenda mjini? 6. Nani aliwapa shauri vijana hao? 7. Walipendelea kusafiri mpaka mjini namna gani? 8. Dereva wa teksi alitaka walipe kiasi gani? 9. Je, Tatu na Asha walikubali kutoa kiasi hicho? 10. Waliamua kwenda kwa teksi au kwa basi?

22. Дополните диалог разговором между Тату и полицейским.

23. Выучите диалог наизусть.

24. Переведите:

1. Jumba la utamaduni lililoanzishwa na viongozi wa mji mwezi uliopita haliko mbali na mahali hapa. 2. Alitushauri twende tukatazame Jumba jipya la sinema. 3. Usisome sana wakati wa usiku kwani unaweza kudhuru macho yako. 4. Askari walimshika mwizi aliyeiba ushanga wa mwanamke yule wakampeleka katika kituo cha polisi. 5. Tiketi ya kuingia disko ilikuwa ghali sana, kwa hivyo vijana waliamua waende wakaangalie filamu mpya. 6. Mtoto huyo asilipe nauli ya basi kwa sababu bado ni mdogo. 7. Mwanamume yule aliyevaa kofia nyeupe na miwani myeusi ni mchezaji mashuhuri wa sinema. 8. Haidhuru baridi ni kali mno, viatu vyangu ni vya manyoya.

25. Раскройте скобки, используя желательно-побудительное наклонение глагола. Переведите.

1. Asha alitaka kupita madukani na Tatu alitaka wao (-tazama) mchezo wa mpira wa wavu. 2. Umwulize askari polisi kama sisi (-chagua) njia gani kwenda mpaka uwanja wa michezo. 3. Roza alipenda sana kujinunulia viatu vile virefu vyekundu akamwomba mwuzaji (-punguza) bei. 4. Basi letu liliondoka dakika tano tu zilizopita na basi jingine lazima (-fika) baada ya nusu saa. 5. Majumba haya ni ya kizamani sana, lazima (-tengenezwa). 6. Mara iliyopita tulikwenda Unguja na sasa hebu (-safiri) mpaka Moshi.

26. Переведите:

1. Все билеты на футбольный матч, который скоро начнется, уже проданы. 2. Попроси дедушку, пусть он сплетет большую корзину для фруктов. 3. Ты готова идти в магазин? Пошли купим три белых простыни. 4. Люди, которые много едят, могут причинить вред своему здоровью. 5. Не стой на краю дороги, движение автомобилей здесь очень интенсивное. 6. Африканская культура должна охраняться как часть мировой

культуры. 7. Рыбакам не стоит ловить рыбу сетями в этом озере. 8. Не ставьте мой багаж на землю. 9. В этом национальном танце женщины, одетые в разноцветные ткани, танцуют под звуки барабанов и флейт.

27. Переведите следующий диалог и выпишите из него все глаголы в желательно-побудительном наклонении:

Maneno mapya

-jaribu пробовать; пытаться
-ogesha купать
pudini (-) пудинг
-chemsha кипятить
-poa остывать, охлаждаться
labda/labuda возможно, вероятно, может быть
wasiwasi (ед.) беспокойство, волнение
pasi (-) утюг
-piga pasi гладить
-piga deki мыть пол (*шваброй*)
kelele (-) крик, гам; шум
-piga kelele кричать, шуметь
-jitahidi стараться; стремиться

Mazungumzo

Bibi: Tabita, mimi sasa natoka. Tafadhali watazame watoto.
Tabita: Utarudi lini?
Bibi: Nitachelewa kurudi. Labda nitarudi saa mbili. Watoto wamelala sasa. Jaribu usipige kelele.
Tabita: Niwape chakula gani?
Bibi: Wape maziwa, mayai na pudini. Usiku waogeshe na walaze.
Tabita: Maziwa lazima niyachemshe?
Bibi: Ndiyo, uyachemshe, halafu uyaache yapoe.
Tabita: Unataka leo nifue nguo au nipige pasi?
Bibi: Utafua kesho, lakini piga pasi nguo za watoto.
Tabita: Je, kuna kazi nyingine kufanya leo?
Bibi: Upige deki na usisahau kutilia mimea maji. Tafadhali kesho njoo mapema kwa sababu nitakuwa na wageni.
Tabita: Nije saa ngapi?
Bibi: Jaribu ufike saa kumi na mbili na nusu.
Tabita: Unajua, bibi, hakuna basi wakati huo na mimi naishi mbali. Lazima nije kwa miguu.

Bibi: Basi, jitahidi kufika saa moja.
Tabita: Vyema, nitajaribu nisichelewe, usiwe na wasiwasi. Lazima niondoke nyumbani mapema sana.

28. Составьте предложения со следующими словами и словосочетаниями:
-wa na wasiwasi; -jitahidi sana; -chemsha maji; -jaribu; -poa; -piga kelele; -piga pasi; -chelewa kurudi.

29. Перескажите диалог из упражнения 27 от третьего лица.

30. Назовите, какие из перечисленных ниже слов употребляются с глаголом -piga, а какие с глаголом -fanya:
picha, harusi, simu, hodi, sherehe, sindano, mtihani, kituo, deki, hatua, zumari, pasi, mazoezi, kelele, muziki, haraka, kazi, ngoma.

31. Запомните пословицы и объясните на суахили, как вы понимаете их смысл. Подыщите им русские эквиваленты:
A/ **Kawia ufike**; B/ **Kujaribu si kushindwa**

32. Переведите вопросы и дайте на них ответы на суахили:
1. Какой вид развлечений ты любишь больше всего? 2. Ты любишь спорт? 3. Какой вид спорта ты предпочитаешь? 4. В какие дни недели ты ходишь на дискотеку? 5. Когда ты был в кинотеатре последний раз? 6. Какой актер сейчас самый известный в этой стране? 7. Твои родители будут волноваться, если ты поедешь в Африку? 8. Ты помогаешь маме гладить белье или мыть полы? 9. Обычно ты пьешь кипяченую воду или сырую? 10. Ты пробовал водить машину?

33. Дайте русские эквиваленты:
burudani za watu wa mjini; -maliza mchezo kwa kufaulu; upepo unatikisa miti; koti la manyoya; -pamba nguo kwa nakshi za rangi; mdundo wa kupendeza; mdundo wa damu; mlio wa chombo cha muziki; chakula kinachodhuru afya; askari wanaolinda jumba la serikali; mwizi aliyekimbia kituo cha polisi; tiketi ya kwenda na

kurudi; viatu virefu; saa mbili zilizopita; maji yasiyochemshwa; -weka mbolea kwenye ardhi.

34. Дайте эквиваленты на суахили:
купить билет в кино; победить в футбольном матче; сбежать с уроков; возможно, мы опоздаем; трудиться плечом к плечу; магазин мужской одежды; красивый узор на ковре; стоять на обочине дороги; книга, рассказывающая об африканской культуре; меховая шапка; забыть заплатить за проезд; купить обратный билет; дворец культуры; пройтись по магазинам; пойти на стадион; плести корзину; прошедшие экзамены; кипяченое молоко; живущие под землей насекомые.

35. Напишите сочинение на тему “Мой любимый вид отдыха”.

УРОК 15 (Somo la kumi na tano)
Лексическая тема: Погода и климат (Hali ya hewa)

Грамматика

1. Согласование существительных в локативной форме.
2. Сослагательное наклонение.
3. Взаимный залог.

Согласование существительных в локативной форме. Существительные, оформленные суффиксом локатива -ni, определяют модель согласования с глаголом, указательными, притяжательными и обобщительными местоимениями, посессивным формантом. Выбор согласователя pa-, ku- или mu- зависит от того, какое местонахождение имеется в виду, сравните: nyumbani pananipendeza/kunanipendeza/mnanipendeza "[место] в доме мне нравится": pa- – "рядом с домом" ku- – "где-то рядом с домом", m- – "внутри дома".

Как видно из выше приведенного примера, существительное в локативной форме может быть подлежащим предложения. Глагол "иметь/иметься" также при спряжении выбирает один из локативных субъектных согласователей, например:

shambani pana/palikuwa na/patakuwa na maua "на поле есть/были/будут цветы",

kisiwani kuna/kumekuwa na/kutakuwa na majengo ya zamani "на острове есть/были/будут старые здания",

chumbani hamna/hamkuwa na/hamtakuwa na viti "в комнате нет/не было/не будет стульев".

Притяжательные местоимения имеют следующие формы:

pangu petu	kwangu kwetu	mwangu mwetu
pako penu	kwako kwenu	mwako mwenu
pake pao	kwake kwao	mwake mwao

Посессивный согласователь представлен тремя формами: **pa**, **kwa**, **mwa**, например, mabegani pa wachezaji "на плечах

игроков", mwishoni mwa wiki "в конце недели", mjini kwa mwenzangu "в городе моего друга". Некоторые существительные в локативной форме регулярно определяются посессивом mwa: mwanzoni mwa "в начале", mwishoni mwa "в конце", mikononi mwa "в руках", mpakani/mipakani mwa "на границе/границах», miongoni mwa "среди", kandoni mwa "на берегу" и некоторые другие.

Указательные местоимения:

hapa	huku	humu
hapo	huko	humo
pale	kule	mle

Обобщительное местоимение имеет формы **pote**, **kote**, **mote**, например, bandarini kote "по всей гавани", sokoni pote "повсюду на рынке". При этом следует отметить, что обобщительные местоимения, согласованные по классу mu-, употребляются редко.

Mazoezi

1. Переведите:

1. Ziwani humu hamna samaki. 2. Kikapuni mwa shangazi mna mayai mengi ya kuku. 3. Kijijini kwetu kuna nyumba za ghorofa nyingi. 4. Mabegani pa mchezaji palikuwa na manyoya ya rangi. 5. Vijana hawa watakuwa na harusi mwishoni mwa wiki hii. 6. Harusini kwao hakutakuwa na wageni wengi. 7. Hakukuwa na magari mengi mjini kwetu mnamo saa za usiku. 8. Tunapenda kutembea msituni hapa ambapo pana maua mengi ya kupendeza. 9. Mwalimu alipoingia darasani, humo mlikuwa na kelele nyingi. 10. Nyumbani kwake kote kulikuwa na vitabu. 11. Kisiwani hapa pote pana mimea ya ajabu. 12. Fisi aliyeingia bandani ambamo mlikuwa na kuku wengi alifukuzwa na mbwa.

2. Раскройте скобки:

sokoni (-le, -ote); chumbani (-angu, -ote); dukani (-a bwana, amba-); kichwani (-ake); ukingoni (-a barabara); shuleni (-etu -ote);

ofisini (-le, -a baba); bandarini (-ao, -ote); katika mkahawa (-le, -a mbali); karibu na uwanja (-a michezo, amba-).

3. Переведите словосочетания, употребив локативную форму существительного там, где это возможно:
у меня дома; в его столе; на наших глазах; в офисе брата; на одном маленьком корабле; в посольстве России; во всем городе; на горе Килиманджаро; в тени дерева; в этом большом лесу; в нашей гостиной; в том красном словаре; на этой широкой улице; в этом магазине; на африканском континенте; в той красивой долине; на наших занятиях; на уроке английского языка; во всех портах Восточной Африки; на автобусной остановке; в его спальне; на овощном рынке; в рабочем столе; в загоне для скота; в магазине женской одежды; на кукурузном поле; на всех его картинах; в ваших руках.

4. Замените настоящее время прошедшим и будущим. Образец:

Shambani kuna mahindi > shambani kulikuwa na mahindi > shambani kutakuwa na mahindi

1. Darasani kwetu kuna viti vingi. 2. Chumbani mwa bibi mna chombo cha redio. 3. Shambani pa bwana Musa pana maua. 4. Hospitalini kwao kuna dawa nzuri. 5. Shingoni pa dada pana shanga nyekundu. 6. Mezani humu mna kalamu na penseli.

5. Замените утвердительную конструкцию отрицательной:
1. Msituni hapa pana mimea mirefu. 2. Sokoni kule kuna mboga rahisi. 3. Ubaoni petu pana maneno mapya. 4. Zizini mwake mna mbuzi wengi. 5. Mjini hapa pana posta na benki. 6. Ardhini humu mna mbolea.

6. Переведите, употребив локативную форму существительного:
1. На нашей улице есть продовольственный магазин и почта. 2. На ногах у танцоров были маленькие колокольчики. 3. В этом словаре есть все новые слова. 4. В нашем посольстве есть спортивная площадка и кинотеатр. 5. У вас в доме есть

животные? 6. На той стене был большой синий ковер. 7. В этом озере вода очень холодная. 8. В конце этого месяца в их офисе будут новые компьютеры (kompyuta).

Maneno mapya

hewa (-) воздух
unyevunyevu (ед.) сырость, влажность
-vuma дуть, бушевать (*о ветре*)
theluji (-) снег
majira (мн.) 1) сезон, период 2)время, промежуток времени
msimu (mi-) сезон, период
mvua (-) дождь
-nyesha лить, идти (*о дожде*)
-sita останавливаться, прекращаться
-tanda 1)стелить, покрывать 2)стелиться, расстилаться
mche (mi-) побег, росток; молодое растение
ngurumo (-) 1)грохот, гул, гром 2)рев, рычание
radi (-) молния
-malizika заканчиваться
-vuna собирать урожай
-zuru посещать; навещать
-kua 1)развиваться 2)расти
-chanua распускаться, раскрываться (*о цветах, листьях и т. п.*)
-pungua снижаться, уменьшаться
baadhi (-) некоторое количество, часть
mbegu (-) семя
digrii (-) градус

Hali ya hewa ya Afrika ya Mashariki

Hali ya hewa ya Afrika ya Mashariki ni tofauti katika sehemu mbalimbali. Sehemu za juu kama Nairobi na Arusha ni baridi na hata kwenye vilele vya milima kuna theluji. Sehemu za chini na karibu na pwani kama Mombasa na Dar es Salam jua ni kali na kuna joto na unyevunyevu, lakini upepo ambao unatoka upande wa baharini unapunguza joto, hasa saa za usiku.

Misimu ya mwaka katika Afrika ya Mashariki ni hii. Msimu wa kiangazi huanza mwezi wa Disemba na kuendelea mpaka Machi. Upepo wa mashariki ya kaskazini huvuma. Ni wakati wa joto kali sana, na joto hufika digrii 35 sentigredi. Halafu kuna msimu wa masika, unaoanza mwishoni mwa Machi na kumalizika Mei. Huu ni wakati wa mvua kubwa sana. Mvua hunyesha kila siku na kwa muda mrefu bila ya kusita. Hakuna jua na mawingu hutanda kila siku. Ngurumo na radi ni mambo ya kawaida siku hizi.

Kipupwe ni wakati wa kuvuma upepo wa magharibi ya kusini. Msimu huu huanza Juni na kumalizika Agosti. Huu ni wakati wa baridi, na wakati bora wa kuizuru Afrika ya Mashariki. Hali ya hewa huwa nzuri. Miche huwa imekua mashambani kwa wakulima na maua yamechanua. Wakulima wanavuna.

Mwezi wa Septemba mpaka Novemba ni siku za vuli. Baridi hupungua, na joto kidogo huwa limeanza. Mvua hunyesha hasa saa za mchana. Wakati huo baadhi ya wakulima huanza kupanda mbegu zao.

Maelezo

1. Словосочетание hali ya hewa (*букв.* "состояние воздуха") имеет значение "климат" и "погода": Kesho hali ya hewa itakuwa nzuri "Завтра погода будет хорошая". Hali ya hewa nchini humu ni tofauti na ile ya nchini kwetu "Климат в этой стране отличается от нашего".

2. Жители Восточной Африки различают два больших сезона: **kusi** "куси" – прохладное время года, в течение которого дует юго-западный муссон, и **kaskazi** "каскази" – жаркое время года, период северо-восточного муссона. В рамках этих двух основных сезонов выделяются следующие периоды: **kiangazi** "киангази" - жаркое сухое время года (декабрь - февраль); **masika** "масика" - жаркий период больших дождей (март – май); **kipupwe** "кипупве" - прохладный дождливый сезон с частыми ветрами (июнь – август); **vuli** "вули" - период дождей (сентябрь – ноябрь).

Для обозначения сезонов в странах с умеренным климатом, как правило, используют следующие эквиваленты: лето – **majira ya joto** (*букв.* "жаркий сезон"); осень – **majira ya mapukutiko ya majani** (*букв.* "сезон опадания листьев"); зима – **majira ya baridi [kali]** (*букв.* "холодный сезон"); весна – **majira ya machipuko** (*букв.* "сезон появления побегов, ростков и т.п.").

3. … joto hufika digrii 35 sentigredi "…жара достигает 35 градусов по Цельсию".

4. Слово huwa (hu + -wa) "[обычно] бывает" часто употребляется как наречие со значением "обычно", "как правило" и т.п.: Huwa tunakuja hapa kila siku "Обычно мы приходим сюда ежедневно" Huwa hafanyi kazi Jumamosi "Как правило, он не работает по субботам".

5. Словосочетание ngurumo na radi (*букв.* "гром и молния") может переводиться как "гроза". Возможный вариант с тем же значением mvua ya radi.

Mazoezi

7. Дайте русские эквиваленты:

mvua kubwa; mvua nyingi; vipindi vya mvua; mvua za hapa na pale; mvua inanyesha; hali nzuri ya hewa; hewa ya unyevunyevu; theluji na mvua; -eupe kama theluji; msimu wa baridi; msimu wa kupanda mbegu; msimu wa masomo; majira ya mwaka; majira ya Moscow; upepo unaovuma upande wa baharini; upepo unaopunguza joto; mawingu yametanda; -tanda kitanda; ngurumo na radi; -pigwa na radi; ngurumo za wanyama wa porini; ngurumo za ndege; likizo iliyomalizika; wakati bora wa kuizuru Afrika; mtoto anayekua upesi; baadhi ya miche imekua mashambani; miche ya migomba; -panda miche.

8. Дайте эквиваленты на суахили:

хорошая погода; другой климат; чистый воздух; морской воздух; сильный дождь; дождь льет не переставая; дожди прекратились; сезон дождей закончился; влажная земля; жаркий сезон; учебный семестр; времена года; восточно-африканское время; ветер, дующий с севера; снег с дождем; небо заволокло тучами; гул самолета; бояться грозы; услышать рычание льва; дерево поразила молния; посещать музей; навестить дедушку; быстро развиваться; ребенок вырос; распустившиеся цветы; собирать урожай манго; сеять семена в землю; несколько студентов; некоторые земледельцы; часть людей; побеги кукурузы; ростки картофеля.

9. Заполните пропуски, опираясь на содержание текста:
1. Katika sehemu mbalimbali za Afrika ya Mashariki hali ya hewa ni … 2. Mtu anaweza kuona theluji kwenye vilele vya milima katika … 3. Jua huwa ni kali katika sehemu … 4. Saa za usiku upepo ambao … unapunguza joto. 5. Upepo wa mashariki ya kaskazini huvuma wakati wa msimu wa … unaoendelea toka … mpaka … 6. Kiangazi hufuatiwa na msimu wa … 7. Ngurumo na radi ni mambo ya kawaida ya msimu wa … 8. Msimu unaofuata baada ya masika ni … ambapo huvuma … 9. Wakati bora wa kuizuru Afrika ya Mashariki ni … kwa sababu … 10. Kama kawaida wakulima huvuna mazao wakati … na kupanda mbegu wakati … 11. Vuli ni msimu ambapo … 12. Masika ni kipindi cha mvua … na vuli ni kipindi cha mvua …

10. Переведите:
1. Климат в северных и южных районах Восточной Африки различный. 2. Во многих местах, особенно на побережье, бывает очень жарко и влажно. 3. На вершинах некоторых гор вы можете увидеть даже снег. 4. Ветер, дующий с океана, приносит прохладу в вечернее время. 5. Сезон, когда идут обильные дожди, называется ‘масика’. 6. Гром и молнии – обычное явление в сезон дождей. 7. Во время сезона ‘кипупве’ погода бывает очень хорошая. 8. Молодые растения быстро развиваются в это время года, цветы и листья раскрываются. 9. В сезон ‘вули’ не бывает много дождей, и жара еще не очень сильная. 10. Крестьяне предпочитают сеять семена в период, который начинается в сентябре и заканчивается в ноябре. 11. В некоторых районах урожаи манго собирают несколько раз в году.

11. Расскажите на суахили о климате Восточной Африки.

12. Переведите следующий текст, предварительно ознакомившись с новой лексикой:

Maneno mapya

tete (ma-) тростник, камыш
-sumbua беспокоить, тревожить
-vunjika 1)ломаться 2)разбиваться
-inama наклоняться, нагибаться
wima прямо, вертикально
-anguka падать
-tulia утихать, успокаиваться
-lalamika жаловаться; возмущаться
nguvu (-) сила, мощь
ujeuri (ед.) высокомерие, надменность

Matete na mpapai

Mpapai uliota katikati ya matete. Mpapai ulikuwa mrefu kuliko matete. Mimea hiyo yote ilisumbuliwa na upepo.

Siku moja mvua ilinyesha na upepo mkali ulivuma. Matete yaliinama, upepo ukapita. Mpapai ulisimama wima. Upepo uliendelea kuvuma kwa nguvu. Mpapai ukavunjika.

Upepo ulipotulia mpapai uliona matete yamesimama wima, hayakuanguka. Mpapai ulilalamika sana ukayauliza matete, “Kwa nini nyinyi wadogo hamkuvunjika wakati wa upepo mkali? Mimi nina nguvu, nimevunjika!” Matete yakajibu, “Wewe umevunjika kwa sababu ya ujeuri wako. Upepo ulipovuma sisi tuliinama. Wewe hukuinama, kwa hivyo umevunjika”.

Mazoezi

13. Ответьте на вопросы к тексту из упражнения 12:
1. Mpapai uliota wapi? 2. Mimea hiyo ilisumbuliwa na kitu gani? 3. Matete yalifanya nini wakati upepo mkali ulipovuma? 4. Kwa nini mpapai ulivunjika? 5. Mpapai uliona nini baada ya upepo kutulia? 6. Kwa nini mpapai ulilalamika sana? 7. Matete yalitoa maelezo gani kwa kuujibu mpapai? 8. Je, maneno ya matete yalikuwa ya haki?

14. Составьте предложения со следующими словами и словосочетаниями:
-sumbuliwa na kelele nyingi; -simama wima; -anguka chini; -vunjika mara moja; -tulia; -lalamika sana; -inama.

15. Переведите:
1. Самые высокие папайи на его поле сломались из-за сильного ветра. 2. Не тревожь отца, пусть он немного отдохнет. 3. После обеда ветер, бушевавший все утро, стих, но начал идти дождь.

4. Оставь свое высокомерие и попроси брата помочь тебе. 5. Покупатели жалуются на высокие цены в этом магазине. 6. Спортсмен старался изо всех сил победить в той игре. 7. Он очень высокий, и ему приходится нагибаться каждый раз, когда он входит в эту дверь. 8. После грозы мы обнаружили, что несколько деревьев в нашем саду повалились.

* * *

Грамматика

Сослагательное наклонение употребляется для выражения совета, пожелания, просьбы, побуждения вместо категорично звучащих форм повелительного наклонения. Показателем этого наклонения является формант -nge-, занимающий позицию за субъектным согласователем:

Hukuchoka kutazama televisheni? Ungesoma kitabu “Не устал ли ты смотреть телевизор? Почитал бы книгу”.

Сослагательное наклонение с показателем -nge- передает также значение возможности или обязательности совершения действия в будущем (чаще после глаголов -tumai “надеяться”, -fikiri “думать”, -ahidi “обещать” и т.п. в главном предложении):

Tulitumai kwamba mwalimu angetueleza mara tena “Мы надеялись, что учитель объяснит (должен объяснить) нам еще раз”.

Сослагательное наклонение может передавать значение условности. Реальное условие выражается с помощью показателя -nge- в обеих частях сложного предложения, показатель -ngeli-/-ngali- передает значение меньшей вероятности совершения действия:

Bibi angekuwa na miwani angesoma magazeti “Будь у бабушки очки, она бы читала газеты”.

Angelikuja kwa wakati leo tungelikwenda kutazama mpira “Если бы он пришел сегодня вовремя, мы бы пошли на футбол”.

Значения показателей -nge- и -ngeli-/-ngali- близки, поэтому можно в одной части сложного предложения употребить показатель -nge-, а в другой – -ngeli-/-ngali-.

Показателям сослагательного наклонения в условном значении может предшествовать союз kama “если” перед придаточным предложением:

Kama mvua ingenyesha tungepanda miche “Если бы пошел дождь, мы бы высадили рассаду”.

Односложные глаголы и глаголы -enda, -isha употребляются в сослагательном наклонении со слоговым расширителем ku-:

Angekwisha kazi angekuja mapema “Если бы он закончил работу, он бы пришел пораньше”.

Отрицание показателей сослагательного наклонения образуется при помощи форманта -si-, стоящего перед показателем наклонения:

Usingetia wasiwasi “Ты бы не волновался”; Asingepanda basi angelifika kwa gari “Если бы он не сел на автобус, он бы приехал на машине”.

Взаимный залог передает значение совместного действия. Он образуется при помощи суффикса -na, присоединяемого к основе бантуского глагола:

-piga “бить” > -pigana “бить друг друга, драться, сражаться”, -jua “знать» > -juana “знать друг друга, знакомиться”.

Если глагол оканчивается на два гласных -ua, -aa, -ia, используется суффикс -liana, вытесняющий конечный гласный:

-fungua “открывать” > -funguliana “открывать друг другу”,

-kataa “запрещать” > -kataliana “запрещать друг другу”,

-tia “помещать” > -tiliana “помещать друг друга”.

Глаголы арабского происхождения, оканчивающиеся на /i/, /e/, при образовании взаимного залога используют суффикс -ana:

-ahidi “обещать” > -ahidiana “обещать друг другу”,

-samehe “прощать” > -sameheana “прощать друг друга”.

Арабские глаголы, оканчивающиеся на -u, образуют взаимный залог с помощью суффикса -iana, вытесняющего конечный гласный:

-arifu “сообщать” > -arifiana “сообщать друг другу”.

Односложные глаголы образуют взаимный залог нестандартно:

-pa “давать” > -peana “давать друг другу”,

-ja “приходить” > -jiana “приходить друг к другу”,

-la “есть” > -lana “поедать друг друга” и др.

Суффикс взаимного залога -na может присоединяться к глаголам в направительной форме:

-tembea > -tembelea > -tembeleana “навещать друг друга”,

-taka > -takia > -takiana “желать друг другу”,

-andika > -andikia > -andikiana “переписываться”.

Mazoezi

16. Переведите предложения и проанализируйте употребление сослагательного наклонения:

A/ 1. Tungeweza kuzungumza juu ya hayo baada ya masomo. 2. Babangu angekubali kufanya kazi katika Afrika lakini hapendi joto. 3. Ningekula wali zaidi lakini nimeshiba. 4. Watalii walitumai kuwa kiongozi angewaonyesha njia bora ya kusafiri katika mbuga ya wanyama. 5. Wafanya kazi wameahidi kuwa wangeweza kutujengea nyumba mpya kwa haraka. 6. Ninafikiri ningepika maandazi leo. 7. Nisingekwenda huko bila ya kuwapigia simu kwanza.

B/ 1. Bibi angekuwa na miwani angeweza kukisoma kitabu hiki. 2. Polisi wangelikuja kwa wakati wangelimshika mwizi. 3. Usingepanda gari usingelifika mapema. 4. Ningelikwenda kucheza mpira nanyi kama nisingelikuwa na kazi nyingi za nyumbani. 5. Angekuwa na nguvu angeweza kubeba mizigo yote peke yake. 6. Ningepata likizo ningekwenda nyumbani. 7. Mama angekubali ningenunua mbwa wawili. 8. Kama mbu wasingekuwa wengi chumbani humu ningelala vizuri.

17. Составьте сложно-подчиненные предложения, употребив глагол в сослагательном наклонении:

1. Ramadhani angekuwa mtoto hodari … 2. Kaka asingeliacha ufunguo wa gari ofisini mwake … 3. Tungeweza kusafiri katika Ulaya mwaka huu kama … 4. Ungelikuja kwa wakati leo … 5. Kama wangelialikwa kwenda harusini mwa rafiki yao … 6. Ningelipata nafasi ya kuwinda katika misitu ya Afrika ya Mashariki … 7. Kama tungeliona njaa … 8. Ningekuwa na pesa nyingi … 9. Kama mvua isingenyesha sasa …

18. Переведите:

1. Я бы с удовольствием выполнил эту работу, но у меня нет времени. 2. Если бы ты выпил это лекарство вчера, сейчас тебе было бы легче. 3. Он мог бы получить хорошее образование в Англии. 4. Если бы мы не устали, мы бы посадили еще десять деревьев. 5. Я бы выпил еще кофе, но боюсь, что буду плохо спать ночью. 6. Если бы ты купила курицу, повар приготовил бы нам ужин. 7. Если бы не пошел дождь, мы бы успели собрать урожай кукурузы. 8. Будь у рыбака сеть, он наловил бы больше рыбы. 9. Если бы вы летели самолетом, вы бы не опоздали. 10. У тебя бы не было проблем, если бы ты послушал совета родителей.

19. Образуйте взаимную форму следующих глаголов и переведите их:

-shinda, -ambia, -pa, -kumbuka, -toboa, -tia, -ambukiza, -tembelea, -toa, -julisha, -chagua, -ahidi, -fukuza, -kataa, -kubali, -funga, -fungua, -samehe, -karibisha, -kabili, -shukuru, -uliza, -arifu, -andika, -uma, -ruhusu, -weka, -elewa, -tafuta, -uza.

20. Переведите следующие словосочетания:

-andikiana barua; -pimana nguvu; -fahamiana vizuri; -funguliana milango; -saidiana kwa kazi; -pigana na dada; -onana kila siku; -shikana mikono; -kataliana maombi; -agana na rafiki; -takiana afya nzuri; -sumbuliana kila wakati; -achana kabisa.

21. Переведите, употребив взаимную форму:

1. Давайте будем переписываться и сообщать друг другу все новости. 2. Они попрощались и решили созвониться в конце

недели. 3. Мы пообещали друг другу съездить на рыбалку в следующем месяце. 4. Дети, почему вы все время жалуетесь друг на друга? 5. Только вчера они дрались, а сегодня уже друзья. 6. Перед свадьбой молодые люди обменялись подарками. 7. Не толкайтесь, вы успеете купить билет на этот автобус. 8. Мои родители прожили долгую жизнь и всегда уважали друг друга. 9. Они долго стояли напротив друг друга, не говоря ни слова. 10. Мы не виделись и не навещали друг друга уже полгода.

Maneno mapya

kosa (ma-) ошибка, промах; вина
-kosa 1)ошибаться 2)упускать, пропускать; лишаться
-gombana ссориться, ругаться
-tokea происходить, случаться
moto moto/motomoto в быстром темпе, стремительно
-shindana соревноваться, состязаться
-karibia приближаться, подходить [близко]
-pambana бороться, сражаться
goli (ma-) гол
-funga goli забивать гол
timu (-) 1)команда 2)экипаж
shughuli (-) дело, занятие
mtazamaji (wa-) зритель

Mazungumzo

Juma: Jana nilikwenda mpirani. Si mpira huo! Ulikwenda?
Ali: La, sikwenda. Je, mpira ulikuwaje?
Juma: Ulikosa mambo. Kwani wewe si mtazamaji wa mpira?
Ali: Hutokea naenda mara nyingine.
Juma: Ningalijua kuwa ulitaka kwenda basi ningalikwambia tufuatane.
Ali: Hebu nieleze mpira ulikuwaje?
Juma: Mpira uliendelea motomoto. Watu walishindana, waligombana, walisukumana hata walikaribia kupigana.
Ali: Lo! Basi kweli nilikosa mambo! Wachezaji walikuwa nani?
Juma: Wachezaji wa Dar es Salam walipambana na wachezaji wa Unguja.
Ali: Walioshinda ni nani? Timu ya Unguja?

Juma: Hapana. Waliocheza vizuri si wale walioshinda, na walioshinda hawakucheza vizuri. Timu ya Dar es Salam ilifunga magoli matano kwa matatu ya wachezaji wa Unguja.
Ali: Kama utakwenda Ijumaa inayokuja, tafadhali niarifu na mimi nitapenda kufuatana nawe.
Juma: Ningalijua unataka kwenda jana ningalikupitia.
Ali: Jana nisingaliweza kwenda kwa sababu nilikuwa na shughuli nyingine.

harufu (-) запах, аромат
-shtuka поражаться, удивляться
-tambua 1)узнавать, распознавать 2)догадываться
-amsha будить
kishindo (vi-) шум; стук; удар
mbio (-) бег; гонки
maskini бедный, нищий
bunduki (-; ma-) ружье; винтовка
-umiza причинять боль, ранить
risasi (-) пуля; патрон
-fa умирать, погибать
-tambaa ползать, ползти
-nyanyua поднимать
-kumbatia обнимать
tone (ma-) капля
kenge (-) варан
jeraha (ma-) 1)рана 2)болячка
-poteza терять, утрачивать
uamuzi/ uwamuzi (ед.) решение
-sikitika 1)горевать 2)сожалеть
sikitiko (ma-) огорчение, сожаление

Fikiri kabla ya kutenda

Fineasi alikuwa na mbwa mweusi aliyeitwa Pegi. Alikuwa mbwa mkubwa tena mkali sana. Pegi alikuwa pia mlinzi hodari wa nyumba ya Fineasi. Alilinda usiku na mchana. Kila wakati alitembea kuzunguka nyumba ya Fineasi. Wageni waliomtembelea Fineasi walimwogopa mbwa huyo kwa sababu ya ukali wake. Mara nyingi Pegi aliwafukuza wezi walipojaribu kuiba nyumbani au fisi walipotaka kukamata kuku. Pegi alikuwa habweki ovyo. Alibweka

alipoona adui au mtu asiyemfahamu. Pua yake ilimsaidia kutambua harufu ya watu na wanyama mbalimbali.

Siku moja Fineasi alipumzika ndani baada ya chakula cha mchana. Mkewe alikuwa na mtoto nyuma ya nyumba yao. Baadaye alimwacha mtoto akaenda jikoni kuosha vyombo. Pegi alipumzika akilala karibu na mtoto. Mara mkewe Fineasi alisikia vishindo nje. Alishtuka akakimbilia ndani akamwamsha mumewe akisema, "Mume wangu, amka! Nje kuna hatari!" Kisha akatoka nje haraka. Mkewe Fineasi alipofika mlangoni alimwona Pegi ana damu mdomoni. Moyo wake ulikwenda mbio akilia kwa sauti, "Maskini mwanangu! Pegi akamla mwanangu!" Fineasi aliposikia kelele za mkewe alitoka na bunduki yake. Akampiga Pegi risasi moja. Pegi akaanguka chini akafa mara moja. Fineasi na mkewe walitazama hapa na pale lakini hawakumwona mtoto. Mara wakasikia sauti ya mtoto akilia. Kumbe mtoto alitambaa kuelekea upande mwingine wa nyumba. Mkewe Fineasi alimkimbilia mwanawe. Akaona hakuumizwa hata kidogo, akamnyanyua akamkumbatia kifuani mwake.

Fineasi alirudi kumtazama mbwa wake. Kabla hajamfikia aliona matone ya damu ardhini. Aliyafuata matone hayo hadi kwenye majani. Alishtuka kumwona kenge mkubwa amekufa. Kenge huyo alikuwa na majeraha mengi mwilini. Fineasi akamwambia mkewe, "Unaona! Kumbe Pegi alipigana na huyu kenge. Bila shaka kenge alitaka kumwumiza mtoto. Loo! Sasa tumempoteza mlinzi. Tulifanya uwamuzi wa haraka. Kila mara ni vizuri kufikiri kabla ya kutenda. Mkewe Fineasi alimtazama Pegi kwa masikitiko makubwa akasema, "Haraka haraka haina baraka".

Maelezo

1. ... alitembea kuzunguka nyumba "... она бродила вокруг дома"; ... alitambaa kuelekea upande mwingine wa nyumba "... он полз по направлению к другой стороне дома". Инфинитивная форма глагола -zunguka "поворачиваться", "обходить" выполняет функцию предлога "вокруг", а инфинитив глагола -elekea "направляться" соответствует русским предлогам "к", "по направлению" и т.п. (Сравните инфинитив kwenda с тем же значением).

Mazoezi

14. Найдите в тексте из упражнения 13 суахилийские эквиваленты:
большой и очень злой пес; отличный сторож; охранять и днем и ночью; бродить вокруг дома; лаять понапрасну; учуять запах; в ужасе она бросилась в дом; ее сердце бешено заколотилось; выпустить пулю; свалиться замертво; осмотреться; ничуть не пострадал; прижать к груди; капли крови привели его в траву; быть израненным; принять поспешное решение; с огромным сожалением.

15. Дайте русские эквиваленты:
-tenda kazi; -tenda vizuri; -tenda vibaya; -anguka kwa kishindo; vishindo vya ngurumo; kishindo cha bunduki; mbio za magari; -piga mbio; -piga bunduki; -piga risasi; -nyanyua mkono; -nyanyua macho; -tambua sauti; -tambua adui; -tambua ukweli; adui wa hatari; adui mkali; tone la mvua; tone la maji; harufu ya maua; harufu ya rangi; -sikia harufu; -pata jeraha; -tibu majeraha; -poteza maisha; -poteza wakati; -poteza pesa; uamuzi bora; -fanya uwamuzi; -fikia uwamuzi; -fa kwa ugonjwa wa hatari; -fa kwa risasi; kufa kwa babu; mkulima maskini; nchi maskini; ukoo maskini; wadudu wanaotambaa; mimea inayotambaa; -kumbatia mtoto kifuani; -kumbatiana; -sikitika sana; kwa masikitiko makubwa.

16. Перескажите на суахили текст из упражнения 13.

17. Переведите:
1. Они все сделали правильно, застрелив злую собаку. 2. Мой брат поступил плохо, обидев (*причинив боль*) маленькую девочку. 3. Вы зря приехали, все билеты уже проданы. 4. Ты узнал врача, который залечивал раны нашей собаки? 5. Не теряйте время, начинайте готовиться к экзаменам. 6. К большому сожалению, наш руководитель принял ошибочное решение. 7. Мы с ужасом узнали, что у этого бедного крестьянина умерла жена. 8. Гулять в этом парке опасно, здесь ползает много змей. 9. Отец поднял сына, чтобы он смог лучше

видеть автомобильные гонки. 10. Дедушка получил это ружье в подарок, так как он был очень хорошим сторожем. 11. Многие солдаты потеряли свои жизни в борьбе с этим жестоким врагом. 12. Цветы, посаженые вокруг нашего дома, издают чудесный аромат.

* * *

Mazoezi ya kujiandaa kusikiliza hadithi

Maneno mapya

siafu (-) муравей
mwewe (-; wewe) коршун
-ota jua греться на солнце
-shuka спускаться, опускаться
shimo (ma-) яма; нора; отверстие
huruma (-) сочувствие, сострадание
uchokozi (ед.) 1)провокация 2)агрессия
mate (мн.) слюна
-tema mate плевать
sumu (-) яд, отрава
umoja (ед.) единство

18. Дайте русские эквиваленты:
hapo zamani sana; -tafuta chakula; -penda kuota jua; -shuka chini kwa haraka; -ingia ndani ya shimo; -ona huruma; -anza uchokozi; -acha uchokozi; -kasirika mno; -ishi kwa raha; -tema mate; -meza mate; sumu kali; -ua kwa mate ya sumu; -fa kwa sumu; -uma bila ya huruma; -zidi kuuma; kumshinda nyoka; -toka damu; umoja ni nguvu; -fikia umoja kamili.

19. Переведите:
1. Siafu ni mdudu mdogo ambaye hujitahidi sana kufanya kazi. 2. Mwewe ni ndege ambaye macho yake ni makali sana. 3. Wanyama wadogo wanaokaa chini kama panya, nyoka au kuku ni chakula cha mwewe. 4. Mwewe akitaka kula hana budi kushuka chini. 5. Nyoka kama kawaida hana huruma kwa wanyama, huwaua akiwatemea mate yake ya sumu. 6. Mwili wa nyoka ni mrefu na anamzidi siafu ambaye mwili wake ni mfupi kabisa. 7. Panya akimwona mwewe anayeruka mbinguni hukimbia shimoni kujificha kwa sababu hapendi kufa. 8. Wanyama wakali wengi kama mamba, fisi au faru mara nyingi huonyesha uchokozi. 9. Hadithi niliyosimuliwa na baba yangu inaeleza kuwa zamani sana wanyama wote waliishi kwa

umoja, walikutana uwanjani, kuota jua na kupeana habari. 10. Mtu na mbwa wana uhusiano mzuri kwa vile mbwa huilinda nyumba ya mtu na hivyo kumpatia nafasi ya kuishi salama na kwa raha.

20. Ответьте на вопросы:
1. Siafu ni mdudu au mnyama? 2. Mwewe ni mnyama au ndege? 3. Nani ni hodari zaidi katika kufanya kazi, siafu au tembo? 4. Nani ana mwili mkubwa zaidi, tembo au chura? 5. Sumu ya nani ni kali zaidi, ya nyoka au ya mbu? 6. Je, siafu anaweza kuruka? Nani anaweza kuruka? 7. Wanyama gani wanaishi shimoni? 8. Watu huogopa wanyama gani? 9. Ukimwona mnyama au ndege akitoka damu utamwonea huruma? Utamsaidia vipi? 10. Wanyama gani hupenda kuota jua?

21. Дайте эквиваленты на суахили:
быть друзьями с давних пор; пригласить друга погреться на солнце; убегать от опасного зверя; жить комфортно; в поисках единства; одерживать победу; несколько муравьев; ядовитая слюна; проявлять (*показывать*) агрессию; искусать все тело; истекать кровью; сильно бояться; покинуть чужое жилище (*дом*); умереть от страха.

22. Согласуйте существительные со словами в скобках:
mashimo (-embamba, -a panya, -ngapi); sumu (-ingine, -ote, -a hatari); mwewe (-le, -moja, -epesi); jua (-kali, -a Kiafrika); uchokozi (-ake, -ingi); mate (-enu, -ote); mwili (-ako, -zima).

23. Переведите, используя желательно-побудительное наклонение:
1. Коршун опустился вниз, чтобы схватить зайца. 2. Змея попросила муравьев спрятать ее. 3. Змея сказала насекомым: "Пожалейте меня". 4. Муравьи захотели, чтобы их дом был также домом и для их давнего друга. 5. "Давайте жить все вместе! – сказали они. 6. Маленькие насекомые сразу поняли, что им следует прогнать чужака из своей норки. 7. "Иди к себе домой!" – закричали они. 8. Змея просила, чтобы ее не кусали. 9. Она плакала и говорила: "Не убивайте меня". 10. Муравьи

решили, что им не стоит иметь отношения с животными, которые предпочитают агрессию дружбе.

24. Поменяйте конструкцию на отрицательную:
1. Umoja wao umekwisha. 2. Ndege wengi waliruka angani. 3. Mwili wake unaumwa sana. 4. Mdudu yuko shimoni mwake. 5. uchokozi wa nyoka uachwe. 6. Sumu kali zinatumiwa katika maabara. 7. Mate ya mgonjwa yatapelekwa kwa daktari. 8. Nyumba ya mwewe iko milimani. 9. Siafu walikufa kwa hofu.

Kusikiliza hadithi

- Прослушайте текст полностью.
- Повторите в паузах фразы вслед за диктором.
- Закончите предложения вместо диктора.
- Задайте друг другу вопросы на суахили по содержанию прослушанного текста и дайте на них ответы.
- Ответьте на суахили на вопросы диктора.
- Изложите письменно на суахили содержание текста.

* * *

Mazoezi

25. Переведите следующий текст и переделайте его в диалог:

Siku moja mtoto mdogo alimwona mama yake akilia. Alitaka kujua mbona analia. Akamwendea baba yake aliyekaa nje akisoma gazeti, akaanza kumwuliza maswali. Lakini baba hapendi kusumbuliwa, hasa anapsoma magazeti. Yule mtoto akitaka sana kuelezewa sababu ya kulia kwa mamake, alizidi kumwuliza baba swali lake. Hapo baba akamwambia mwanawe aende akamwulize mama kama analia kitu gani. Sauti ya baba ilionyesha kuwa amekasirika kidogo.

Hata hivyo mtoto hakuondoka pale alipokuwa wala hakuonekana anaogopa. Akamwuliza baba, mbona yeye halii. Yule baba kwanza alijibu kwamba wanaume hawalii kabisa, lakini punde akafahamu kuwa anasema uongo. Kama mwanawe atagundua kuwa hata wanaume wakati mwingine hulia, ataona haya. Kwa hivyo

alimjibu kwamba wanaume hulia usiku wakati watoto wadogo wanapolala usingizi mnono. Hapo mtoto yule aliahidi kuwa yeye ataacha kulala usiku ili amwone na baba yake akilia. Alisema hayo huku akiondoka kwenda kuchezea vitu vyake.

26. Переведите следующие анекдоты и перескажите их на суахили:

Maneno ya kusaidia tafsiri

pipi (-)	конфета (*карамель*)
-hesabu	считать, подсчитывать
Sasa nini?	Ну и что?

1. Мама говорит своей дочке:
   - Вот тебе десять конфет, половину отдай брату.
   - Хорошо. Я дам ему три конфеты, – отвечает девочка.
   - Разве ты не умеешь считать?
   - Я-то умею, а он нет.

2. Максу шесть лет. Он говорит своему другу:
   - Борис, твоя мама учительница, а ты совсем не умеешь ни читать, ни писать.
   - Ну и что? Твой отец – зубной врач, но у твоего маленького брата совсем нет зубов.

27. Напишите на суахили сочинение на тему "Watu hufuga mbwa kwa ajili gani?". Используйте лексику урока.

SOMO LA TATU
Лексическая тема "Путешествие"

Грамматика

Местоимение -o -ote. Местоимение -o -ote – это релятивная форма обобщительного местоимения "весь". Оно состоит из двух частей: релятивного показателя, который согласуется по нормам согласования этого форманта, и обобщительного местоимения, согласуемого, как это свойственно разряду местоимений:

класс	ед.ч.	мн. ч.
m-/wa-	ye yote	wo wote
m-/mi-	wo wote	yo yote
ji-/ma-	lo lote	yo yote
ki-/vi-	cho chote	vyo vyote
n-/n-	yo yote	zo zote
u-/n-	wo wote	
ku-	ko kote	
(pa-/ku-/mu-)	po pote, ko kote, mo mote	

Местоимение -o -ote в зависимости от контекста переводится как "любой", "всякий", "какой-либо", "какой-нибудь", "какой-то" и т.п., а в отрицательных предложениях – "никакой", например:
Maswali yo yote yatajibiwa "На любые вопросы ответят";
Nipe kitabu cho chote "Дай мне какую-нибудь (любую) книгу";
Hali nyama yo yote "Он не ест никакого мяса".

При опущении в предложении таких слов как jambo "дело", kitu "вещь", neno "слово" согласованное с ними местоимение переводится соответствующим русским неопределенным местоимением:
Sikuona (*kitu*) cho chote "Я ничего не видел";
Wataka kusema (*neno*) lo lote? "Ты хочешь что-то сказать?";
Wao hukubali na (*jambo*) lo lote "Они согласны с чем угодно".

Mazoezi

1. Согласуйте существительные с местоимением -o -ote: vitunguu, saa, mawingu, ubao, tofauti, nguo, karani, vyeti, raha (*ед.*), mchezo, kitafunio, mkoa, matembezi, miche, ufunguo, tofali, mkoa, matembezi, uzuri, wasiwasi, mahali.

2. Переведите:

1. Kazi yo yote itanifaa sasa. 2. Usikae kimya, ujibu swali lo lote. 3. Mtu ye yote angefurahi kupata zawadi kama hii. 4. Vijana wa umri wo wote wanakubaliwa kusoma katika chuo hiki. 5. Polisi alipoingia chumbani kwanza hakusikia harufu yo yote. 6. Msiache cho chote hapa baada ya somo kumalizika. 7. Sioni matunda yo yote mabivu kwenye mti huu. 8. Hamtakuwa na taabu zo zote katika safari hiyo. 9. Hakuna daraja lo lote la kuvukia mto mahali hapa. 10. Huyu ni mtu mkali sana, hana huruma yo yote kwa wengine, hasa kwa maadui wake. 11. Sina hakika yo yote kama atakuja.

3. Переделайте конструкцию предложений по образцу:

Ninataka vitabu vyote > Sitaki kitabu cho chote

1. Ameleta picha zote za rangi. 2. Nilitembelea miji yote mikubwa ya Tanzania. 3. Mtoto amekula matunda yote yaliyonunuliwa na mama. 4. Tutatafsiri mazoezi yote ya Kiingereza. 5. Aliwakuta wageni wote kwenye kituo cha basi. 6. Mwalimu ameyasamehe makosa yote ya mwanafunzi yule mvivu. 7. Mpishi ameweka vitoweo vyote mezani. 8. Anatia mbolea zote shambani mwake.

4. Переведите:

1. Я выполню любую твою просьбу. 2. Ты уже принял какое-либо решение? 3. Нам не нужен никакой менеджер. 4. Звони мне в любое время дня и ночи. 5. Он еще не получал никакой зарплаты на новой работе. 6. Приготовь что-нибудь поесть, я ужасно голоден. 7. Ты знаешь хоть какой-нибудь иностранный язык? 8. В этой комнате нет никаких стульев. 9. Дай мне, пожалуйста, какой-нибудь листок бумаги, мне надо написать письмо. 10. Нас устроит любая цена этого дома.

Maneno mapya

-tangaza объявлять, сообщать
-jali обращать внимание, придавать значение
mafuta (мн.) 1)масло, жир 2)нефть; топливо
-kagua осматривать, обследовать; инспектировать
-tayarisha приготавливать, готовить
-simamisha останавливать, прекращать
honi (-) гудок, сирена
motokaa (-) автомобиль
-shangaa удивляться, изумляться
-zima гасить, тушить; глушить
injini (-) двигатель, мотор
-dhani думать, считать
-kanyaga наступать (*ногой*), наезжать
-gonga 1)ударять, бить 2)ударяться, сталкиваться
moshi (ед.) 1)дым 2)пар
mjinga (wa-) глупец, дурак
ukanda (kanda) ремень, пояс, лента
-chemka кипеть, бурлить
-funika покрывать, накрывать
kifuniko (vi-) крышка
-shangilia/-shangiria устраивать овацию, приветствовать (*криками*)
kofi (ma-) 1) ладонь 2)аплодисменты

Kuvunja safari

Redio ilitangaza siku moja kuwa wachezaji wa ngoma za kienyeji watashindana Nairobi. Wanafunzi bora wa shule moja wamechaguliwa kwenda mjini kutazama michezo hiyo.

Siku ya safari hiyo watoto wote waliamka asubuhi na mapema na baada ya kula kifungua kinywa kila mmoja alijichukulia chakula chake cha mchana. Walifika shuleni kabla ya saa mbili lakini gari lilichelewa sana. Dereva wa gari hilo hakujali kuchelewa kwake, akisema, “Nilikwenda kulijaza gari langu mafuta na pia kulikagua na kutengeneza sehemu ambazo ni mbaya ili kulitayarisha gari kwa safari ya Nairobi. Sasa niko tayari. Hamna shida zo zote. Ingieni, twende.”

Watoto waliingia garini pamoja na mwalimu wao. Gari lilianza kuondoka, likashika mwendo wake vizuri sana na likasafiri kwa muda wa saa nzima. Kisha mwalimu akamwambia dereva asimamishe gari ili watoto wapumzike kidogo. Baada ya robo saa dereva alipiga honi ya motokaa akiwaita watoto warudi garini.

Gari lilianza mwendo kwa mara ya pili na kabla halijashika mwendo vizuri wote walisikia kishindo kikubwa kwenye kichwa cha motokaa hiyo, wakashangaa mno. Hapo hapo dereva akalisimamisha gari, akazima injini, akafungua kichwa cha gari, akakagua sehemu zote lakini hakuona cho chote kilichoharibika. Akasema, "Nadhani gari lilikanyaga jiwe, halafu jiwe hilo likaruka na kuligonga gari. Watoto, ingieni garini, twende."

Mwalimu alikuwa na mashaka, akamwuliza dereva, "Una hakika ni jiwe? Hakuna sababu nyingine yo yote?" Dereva alicheka tu, akatia injini moto, akasema, "Mnaona, gari limeshika moto vizuri. Twendeni, tunachelewa michezoni."

Gari lilishika mwendo na baada ya mwendo mrefu kidogo kishindo cha pili kilifuata. Gari likasimama. Watoto wakaona moshi unatoka kwenye kichwa cha gari. Dereva akafanya haraka akafungua kichwa cha gari, moshi mwingi ukatoka. Watoto waliambiwa waondoke karibu na gari hilo wakati gari linapokaguliwa. Dereva na mwalimu walilikagua, halafu dereva akasema, "Ah, mimi mjinga! Gari hili halina ukanda. Ulikatika wakati wa kishindo cha kwanza, na maji yakachemka na kutupa kifuniko hiki juu. Na hiyo ilikuwa sababu ya kishindo cha pili." Mwalimu akamwuliza, "Sasa tufanyeje?" Dereva akasema, "Gari hili haliwezi kwenda. Lazima niende Nairobi kununua ukanda mpya." Akasimamisha motokaa nyingine iliyopita wakati ule, naye mwalimu akabaki na watoto wake kwenye gari lililoharibika.

Saa tisa hivi dereva alirudi kutoka Nairobi na akaanza kulitengeneza gari. Alilitengeneza kwa muda wa nusu saa, halafu akalitia gari maji, kisha akaiwasha injini, ikashika vizuri. Watoto wakamshangilia kwa makofi. Dereva akawaambia watoto waingie garini, lakini mwalimu alisema, "Nasikitika tutaivunja safari ya kwenda Nairobi kwa sababu tumechelewa sana njiani. Basi, dereva, turudi nyumbani."

Maelezo

1. kifungua kinywa "первый завтрак" (*букв.* "то, что открывает рот").

2. kichwa cha motokaa "капот автомобиля".

3. Словосочетание -shika mwendo означает "набирать скорость" (*букв.* "хватать движение"), а -shika moto – "заводиться" (*букв.* "хватать огонь"). Для передачи значения "включить зажигание", "завести двигатель" используются выражения -tia gari/injini moto или -washa gari/injini.

Mazoezi

5. Найдите в тексте эквиваленты следующих словосочетаний:

по радио объявили; проснуться рано утром; позавтракать; не придал значения своему опозданию; заправить машину топливом; починить неисправности; нет никаких проблем; я готов; садитесь и поехали; машина быстро набрала скорость; сигналить; трогаться с места; капот автомобиля; заглушить двигатель; проверить все детали; наехать на камень; камень отскочил и стукнулся об автомобиль; у него были сомнения; он не обнаружил никакой поломки; машина сразу же завелась; последовал второй удар; из капота повалил дым; во время осмотра автомобиля; какой же я глупец!; лопнул приводной ремень; вода закипела и отбросила крышку; остановить проезжавшую мимо машину; остаться в сломанном автомобиле; дети ему зааплодировали; отменить поездку.

6. Дайте русские эквиваленты:

-tangaza habari; -tangaza kufunguliwa kwa mkutano; bila ya kutangaza lo lote; -jali makosa; kutojali hali mbaya ya hewa; kwa kutojali cho chote; mafuta ya kupikia; -jaza gari mafuta; bei ya mafuta; -kagua mgonjwa; -kagua ndege; -tayarisha mkutano; -tayarisha shule kwa masomo; -jitayarisha kwa mitihani yo yote; -simamisha mtu ye yote njiani; -simamisha kazi; -piga honi; honi ya motokaa; kwa kushangaa sana; sauti ya kushangaa; bila ya kushangaa; -zima taa; -zima moto; -zima injini; unadhani hivi?; sidhani atakuja; -kanyaga jiwe; usikanyage hapa; gari limemkanyaga mpitanjia; -gonga mlango; -gongana na gari; -gonga ukuta; moshi mwingi; gari la moshi; harufu ya moshi; wingu la moshi; mjinga; swali la kijinga; ujinga wake; -funga ukanda; ukanda wa kushika nywele; ukanda mwembamba; mafuta

yanachemka; -chemsha maji; kifuniko cha sufuria; kifuniko cha taa; -funika uso kwa mikono; -jifunika kwa kitambaa cho chote; -shangilia kwa furaha; -shangilia kwa makofi; -piga makofi.

7. Запомните следующие выражения и составьте с ними предложения:

mafuta mazuri	духи
-zima kiu	утолять жажду
mjinga wa kutojua kusoma wala kuandika	безграмотный

8. Замените утвердительную форму подчеркнутого глагола отрицательной:

1. Wachezaji wa ngoma watashindana mjini mnamo Ijumaa. 2. Michezo itaonyeshwa kwa wanafunzi wote. 3. Siku hiyo vijana walichelewa kuamka. 4. Mwalimu aliwaambia watoto wajichukulie chakula cho chote cha mchana safarini. 5. Kuchelewa kwa dereva kulimpendeza mwalimu. 6. Gari lilitayarishwa vizuri kwa safari. 7. Wote waliona kuwa dereva yuko tayari kuondoka. 8. Watoto waliombwa waingie ndani. 9. Motokaa ilishika mwendo vizuri. 10. Dereva alisema kwamba akileta ukanda mpya gari litaendelea na safari. 11. Sehemu zote za gari lililoharibika zimeshatengenezwa. 12. Mwalimu alikuwa na mashaka mengi moyoni mwake. 13. Kuna mawe mengi njiani huko. 14. Dereva angekuwa mjinga watoto wangevunja safari ya Nairobi.

9. Согласуйте существительные со словами в скобках:

injini (-moja, -o -ote); wajinga (-ingine, -o -ote); kifuniko (-zito, -o -ote); honi (-le, -a basi); motokaa (-ingine, -o -ote, -tasimamishwa); mafuta (-ingi, -mejazwa); ukanda (-embamba, -o -ote); makofi (-ingi, -a watazamaji); kifungua kinywa (-o -ote, -nafaa); mwendo (-kali, -a motokaa); dereva (-ingine, -o -ote); vishindo (-ote, -wili); moshi (-ingi, -litoka).

10. Переведите:

1. В тот день радио Найроби объявило, что праздник национальных танцев начнется ровно в 10 часов утра. 2. Ты можешь остановить любой проезжающий автомобиль и доехать до города. 3. Осмотрев машину, водитель понял, что лопнул приводной ремень. 4. Сначала пассажиры автобуса не обращали внимания на стук двигателя, но увидев много дыма, шедшего из-под капота, очень удивились. 5. Мы считаем, что наша поездка была отменена по вине водителя, который плохо подготовил свой автомобиль. 6. Вода уже закипела, сними чайник с плиты (*огня*). 7. Автобус наехал на камень, который отскочил и ударился о капот. 8. К сожалению, эта дорога очень плохая, на ней много рытвин, выберите любую другую дорогу, которая покрыта гравием (*маленькими камнями*). 9. Дети наблюдали за мастером, чинившим автомобиль, а затем приветствовали его аплодисментами.

11. Подтвердите или опровергните следующие утверждения, опираясь на содержание текста:

1. Wanafunzi bora wa shule walichaguliwa kwenda mjini kwa ajili ya kutembelea nyumba ya makumbusho. 2. Mnamo siku ya safari wanafunzi wachache walichelewa kuamka, kwa hivyo waliikosa safari ya kwenda Nairobi. 3. Dereva wa gari aliona haya kwa sababu ya kuchelewa mno. 4. Gari lilikuwa na mafuta ya kutosha siku hiyo. 5. Dereva alipiga honi kwa ajili ya kuwashangilia madereva wa magari mengine yaliyopita njiani. 6. Kishindo cha kwanza kilitokea kwa sababu ya gari kukanyaga jiwe. 7. Mwalimu alidhani kuwa kulikuwa na sababu nyingine ya kishindo hicho. 8. Kishindo cha pili kilifuata wakati wanafunzi walipofika mjini. 9. Sababu ya kishindo cha pili ilikuwa ni kukatika kwa ukanda wa gari. 10. Kifuniko kilitupwa juu kwa nguvu ya maji yaliyochemka. 11. Dereva alikuwa na ukanda wa akiba, kwa hivyo aliweza kulitengeneza gari upesi. 12. Mwalimu na wanafunzi walitosheka na safari yao.

12. Переведите вопросы и дайте ответы на суахили:

1. Почему школьники решили поехать в Найроби? 2. Как водитель объяснил причину своего опоздания? 3. Зачем школьники остановились, проехав около часа? 4. Почему

водитель остановил машину во второй раз? 5. Что сделал водитель, услышав удар в передней части автомобиля? 6. Он понял настоящую причину этого удара? 7. Зачем водитель решил остановить проезжавшую машину? 8. В котором часу он вернулся из города? 9. Почему дети захлопали в ладоши? 10. По какой причине преподаватель решил отменить поездку в город? 11. Что вы можете сказать о водителе этого автомобиля?

13. Изложите коротко на суахили содержание рассказа "Kuvunja safari".

14. Переведите следующий текст:

Maneno mapya

-kata shauri решать (*что-л. сделать*)
-kwea восходить, взбираться
-ota ndoto 1)видеть сон 2)мечтать
ruhusa/ ruhsa (-) разрешение, позволение
blanketi (ma-) одеяло
kibiriti/ kiberiti (vi-) спичка
mafuta ya taa керосин
alfajiri (-) рассвет, утренняя заря (≈*в 4-5 часов*)
woga (ед.) страх, боязнь
-fungamana сплетаться, переплетаться
-jikaza брать себя в руки, собираться с силами
-sinzia дремать; засыпать
-hifadhi 1)хранить, беречь 2)защищать

Kupanda mlima Kilimanjaro

Siku moja vijana walizungumza habari za mlima Kilimanjaro na wakakata shauri kuukwea mlima huo. Waliota ndoto kuona vilele vyake maarufu ambavyo vinajulikana kwa majina ya Kibo na Mawenzi. Basi kila mtu akaenda kwa wazazi wake kutaka ruhusa, kwa bahati nzuri wazazi hawakuwa na taabu yo yote na mara wakatoa ruhusa yao.

Vijana walichukua siku saba kujitayarisha. Walikusanya mablanketi, chakula cha siku tatu, vibiriti pakiti tatu, sufuria mbili, jiko la kupikia na mafuta ya taa. Wakaanza safari yao siku ya nane alfajiri. Njia ilikuwa na miti iliyofungamana na kufanya giza. Walikuwa na woga mwingi ndani ya msitu huo lakini walijikaza na kuendelea na safari.

Usiku ulipoingia walikaa chini ya mti na kupika chakula chao. Walipomaliza kula walianza kusinzia, wakajificha kwenye nyasi na kulala mpaka asubuhi. Waliamka na kuendelea na safari yao. Jua lilikuwa kali sana lakini halikuwachoma kwa sababu miti iliyofungamana iliwahifadhi. Saa sita za mchana walifika chini ya mlima Kilimanjaro. Wakavaa makoti yao na viatu halafu wakaanza kupanda juu. Walichoka sana walipofika kileleni. Theluji ilifunika kilele chote na kwa hivyo baridi ilikuwa kali sana hata makoti yao hayakufaa kitu.

Maelezo

1. ...walichukua siku saba kujitayarisha "..., на подготовку у них ушло семь дней". Сравните другую возможную конструкцию с тем же значением: kujitayarisha kuliwachukua siku saba.

2. Глагол -choma "жарить", "печь" имеет дополнительные значения – "припекать", "обжигать" и т.п.

3. ... makoti hayakufaa kitu "... пальто не спасало" (*букв.* "пальто не годилось ни на что"). Слово kitu в подобных конструкциях с отрицанием имеет обобщающий смысл: Shauri lake halikunisaidia kitu "Его совет ничуть не помог мне; Kuja kwenu hakutabadili kitu "Ваш приход ничего не изменит".

Mazoezi

15. Дайте русские эквиваленты:
-kata shauri kupumzika kisiwani; -ota ndoto kuukwea mlima maarufu; -pata ruhusa ya kiongozi kwenda livu; -ondoka bila ya kupewa ruhusa; -tetemeka kwa woga; -shikwa na woga; -jifunika kwa blanketi; -washa moto kwa kiberiti; -jikaza na kupiga mbizi; mimea iliyofungamana; -sinzia kwenye kiti cha raha; sheria zinazohifadhi wanyama wa porini.

16. Переделайте конструкцию предложений по модели:
Tulichukua saa moja kuyafanya mazoezi yote >
Kuyafanya mazoezi yote kulituchukua saa moja.

1. Watalii walichukua wiki moja kuukwea mlima ule. 2. Nilichukua dakika 40 kupika kitoweo cha nyama. 3. Fundi alichukua saa moja na nusu kulikagua gari langu. 4. Utachukua muda mrefu kujifunza vizuri lugha ya Kifaransa. 5. Polisi walichukua siku nyingi kumtafuta mwizi. 6. Tulichukua robo saa tu kufika ubalozini. 7. Mama huchukua siku mbili kuusuka mkeka mmoja.

17. Переведите:

1. Мы решили выехать на рассвете, так как дорога до заповедника займет у нас 8 часов. 2. В темноте они потеряли спички и не смогли приготовить себе никакой еды. 3. Свет не проникает (*не проходит*) сюда из-за переплетенных деревьев, поэтому в этом лесу нет никаких высоких растений. 4. Дедушка задремал в уютном кресле и ничего мне не ответил. 5. Вам следует взять себя в руки и преодолеть (*оставить*) свой страх. 6. Любой ребенок мечтал бы посетить дальние страны или взобраться на самую высокую гору.

18. Напишите на суахили окончание рассказа из упражнения 14.

* * *

Mazoezi ya kujiandaa kusikiliza hadithi

Maneno mapya

jirani (ma-; -) сосед
[-a] jirani соседний; близкий
ila за исключением; кроме как; только
mlafi (wa-) обжора, чревоугодник
-songa ugali готовить кашу
-nukia хорошо пахнуть, благоухать
mwiko (miiko) половник
-pakua перекладывать пищу из кастрюли на тарелку, подавать пищу на стол
-inua поднимать
chungu (vy-) горшок (для варки пищи)
-bonyea сплющиваться
-mwaga выливать, разливать, проливать

19. Дайте русские эквиваленты:

-ishi kama majirani wema; duka jirani; kunukia kwa maua; mafuta mazuri yanayonukia sana; -pakua wali; -bonyea kichwani; pipa

lililobonyea; -inua mizigo; -inua mkono wa kushoto; -tengeneza vyungu; -mwaga mafuta; -mwaga kahawa mezani; -mwaga damu.

20. Подберите синонимы или объясните на суахили значение следующих слов:

jirani; mchoyo; mlafi; -songa ugali; -nukia; -pakua chakula; -inua; chungu; -piga hodi; -funika chakula.

21. Дайте эквиваленты на суахили:

относиться друг к другу с любовью; быть обжорой; попросить огня; погасить огонь; услышать стук в дверь; накрыть еду; стукнуть половником; голова сплющилась; вылить воду на голову прохожего.

22. Дополните словосочетания известными вам словами:

-mwaga chai, -mwaga ...	-zima moto, -zima ...
-inua chungu, -inua ...	-piga begani, -piga ...
-pakua nyama, -pakua ...	kofia nyeupe, kofia ...

23. Переведите:

1. Licha ya Juma na Amosi kuwa majirani, hawapendani kabisa. 2. Wanafunzi wote wa darasa letu ni hodari sana ila mmoja ni mvivu. 3. Kila mara ninapofika nyumbani kwake ninamkuta anaangalia televisheni tu. 4. Mafuta mazuri yako yananukia sana. 5. Ameuzima moto akaanza kutupakulia chakula. 6. Mwalimu amesimama na kitabu mkononi. 7. Mpishi hakunipa mwiko wala sahani. 8. Mtoto wa jirani alimpiga mwanangu kichwani na kumwagia maji baridi. 9. Ujivalie ile kofia nyekundu, utaonekana mrembo sana. 10. Mimi bado nina lile gauni jeupe linalofanana na mawingu meupe.

24. Замените отрицательную форму глаголов утвердительной:

hamkuwa marafiki; hatukupendana; sikuwa mchoyo; tusipomkuta; usisonge ugali; hakinukii vizuri; hawakupewa chakula; moto usiozimwa; hatarudi; hujapakua wali; hakuomba mwiko; sisikii hodi; usifunike chungu; usipojua ukweli; hakubonyea kichwani; sitainua birika lile; bado hatuna moto.

25. Согласуйте существительные со словами в скобках: moto (-le, -ekundu); ugali (-ako, -tamu); chungu (-ingine, -o -ote); jirani (-o -ote, -zuri); miiko (-ingi, -refu); kofia (-o -ote, -a kupendeza); njiani (-ao, -le); mabega (-ote, -wili).

26. Переведите:

1. Мы с братом очень любим друг друга, только редко встречаемся. 2. Салюм зашел к нам в общежитие попросить словарь. 3. Еда на кухне очень вкусно пахла, и я почувствовал голод. 4. Почему повариха еще не подала нам рыбу? 5. Услышав стук в дверь, хозяйка погасила огонь и пошла открывать. 6. Он не дал ему ни огня, ни спичек. 7. Бабушка взяла горшок с кашей и вылила всю кашу в миску. 8. У меня до сих пор есть то ружье, которое я получил в подарок от соседа.

Kusikiliza hadithi

- Прослушайте текст полностью.
- Повторите в паузах фразы вслед за диктором.
- Закончите предложения вместо диктора.
- Задайте друг другу вопросы на суахили по содержанию прослушанного текста и дайте на них ответы.
- Ответьте на суахили на вопросы диктора.
- Изложите письменно на суахили содержание текста.

* * *

Mazoezi

27. Переведите следующий текст и задайте друг другу как можно больше вопросов по его содержанию:

rubani (ma-) пилот, летчик; **ukungu (ед.)** туман

Ajali ya ndege

Ndege moja ilikuwa angani. Rubani aliwaambia abiria, “Mnaweza kuvuta sigara sasa”. Baada ya muda mfupi alitoa sauti kubwa akisema, “Zimeni sigara zenu upesi na fungeni kanda mara moja.” Watu wote wakashikwa na woga. Ndege ilikuwa juu ya mawingu, ikaanza kushuka upesi upesi. Chini ya mawingu kulikuwa na ukungu na rubani hakuweza kuona kiwanja cha ndege. Alijaribu kuzunguka lakini ndege ilizidi kushuka.

Baadaye alitua shambani. Abiria wote walimshangilia. Rubani huyo alikuwa hodari sana. Alitua salama licha ya matatizo yote. Hakuna mtu ye yote aliyeumizwa. Ndege ilipotua, abiria wote walitoka wakitetemeka. Wote walimshika rubani mkono na kumshukuru kwa uhodari wake. Watu wengi walikuja kuona ajali hii ya ndege. Walishangaa walipoona kuwa wasafiri wote walikuwa salama kabisa.

28. Переведите диалог и разыграйте его в лицах:

Maneno ya kusaidia tafsiri

Umeadimika!	Ты совсем пропал!
Hata!	Ничуть!
Umebahatika!; Bahati yako!	Тебе повезло!
Wapi!	Куда там!
(kazi n.k.) **chungu nzima**	полно (*работы и т.д.*)
Tutaonana!	Увидимся!

А: Ты совсем пропал. Где ты был?
Б: Мы были в отпуске. Ездили на машине на север. Там есть очень красивые озера.
А: А разве там не холодно?
Б: Ничуть. Солце пекло очень сильно. Мы плавали в озере, загорали (*лежали на солнце*).
А: Да, повезло тебе. Ты выглядишь вполне отдохнувшим.
Б: А ты? Уже был в отпуске?
А: Куда там! У меня полно работы.
А: Мне очень жаль.
Б: Ничего, отдохну в следующем году. Извини, мой автобус идет. Еще увидимся.

29. Расскажите о какой-нибудь вашей поездке:

1. Ulikwenda wapi? 2. Safari ilitokea lini? 3. Ulitumia njia gani ya usafiri? 4. Ulisafiri na nani? 5. Vifaa gani ulichukua safarini? 6. Ulikaa huko kwa muda gani? 7. Je, ulipiga picha zo zote? 8. Hali ya hewa ilikuwa nzuri au mbaya? 9. Safari yako ilikuwaje?

SOMO LA NNE
Лексическая тема “Выбор профессии”

Грамматика

1. Выделительная связка **ndi-**.
2. Местоимения **hivi, hivyo, vile** в функции наречий образа действия.

Выделительная связка ndi-. Неизменяемая основа ndi- оформляется релятивным показателем соответствующего класса так же, как и указательные релятивные местоимения “этот упомянутый”. Поэтому эту связку называют также уточняющим (выделительным) местоимением: ndicho kitabu hicho “именно эта книга”.

класс	ед.ч.	мн.ч
m-/wa-	ndiye	ndio
m-/mi-	ndio	ndiyo
ji-/ma-	ndilo	ndiyo
ki-/vi-	ndicho	ndivyo
n-/n-	ndiyo	ndizo
u-/n-	ndio	
ku-	ndiko	
(pa-/ku-/mu-)	ndipo/ndiko/ndimo	

В сочетании с личными абсолютными местоимениями выделительная связка образует следующие формы: ndimi “именно я”, ndiwe “именно ты”, ndisi “именно мы”, ndinyi “именно вы”.

Обычно выделительная связка употребляется в сочетании с указательными местоимениями: ndiye mtu yule “именно тот человек”.

В зависимости от позиции в словосочетании акцентируется тот или иной его член:

Ndicho kitabu chake hiki “именно эта его книга”;

Kitabu ndicho chake hiki “это и есть его книга”;

Kitabu chake ndicho hiki “его книга и есть как раз эта”.

Как видно из примеров, выделительная связка выступает в качестве сказуемого именного предложения: Nani aliingia hapa? Ndimi “Кто вошел сюда? Это я (именно я, а не кто другой)”. К такому именному предложению может присоединяться определительное придаточное предложение, в глаголе-сказуемом которого релятивный формант совпадает с релятивом выделительной связки: Hawa ndi*o* watu tana*o*wangoja “Эти люди именно те, которых мы ждем”. На русский язык такие сложно-подчиненные суахилийские предложения могут переводиться простыми глагольными: Hawa ndi*o* watu tuna*o*wangoja “Именно этих людей мы ждем”.

Указательные местоимения, согласованные по классу ki-/vi-, т.е. hivi, hivyo, vile выполняют в предложении функции наречий образа действия: usiseme hivi “не говори так”; fanya hivyo ulivyoambiwa “делай так, как тебе сказано”. Уточняющее местоимение этого класса, состоящее из выделительной связки ndi- + релятив, т.е. ndivyo (в сочетании с hivyo) также выступает в функции наречия образа действия, передавая значение “именно так”, “именно таким образом”: Tulijenga nyumba hii ndivyo hivyo “Мы построили этот дом именно таким образом”.

Mazoezi

1. Дополните словосочетания связкой ndi- по образцу и объясните, как меняются смысловые оттенки в зависимости от позиции данной связки. Образец:

wageni wetu hawa > *ndio wageni wetu hawa,*
> *wageni ndio wetu hawa,*
> *wageni wetu ndio hawa;*

mti huu; shule yetu; ukungu mnene; mwalimu wetu yule; matunda haya mabivu; karatasi zile nyeupe; kikapu hicho cha babu; mkoa wetu; mafundi hawa bora; ufunguo ule; vinywaji vya baridi; meno ya juu; milango yote; wakati huu; madereva wale hodari.

2. Дополните предложения локативной выделительной связкой ndipo/ ndiko/ ndimo. Образец:

Anaishi huko > Huko ndiko anakoishi

Tutaondoka kesho > Kesho ndipo tutakapoondoka

1. Walikwenda huko. 2. Tutasimama hapa. 3. Utalala chumbani humu. 4. Nilimwona jana. 5. Daktari atakuja jioni. 6. Mkulima amepanda hapa mbegu zake. 7. Mamba wanaishi mtoni humu. 8. Mkutano utafanywa siku ya Jumamosi. 9. Binadamu wa kale waliishi huko. 10. Mboga zote zinahifadhiwa vizuri ghalani humu.

3. Переведите:

1. Именно этот словарь мой. 2. Они зарезали как раз ту жирную овцу. 3. Наш багаж именно этот. 4. Это как раз та дорога, которая ведет в город. 5. Именно соседи принесли нам билеты в музей. 6. Как раз это время мне подходит. 7. Мы встретимся именно там. 8. Я положил ключи от твоей машины именно в этот стол. 9. Это как раз то самое место, которое выбрано для строительства многоэтажного дома. 10. Именно в июле начнутся вступительные экзамены в этот вуз. 11. Мне не нравилось как раз это его высокомерие. 12. Дети потеряли мяч именно в этой яме.

4. Поменяйте смысл предложений на отрицательный и переведите их. Образец:

Hiki ndicho kisu nilichoomba > Hiki sicho kisu nilichoomba

1. Mtu huyu ndiye rubani atakayeendesha ndege yetu. 2. Huu ndio umri unaofaa kwa kusoma katika chuo kikuu hiki. 3. Hali ya hewa ya Afrika ya mashariki ndiyo inayodhaniwa kuwa nzuri kwa afya. 4. Sheria hizi ndizo zinazoheshimiwa na kabila hili. 5. Bondeni humu ndimo mbuzi wake wanamochungwa. 6. Hili ndilo shamba utakalopalilia. 7. Huyu ndiye msichana ambaye ningependa kumwoa. 8. Hapa ndipo mahali pa kuvuta sigara. 9. Watu hawa ndio walioita teksi.

5. Переведите:

1. Tunalima hivi kwa sababu tunataka migomba yetu iote haraka. 2. Fundi ametekeleza kazi zote vile alivyoambiwa. 3. Ndivyo hivyo wanawake wa Tanzania wanavyosonga ugali. 4. Mbona bei za mboga zimeongezeka hivi siku hizi? 5. Vijana hupenda

kusherehekea harusi zao ndivyo hivyo. 6. Siwezi kufahamu kwa nini kaka yangu hakutenda vile ulivyomfundisha. 7. Angalia vizuri, madirisha ofisini hapa hufungwa hivi. 8. Hatupendi vile babu yetu anavyotunzwa na mwuguzi huyu. 9. Ndege iliruka hivyo kwa sababu ya ukungu mnene. 10. Hivyo ndivyo wenyeji walivyotusaidia kuuvuka mto ule.

6. Переведите:

A/ 1. Это не те люди, которых мы ищем. 2. Это не его голос. 3. Туристы не здесь будут отдыхать. 4. Этот пассажир не тот, кто хочет поменять свой билет. 5. Это не тот напиток, который я просил. 6. Это не те новости, которые мы все ждали.

B/ 1. Почему они так думают? 2. Он так сказал. 3. Львы охотятся именно так. 4. Не смотри так на меня. 5. Мы перевели предложение именно так. 6. Мама готовит булочки таким образом. 7. Они построили себе дом именно так. 8. Давай считать именно таким образом. 9. Не веди машину так быстро. 10. Те цветы пахнут именно так. 11. Это озеро было обнаружено именно таким образом. 12. Как ты сдал экзамены? 13. Как мы поедем в город, на машине или автобусом?

Maneno mapya

mfugaji (wa-) фермер, скотовод
ufugaji (ед.) животноводство, разведение (животных)
mchungaji (wa-) пастух
maana (-) 1)смысл, значение, суть 2)потому что
mwiba (mi-) шип, колючка
malisho (мн.) пастбище, выпас
ndama (-) детеныш домашнего животного; молодняк
mkuki (mi-) копье
upinde (pinde) 1)лук 2)дуга, изгиб
hasara (-) 1)ущерб, убыток 2)вред
ngozi (-) кожа, шкура
mali (-) 1)имущество, собственность 2)богатства
-stawi 1)успешно произрастать 2)процветать, преуспевать
-udhi беспокоить, докучать
-tisha пугать, устрашать
-kama выдавливать; доить
-himiza торопить, поторапливать

mshale (mi-) стрела
jike (ma-) самка
dume (ma-) самец
chuma (vy-) железо, металл
siagi (-) сливочное масло
samli (-) топленое масло

-karipia ругать; упрекать
-chuna сдирать, снимать (*кожу, шкуру*)
-kausha высушивать, сушить
-kauka сохнуть, высыхать

Kazi ya mjomba

Mwaka jana nilikwenda kumtazama mjomba wangu anayekaa mbali sana na mji wetu, katika nchi ya wafugaji ng'ombe. Ufugaji ndio kazi yake. Mjomba ana ng'ombe wengi sana, hawapungui mia tatu. Tena ana mbuzi wengi, lakini hana kondoo. Asema ya kwamba kondoo hawasitawi katika nchi yake, maana iko miiba mingi inayowaudhi kwa sababu ya manyoya yao marefu.

Kila asubuhi ng'ombe hupelekwa malishoni na ndama hupelekwa mahali pa peke yao pamoja na mbuzi. Wachungaji huchukua mikuki na pinde pamoja nao kwa sababu wako simba katika nchi hii. Usiku mmoja simba aliingia katika zizi la ng'ombe, akawaua ng'ombe wawili. Lakini hakuwala, maana mjomba alisikia kelele, akatoka mbio akapiga bunduki yake, akamtisha yule simba, na simba akakimbilia porini.

Ng'ombe jike hukamwa maziwa kila asubuhi kabla ya kwenda malishoni, na baada ya kurudi jioni ndipo hukamwa tena. Mjomba anapata maziwa mengi sana kila siku, lakini hayatumii yote. Mjomba ni hodari sana kwa kazi, kila mara hutembea kuwahimiza watu wake na kuwatazama wasiharibu kazi. Watu wale wanaokama maziwa wanakaripiwa mara kwa mara, maana mjomba aliwaambia lazima wanawe mikono kabla hawajaanza kuwakama ng'ombe maziwa. Tena aliwaambia ya kuwa vyombo vyote vinavyotumiwa lazima visafishwe kwa maji ya moto. Lakini watu husahau kufanya hivyo, au labda ni wavivu tu.

Mzungu mmoja anakaa karibu, naye kila siku hupeleka motokaa yake kubwa kuchukua maziwa. Katika motokaa yapo mapipa makubwa ya chuma, na maziwa yote hupimwa na kutiwa humo. Anapeleka motokaa kila mahali pa karibu kukusanya maziwa ya wenyeji. Amepatana nao kuyanunua maziwa yote yasiyotakiwa

nao. Hupata maziwa mengi sana kila siku na watu wake hufanya siagi na samli.

Siku nyingine mjomba huchinja ng'ombe, lakini hachinji ng'ombe ambao ni wadogo. Asema ni hasara kufanya hivi kwa sababu hawana nyama ya kutosha. Ni bora kuwaacha mpaka wawe wakubwa, ndipo wanapokuwa na nyama nyingi. Tena hachinji ng'ombe jike kwa sababu ndio wanaozaa, tena ndio wanaotoa maziwa. Anachinja ng'ombe wasiozaa na madume.

Ngozi za ng'ombe ni mali kwa sababu zinaweza kuuzwa kwa bei nzuri. Mjomba aliniambia ya kuwa watu wengine hufanya ujinga sana, kwa sababu wanapochuna ngozi za ng'ombe huziharibu na kuzitoboa kwa kisu. Tena hawazikaushi vizuri. Lakini mjomba hafanyi hivi. Yeye anaangalia sana wakati ngozi zinapochunwa. Kila mara anatumia kisu kikali. Halafu huondoa mabaki yote ya nyama na mafuta. Baada ya hapo ndipo anapoziweka ngozi kivulini ili zikauke vizuri kwa polepole.

Watu wanaonunua ngozi za mbuzi na ng'ombe za wafugaji wengine husema ya kuwa ngozi nyingi hazifai kitu, kwa sababu zimetoboka, tena hazikukaushwa vizuri.

Maelezo

1. Слово nchi "страна" имеет дополнительные значения "местность", "район", "земля" и т.п.

2. Союзам kwamba и kuwa может предшествовать притяжательный формант ya: alisema ya kwamba ... "он сказал, что ..."; nilidhani ya kuwa ... "я подумал о том, что ...".

Mazoezi

7. Найдите в тексте суахилийские эквиваленты следующих словосочетаний:
съездить навестить дядю; край скотоводов; не менее трехсот; колючки досаждают им; отправлять на пастбища; специально отведенные для них места; вспугнуть льва; доить коров; поторапливать своих работников; весь используемый инвентарь; мыть горячей водой; отправить машину за молоком; договориться о покупке излишка молока; производить

сливочное и топленое масло; так делать невыгодно; шкура коров - ценная вещь; поступать глупо; продырявливать ножом; плохо высушивать; внимательно наблюдать за процессом сдирания шкуры; убрать остатки мяса и жира; шкура ни на что не годится.

8. Дайте русские эквиваленты:

mfugaji kuku; ufugaji wa ng'ombe; ufugaji wa samaki; ufugaji wa kondoo; maana ya neno jipya; jambo la maana; -peleka ng'ombe malishoni; eneo la malisho; upinde na mishale; upinde wa njia; upinde wa mto; pipa la chuma; paa la chuma; hasara nyingi; -leta hasara kwa afya; hasara ya mali; -wa na mali nyingi; mali ya taifa; -poteza mali; koti la ngozi; viatu vya ngozi; -kausha ngozi ya mbuzi; -kausha samaki; mkate uliokauka; mto uliokauka; nchi inayositawi; kusitawi kwa miche shambani; kelele za kuudhi masikio; wadudu wa kuudhi sana; usiniudhi; sauti ya kutisha; wanyama wa kutisha; -kama ng'ombe; -kama mbuzi maziwa; -himiza wafanya kazi; -himiza mpishi; -karipia mwana; maneno ya kukaripia.

9. Запомните словосочетания и составьте с ними предложения:

-tia maanani	принимать во внимание
-tia hasara	наносить ущерб
-pata hasara	нести убытки

10. Образуйте производные формы следующих глаголов и переведите их:

стативная: -fuga, -chunga, -udhi, -tisha, -kama, -chuna, -mwaga, -paramia, -palilia, -okoa, -vuka, -nyanyua, -hifadhi, -inua, -zima, -linganisha, -ziba;

взаимная: -himiza, -karipia, -chinja, -simulia, -tema mate, -sifu, -faa, -shangilia, -tambua, -vuta, -gonga, -umiza, -kagua, -kumbatia.

11. Замените подчеркнутые глаголы антонимами:

1. Kila mara humkaripia mwanawe anapomsaidia katika kupalilia migomba. 2. Katika safari ile tulipoteza mali nyingi. 3. Mkulima amesahau kumkama ng'ombe wake maziwa asubuhi hiyo. 4. Ng'ombe wamepungua sana katika zizi la mfugaji yule. 5. Ngozi za mbuzi wangu huuzwa kwa bei nzuri sana. 6. Aliposikia kelele za marafiki aliparamia mtini kwa haraka. 7. Nilimwomba dereva wa teksi kuizima injini.

12. Ответьте на вопросы по содержанию текста:

1. Mjomba ana ng'ombe kiasi gani? 2. Kwa nini hafugi kondoo? 3. Wachungaji huchukua mikuki, pinde na mishale pamoja nao kwa ajili gani? 4. Mjomba hupata nini kutokana na ng'ombe na mbuzi wake? 5. Kwa nini watu wanaokama ng'ombe maziwa hukaripiwa mara kwa mara? 6. Wenyeji huyatumiaje maziwa yasiyotakiwa nao? 7. Mjomba huchinja wanyama gani? 8. Mbona ngozi za ng'ombe na mbuzi zinazouzwa na wafugaji wengine si nzuri sana? 9. Kwa nini ng'ombe na mbuzi ni mali kubwa kwa mfugaji?

13. Перескажите текст на суахили.

14. Переведите:

1. В прошлом месяце я ездил навестить друга, который живет в тех краях, где развито животноводство. 2. У меня много хороших друзей, не менее восьми, и именно они всегда помогают мне в трудную минуту. 3. Именно разведение длинношерстных пород овец процветает в их краях. 4. Я не сажаю эти цветы в своем саду из-за их колючек, несмотря на то, что они издают чудесный аромат. 5. Местные жители охотятся на диких животных с помощью лука и стрел, иногда используют копья. 6. Дядя выстрелил из ружья как раз в тот момент, когда лев пытался схватить теленка. 7. Наш хозяин очень строгий человек, всегда внимательно следит, как мы работаем, и время от времени подгоняет нас. 8. Руководитель лаборатории сказал, чтобы все рабочие инструменты тщательно мылись в горячей воде. 9. Все остатки топленого масла помещаются в металлический сосуд и отправляются на

склад. 10. Мы договорились с фермерами покупать у них овчину по низкой цене. 11. Очень невыгодно забивать молодняк, поскольку у них еще очень мало мяса. 12. Все очень хвалят шкуры животных, которые продает наш сосед, потому что они все цельные (*в них совсем нет дырок*) и хорошо высушены.

15. Прочитайте следующий диалог в лицах и переведите его. Предварительно ознакомьтесь с новой лексикой:

Maneno mapya

ghafula/ ghafla неожиданно, вдруг
ubishi (ед.) спор, разногласия
-zuka возникать, появляться
maiti (-) умерший человек, труп
mwanahewa (w-) летчик, пилот
mgongo (mi-) спина, спинной хребет
uti wa mgongo 1)позвоночник 2)основа, стержень
akina/ kina (-) родня, семья
jamaa (-) 1)родственник, член семьи 2)товарищ, приятель
mhandisi (wa-) инженер
ubaguzi (ед.) неравенство, дискриминация
uhuru (ед.) независимость, свобода
-tegemea 1)зависеть 2)надеяться, рассчитывать
-hitimu заканчивать, завершать
kasi (-) быстрота, скорость
-kimbiza 1)обращать в бегство 2)гнать, гнаться
mbayuwayu (-) ласточка

Kazi nzuri ni ipi?

Siku moja baada ya masomo vijana wanne walielekea nyumbani kwa pamoja. Ghafula njiani ukazuka ubishi mkali juu ya kazi nzuri ni ipi. Mazungumzo yao yalikuwa hivi:

Sendeki: Mimi naona udaktari ndio kazi bora kuliko zote hapa duniani.

Kimwaga: Loo! Kazi gani hiyo? Kila siku kushika maiti! Hatari sana. Ualimu ndio kazi pekee inayoweza kusifiwa kwa kila njia.

Asha: Ngoja mimi niwaambie! Nyinyi nyote hamjui kitu. Kazi ambayo ni bora kuliko zote ni urubani tu. Kazi yako wewe ni kuruka angani kama mbayuwayu. Hivyo, unaitwa mwanahewa.

Lazaro: Ebu kwanza niwaulize kila mmoja kati yenu. Je, daktari anaweza kufanya kazi akiwa na njaa?

Sendeki: Hapana, ila .....

Lazaro: Hata mwalimu pia hawezi kufundisha akiwa na njaa. Wala rubani hawezi kuruka angani akiwa na njaa. Nyote nyie mnamtegemea mkulima kwa maisha yenu yote. Kwa hivyo, kazi ya ukulima ndio hasa uti wa mgongo wa maisha yetu.

Basi watu wengine wenye huruma walifikiri mambo hayo, wakajaribu kuvumbua namna ya vitabu vinavyoweza kusomwa na vipofu wanaokaa daima gizani. Wakafikiri, kama wangeweza kuvumbua mtindo wa kutengeneza vitabu ambavyo vipofu wangeweza kuvisoma. Wakawaza wakakumbuka uwezo wa vidole vya vipofu, na mwishowe wakafaulu.

Mtu wa kwanza aliyeshughulika katika kazi hii ya huruma alijaribu namna ya kuchora herufi juu ya mbao. Mtu mwingine aliyekuwa mwalimu katika nchi ya Ufaransa alivumbua mtindo mwingine wa kufanya herufi za risasi, lakini alikuwa hana fedha za kufaulu katika kazi hii akaiacha.

Njia nyingine zikajaribiwa bila ya kufaulu mpaka Mfaransa mmoja alivumbua mtindo wa kuzitumia alama za nukta na mistari badala ya herufi. Baadaye mtu jina lake Louis Braille alianza

kushughulika sana katika kazi hii. Akazidi kushiriki katika mambo hayo mpaka katika mwaka 1834 akafaulu, akatengeneza namna ya kupiga chapa vitabu vinavyoweza kusomwa na vipofu, ndivyo vinavyotumiwa siku hizi.

Maelezo

1. ... kwa kumpapasa uso wake "... ощупывая его лицо". Обратите внимание, что объектный показатель в глаголе -papasa согласован не по классу существительного uso, а по 1-му классу. Это происходит в тех случаях, когда речь идет о части и целом, например: Walimchuna simba ngozi yake "Они содрали со льва шкуру"; Daktari amemtibu mgonjwa jicho lake "Врач вылечил глаз больного"; Wanakijiji waliamua kumkata mwizi mkono wake wa kulia "Жители деревни решили отсечь вору его правую руку". В таких случаях не требуется употребление направительной формы глагола, сравните: Mama alimkata mtoto nywele "Мама подстригла ребенку волосы", но Mama alimkatia mtoto shati "Мама укоротила ребенку рубашку" (где shati "рубашка" не является неотъемлемой частью ребенка).

Mazoezi

16. Запомните следующие выражения и составьте с ними предложения:

-waza moyoni думать про себя
siku za usoni будущее; в будущем
-mtakia mtu kila la heri na baraka желать (*кому-л.*) всего наилучшего

17. Переведите:

1. Amezivuka taabu zote kwa baraka ya Mungu. 2. Uso wake ulionyesha furaha nyingi, nikawaza moyoni kuwa labda amefaulu kuipita mitihani yote. 3. Mamangu hupika kuku kwa mtindo wake maalum. 4. Unaweza kuandika japo mstari mmoja kwa Kichina? – Wapi! Nashindwa kuchora hata herufi moja. 5. Ghafula taa zote sebuleni zimezimika, tulikuwa hatuna budi kutoka nje kwa kupapasa kila kitu kilichotuzunguka. 6. Katika mashindano ya mbio

mwenzangu alinizidi kwa nukta chache tu. 7. Wageni wote walioshiriki kwenye sherehe walimtakia mwenyeji kila la heri na baraka. 8. Majirani walikata shauri kujenga daraja mpya kwa kushirikiana. 9. Katika lugha ya Kiarabu hutumiwa alama maalum badala ya herufi za kawaida. 10. Mtumishi aliombwa kwenda livu mwezi huu badala yangu.

18. Дайте эквиваленты на суахили:
школа для слепых; стать слепым; вымыть лицо и руки; иметь привлекательную внешность; благодарить бога; выбирать образ жизни; изобрести новый способ печатанья; автомобиль нового образца; участвовать в соревнованиях по волейболу; принять участие в диалоге; потрогать своими руками; считать по секундам; осталось несколько секунд; вытянутая линия; черные и белые линии; изучать китайский язык вместо арабского; вместо меня; вместо вас; размышлять о будущем; думать про себя; содрать с овцы шкуру; вылечить больному уши.

19. Перескажите на суахили текст из упражнения 15.

20. Напишите на суахили сочинение на тему “Kitabu nikipendacho zaidi”, ответив на следующие вопросы:
1. Kitabu chako kinaitwaje? 2. Nani mwandishi wake? 3. Mwandishi huyu aliishi lini, tena wapi? 4. Kitabu chake hicho kimeandikwa kwa lugha gani? 5. Je, kitabu kinaeleza habari za maisha ya zamani au ya siku hizi? 6. Ni nani uliyempenda zaidi katika kitabu hicho? 7. Yeye ni mtu wa aina gani? Kwa nini amekuvutia? 8. Je, ulisoma vitabu vingine vya mwandishi huyo? 9. Vilikuwa vya kuvutia vilevile au la? 10. Je, wewe mwenyewe ungependa kuwa mwandishi? 11. Kama ungelikuwa mwandishi, ungeliandika juu ya nini?

* * *

Mazoezi ya kujiandaa kusikiliza hadithi

Maneno mapya

-gusa трогать, притрагиваться, [при]касаться
-fyatuka *зд.* захлопнуться
mnofu (mi-) мякоть, филе

-itikia отзываться, откликаться
-sogea приближаться, придвигаться
mtego (mi-) ловушка, капкан, западня

Mazoezi

21. Дайте русские эквиваленты:
-ita mtoto; -itikia ombi la mama; -gusa vitu; kitu kinapoguswa kinakamata; kitu usichokijua; mtego wa hatari; -inua mtego; mtego ukiguswa unafyatuka; -sogea kwenye meza; -sogea karibu ili kusikia vizuri; -tamani kula; -tamani kusoma; mnofu mnene; -kata mnofu wa nyama; -imba kwa sauti kubwa; -ja haraka; mwanangu, huna akili.

22. Дайте эквиваленты на суахили:
позвать друзей; не дотрагиваться до предметов; хватать мышей; мышеловка; быстро откликнуться; подойти к двери и войти внутрь; выйти наружу; кусок рыбного филе; капкан захлопнулся; закричать во весь голос; поднять дверцу ловушки.

23. Закончите предложения:
1. Kukigusa kitu kuna maana ya ... 2. Mnofu ni kipande cha nyama au samaki ambacho ... 3. Mtoto anapomsikia mama akimwita, huitikia na kusema ... 4. Kusogea karibu na kitu fulani maana yake ni ... 5. Mtego umefyatuka ni sawa na kusema kwamba ...

24. Замените утвердительную конструкцию отрицательной:
A/ mtoto anayeitikia haraka; mtego unaowakamata wanyama; sauti inayojulikana; masikio yanayoumwa; mnofu uliokatwa; mwana anayemsikiliza mamake; kitu kinachofyatuka.
B/ maneno unayoyajua; sauti nilizozisikia; hatari wanayoileta; maelezo wanafunzi waliyoyasoma; mitego baba aliyoiweka; vitu watoto wanavyovikamata; mbao fundi anazozipasua.

25. Замените союз amba-релятивом в глаголе. Не забудьте про объектный согласователь:

kalamu ambazo unaziona; sauti ambayo mnaisikia; hatari ambayo wanaikabili; mlango ambao aliufunga; mnofu ambao niliununua; mama ambaye anamkaripia mwanawe; paka ambao wanaipenda minofu ya nyama; mitego ambayo baba anaifungua.

26. Переведите, употребив глагол с релятивом и объектным согласователем:
слова, которые мы хорошо помним; рассказы, которые они читают; предметы, до которых вы дотрагивались; опасность, которую они понимают; капкан, который принесли крестьяне; вопросы, которые задают журналисты; книга, которую сочинил известный писатель.

27. Сделайте словосочетания из упражнения 26 отрицательными и переведите их на суахили:

28. Переведите:
1. Однажды после уроков преподаватель позвал своих учеников и пригласил их погулять в лесу. 2. Когда они подошли *(приблизились)* к лесу, преподаватель сказал ученикам: "Здесь есть очень опасные растения, одни ядовитые, другие колючие. Не трогайте растения, которые вы не знаете". 3. Ученики откликнулись на слова преподавателя, сказав, что они все поняли. 4. Дети гуляли по лесу и слушали преподавателя, который рассказывал им об удивительных цветах, деревьях и кустарниках. 5. Вдруг один мальчик увидел неизвестное ему растение и подошел поближе, чтобы лучше разглядеть его. 6. Это растение было очень красивое, и он решил его потрогать. 7. Но растение оказалось колючим, и когда мальчик дотронулся до него, острые колючки причинили ему боль. 8. Он хотел заплакать, но вспомнил слова учителя, который просил учеников не трогать то, что они не знают.

Kusikiliza hadithi

- Прослушайте текст полностью.
- Повторите в паузах фразы вслед за диктором.
- Закончите предложения вместо диктора.

- Задайте друг другу вопросы на суахили по содержанию прослушанного текста и дайте на них ответы.
- Ответьте на суахили на вопросы диктора.
- Изложите письменно на суахили содержание текста.

* * *

Mazoezi

29. Запомните следующие выражения:

simu inatumika	телефон занят
hakuna jibu	телефон не отвечает
umekosea (nambari)	вы ошиблись (*номером*)
-pata mtu (kwenye simu)	дозвониться (*до кого-л.*)
subiri kidogo	[подождите] минуту
rudia (sema tena) tafadhali	повторите, пожалуйста
wewe nani?	кто спрашивает/говорит?

30. Переведите диалог и выучите его наизусть:

Mazungumzo ya simu

Lusia: Halo, maktaba ya chuo kikuu.
Meneja: Halo, nataka kuzungumza na mkuu wa maktaba yenu.
Lusia: Sema kwa sauti zaidi, sikusikii vizuri.
Meneja: Mkuu wa maktaba yupo?
Lusia: Hayupo. Ametoka sasa hivi, amekwenda mkutanoni. Naweza kukusaidia?
Meneja: Ndiyo, akija tafadhali mwambie anipigie 377 622.*
Lusia: Sidhani atarudi leo. Mkutano utamalizika jioni, akitoka atakwenda nyumbani.
Meneja: Basi asante, nitampigia kesho asubuhi.
Lusia: Haya, kwa heri.
(asubuhi ya kesho)
Lusia: Halo, 491 62.
Meneja: Nataka kuzungumza na mkuu wa Maktaba.
Lusia: Hebu subiri kidogo. Haya, sema naye.

---

* Как правило, номера телефонов называются по одной цифре: tatu saba saba и т.д.

Meneja: Halo, habari za asubuhi.
Mkuu: Salama, nani mwenzangu?
Meneja: Meneja wa duka la vitabu.
Mkuu: Ahaa, habari za siku nyingi?
Meneja: Safi, habari za mkutano?
Mkuu: Ulikuwa mzuri. Tulizungumza sana juu ya vitabu vipya. Basi, wasemaje?
Meneja: Nataka kufika ofisini kwako tuzungumzie masharti ya kuwauzieni vitabu vipya.
Mkuu: Unataka kuja leo?
Meneja: Sasa, kama una nafasi.
Mkuu: Njoo tu, bwana. Utanikuta.
Meneja: Haya, nitakuja.

31. Переведите следующие предложения:
1. Я хочу поговорить с главврачом. 2. Позовите, пожалуйста, Ахмеда. 3. Вы можете подождать минуту? 4. Я могу вам помочь? 5. Повторите, пожалуйста. 6. Говорите громче, я вас плохо слышу. 7. Передайте, чтобы он позвонил мне. 8. Я позвоню вам завтра утром. 9. Г-на В. нет на месте. 10. Г-н В. только что вышел. 11. Позвоните ему минут через десять. 12. Простите, кто его спрашивает? 13. Алло, это номер 935 72 82? 14. Вы ошиблись. 15. Его телефон не отвечает. 16. Я не мог тебе дозвониться вчера вечером. 17. Буду ждать твоего звонка. 18. Хорошо, договорились.

32. Составьте диалог на тему "Mazungumzo ya simu", используя выражения из упражнений 29 и 31.

SOMO LA SABA
Лексическая тема "У лжи короткие ноги"

Грамматика

Безличная форма глагола. Показатели именных классов помимо своего основного значения – маркирования имен существительных и формирования согласовательной цепочки – имеют дополнительные функции. Так, показатели 4-го класса ki-/vi- используются для образования наречных слов: kidogo "мало", vizuri "хорошо", kindugu "по-братски" и др.

Субъктный показатель 5-го класса единственного числа i- придает оформляемому им глаголу безличное значение. Семантика таких глаголов разнообразна, но чаще в безличной форме употребляются глаголы говорения, разрешения-запрещения, согласия-отказа, обещания, модальные глаголы и др.

Глагол может употребляться как в основной, так и в производных формах:

inafaa kusoma vitabu "следует читать книги",
imetangaz*wa* kwamba… "объявили, что…",
inawez*ekana* kufungua dirisha "можно открыть окно".

При этом глаголы в безличной форме спрягаются по всем временам и наклонениям и образуют отрицательные варианты:

i*na*tosha "достаточно",
ikumbukw*e* "стоит напомнить"
i*nge*kuwa vizuri "было бы хорошо"
*ha*iruhusiw*i* "не разрешается".

Mazoezi

1. Переведите предложения и выпишите все глаголы в безличной форме:
1. Imetangazwa kwamba kiwanda cha ngozi kitafungwa kwa sababu ya kutia hasara kubwa mito ya karibu. 2. Je, inawezekana kutumia kamusi wakati wa kufanya mazoezi haya? 3. Inapendeza sana kuogelea baharini kisha kulala pwani na kuota jua. 4. Kwanza inafaa kuijaza fomu hii, halafu kuipeleka kwa karani. 5. Inasemekana kwamba bunduki ya mtindo huu ilivumbuliwa na

bingwa wa Urusi. 6. Haiwezekani kuacha magari kwenye mlango wa kuingia benki. 7. Imearifiwa kwamba ajali ya moto katika bweni hili ilizuka kwa kosa la wanafunzi wenyewe. 8. Ingekuwa vizuri kwenda kuwatazama wazazi wakati wa likizo. 9. Haifai kuandika alama zo zote ndani ya vitabu mnavyovichukua kutoka maktaba. 10. Imeahidiwa kwamba shule mpya itafunguliwa ufikapo mwanzo wa mwaka wa masomo. 11. Hairuhusiwi kuingia katika chumba cha daktari ukivaa koti. 12. Imekatazwa kutupa takataka mahali hapa. 13. Ikumbukwe kwamba dawa hii ni kali sana, inafaa kuitumia mara moja tu kwa siku. 14. Imeamuliwa kwamba sherehe ya utamaduni wa kienyeji itafanyika mwakani. 15. Nikutilie maziwa zaidi? – Inatosha, asante.

2. Сделайте предложения отрицательными:

1. Inawezekana kuingia kiwandani humu bila ya kuwa na cheti malum. 2. Inafaa kuandika maneno yote mapya. 3. Ilikuwa vibaya kuficha habari za kweli. 4. Inatosha kuweka hapa pipa la maji moja tu. 5. Imejulikana vizuri kama karatasi imevumbuliwa na nani. 6. Iliarifiwa kuwa meli imeshafika bandarini.

3. Измените конструкцию предложений, поставив подчеркнутый глагол в безличную форму:

1. Walidhani kuwa mvua itakwisha upesi. 2. Watu wengine wanasema kwamba maua ya aina hii hayasitawi kwenye udongo wetu. 2. Mnaweza kuuvuka mto huu kwenye daraja lile la mbao. 4. Hatutaweza kupumzika Jumamosi ijayo kwa sababu kazi ni nyingi sana. 5. Wakuu wameahidi kwamba mishahara yetu itaongezwa. 6. Kutembea hapa kunapendeza sana. 7. Wanahitaji kununua kompyuta mpya. 8. Sote tumekubali kwamba mkutano utaanza saa sita za mchana. 9. Mnaweza kuvua samaki ziwani humu. 10. Hawajatangaza mchezo wa mpira utatokea lini. 11. Abiria wakumbuke kwamba hawaruhusiwi kufungua kanda zao mpaka ndege itakapotua.

4. Переведите, используя безличную форму глагола:

1. В вашем кафе можно брать еду на дом? 2. Здесь есть какое-нибудь место, где разрешено курить? 3. Только что объявили,

что из-за сильного тумана наш самолет приземлится в другом аэропорту. 4. Известно, что новую городскую больницу откроют к началу будущего года. 5. На этом шоссе запрещено ехать с большой скоростью. 6. Очень приятно гулять в парке после дождя. 7. Работая на компьютере, следует надевать специальные очки. 8. Говорят, что в этих горах очень много ядовитых змей. 9. Было бы хорошо съездить в заповедник в этом сезоне. 10. В библиотеке нельзя громко разговаривать.

Maneno mapya

maendeleo (мн.) развитие, прогресс
madhumuni (мн.) цель, намерение
makubaliano (мн.) 1)согласие 2)соглашение, договоренность
biashara (-) торговля, бизнес
hamu (-) желание, страсть
mahitaji (мн.) нужда, потребность
shaba (-) медь
dhahabu (-) золото
thamani (-) 1)цена, стоимость 2)ценность
utumiaji (мн.) использование, применение
tokeo (ma-) результат, итог; следствие
juhudi (-) 1)усилие 2)усердие, старание
baina ya между; среди
-hangaika суетиться; заниматься (чем-л.)
-rahisisha упрощать, облегчать
-vimbisha kichwa забивать/вскружить голову (*перен.*)
-jitapa хвастать[ся], хвалиться
-changanya 1)соединять 2)смешивать
-badilisha заменять, обменивать

Fedha si msingi wa maendeleo

Inajulikana na wote fedha ni kitu gani. Fedha inatumika mahali pengi na kwa madhumuni mbalimbali. Fedha inatumika kununua vitu madukani, sokoni na mahali pengine.

Fedha haikuanza kutumika zamani sana. Ina historia fupi. Kabla ya kugunduliwa fedha watu walibadilishana vitu. Hawakununua vitu kama sisi tunafanya leo, kwa sababu hawakuwa na fedha. Kama mtu alihitaji kitu fulani, basi alitafuta kitu kingine badala yake. Kisha alikipeleka kitu hicho kwa mtu mwingine

aliyekihitaji, na yule mtu alimpa kitu kingine badala yake. Kwa mfano, kama mtu alihitaji ng'ombe alimtafuta mtu mwenye ng'ombe na kumwomba wabadilishane ili yeye ampe mnyama mwingine kama vile mbuzi au kondoo. Wakati mwingine ilihitajika kuwa na mbuzi au kondoo kadhaa ili kumpata ng'ombe mmoja. Idadi ya mbuzi au kondoo iliyokuwa sawa na ng'ombe mmoja, ilitegemea makubaliano baina ya watu waliobadilishana vitu hivyo.

Ilikuwa vigumu kufanya biashara kwa njia hiyo. Mtu mwenye hamu ya kupata kitu fulani hakuwa na hakika ya kukipata upesi. Kama angekuwa na kitu cha kubadilishana, mara nyingi alikuwa hana budi kuhangaika sana akimtafuta mtu mwenye kitu alichokihitaji na wakati mwingine alimkosa.

Polepole watu walitambua tatizo hilo. Walitafuta njia nyingine rahisi ya kupata mahitaji yao. Njia hiyo rahisi ilikuwa fedha. Inasemekana kwamba Wachina ndio wa kwanza waliotumia fedha. Fedha yao haikuwa sawa na fedha tunayotumia leo. Wao walitengeneza vipande vya fedha, shaba na dhahabu. Ilikubaliwa kuwa kila kipande kilikuwa na thamani yake. Walinunua vitu kwa kutoa vipande vya fedha, dhahabu au shaba vyenye thamani fulani.

Utumiaji wa fedha umerahisisha sana kazi nyingi. Watu wanapata mahitaji yao katika maduka, sokoni na mahali pengine kwa urahisi. Lakini pamoja na kurahisisha kazi fedha imewavimbisha vichwa baadhi ya watu. Watu wengine wanadhani kuwa mtu akiwa na fedha, basi ameendelea. Wengine wanajitapa na kujiona bora kuliko wenzao. Fedha si msingi wa maendeleo ya binadamu bali fedha ni matokeo ya juhudi ya mtu. Juhudi katika kufanya kazi ikichanganywa na maarifa, mazao ya kazi hiyo huonekana. Mazao yakionekana kwa wingi ndipo inapowezekana kusema kuwa mtu ameendelea.

Maelezo

1. Выражение kama vile имеет значение "... как например", "такой/такие как ...": Napenda sana matunda ya Kiafrika kama vile maembe au mapapai "Я очень люблю африканские фрукты, такие как манго или папайи"; Katika mbuga ya wanyama tuliwahi kuona wanyama wa nadra kama vile faru na chui "В заповеднике нам удалось увидеть редких животных, как, например, носорога и леопарда".

Mazoezi

5. Найдите в тексте суахилийские эквиваленты следующих выражений:
основа развития; в различных целях; иметь короткую историю; до изобретения денег; обмениваться вещами; порой требовалось иметь (*что-л.*); количество, эквивалентное (*чему-л.*); зависеть от договоренности между людьми; было сложно; вести торговлю; желавший достать какую-либо вещь; не быть уверенным; иметь что-либо на обмен; приходилось суетиться; осознать проблему; удовлетворять свои потребности; иметь свою стоимость; использование денег; облегчать труд; с легкостью; некоторые люди; (*человек*) преуспел; заноситься и считать себя лучше других; результат усилий; усердие, умноженное на знания.

6. Дайте русские эквиваленты:
maendeleo makubwa; -pata maendeleo; maendeleo ya biashara; biashara ndogo; biashara yenye kusitawi; biashara ya kimataifa; madhumuni yangu; kwa madhumuni ya kupata mahitaji; mahitaji madogo; mahitaji ya kila siku; -badilisha simu ya mkononi; -badilishana vitu vya shaba; -badilishana siri; makubaliano muhimu; makubaliano baina ya pande mbili; -fikia makubaliano; makubaliano ya kihistoria; historia ya maendeleo ya nchi; -ingia katika historia; hamu ya kusoma; hamu ya chakula; bila ya hamu yo yote; -hangaikia tatizo gumu; -hangaika kwa kuandaa harusi; usihangaike ovyo; vitu vya dhahabu; saa ya dhahabu; thamani ya fedha; thamani ya maisha; -wa na thamani; thamani isiyopimika; mawe ya thamani; utumiaji wa mbolea; utumiaji wa nguvu; utumiaji wa akili; mtu mwenye juhudi; matokeo ya juhudi; tokeo la kazi; -leta matokeo ya hatari; kwa matokeo ya uchokozi; -rahisisha maisha; -rahisisha masharti ya biashara; -zoea kujitapa; mtu mwenye kujitapa daima; -changanya yai na maziwa; yote yamechanganyika akilini mwake.

7. Запомните следующие выражения и составьте с ними предложения:

-fanya juhudi	стараться, прилагать усилия
-fanya biashara	торговать, вести торговлю
-pata mahitaji	удовлетворять потребности
-shikwa na hamu	сильно желать (*чего-л.*)

8. Переведите предложения и замените подчеркнутые выражения синонимами:

1. Makubaliano hufikiliwa upesi kati ya watu wenye kufanya biashara na kupeana vitu mbalimbali. 2. Punde si punde tumechoka tukatamani kurudi nyuma. 3. Acha kuishughulikia kazi hii, sasa haina maana yo yote. 4. Kwenye mkutano wa wanakijiji imeelezwa kwamba shida ya maji iliyozuka ingeweza kuamuliwa kwa juhudi za pamoja. 5. Ukitaka kitoweo chako kiwe kitamu, kwanza weka pamoja nyama ya kondoo na vitunguu vingi. 6. Mhandisi ametushauri kununua mabati ya aina bora kwa ajili ya kutengeneza paa jipya lililoharibika kwa sababu ya mvua kali.

9. Ответьте на следующие вопросы:

1. Fedha hutumiwa kwa madhumuni gani? 2. Watu waliwezaje kupata mahitaji yao hapo zamani? 3. Toa mifano yako ya vitu ambavyo watu wangeweza kubadilishana. 4. Kwa nini ilikuwa vigumu kufanya biashara kwa njia ya kubadilishana vitu? 5. Njia rahisi zaidi ya kujipatia mahitaji ilikuwa ipi? 6. Vitu gani vilitumiwa badala ya fedha za aina hiyo tunayotumia leo? 7. Je, thamani ya shaba ni sawa na thamani ya dhahabu au fedha? 8. Je, inatosha kwa mtu kuwa na pesa nyingi ili apate maendeleo? 9. Msingi wa maendeleo ni kitu gani?

10. Переведите:

1. Жители соседних деревень успешно обменивались между собой продуктами труда и без проблем удовлетворяли свои потребности в еде. 2. Говорят, что в результате тяжелой болезни глава компании потерял аппетит и сильно похудел. 3. Считается, что чрезмерное хвастовство – признак глупости. 4. Было трудно достичь договоренности по вопросам развития

города. 5. Известно, что применение силы в разные периоды истории приводило *(приносило)* к огорчительным результатам. 6. Торговля драгоценными камнями получила большое развитие благодаря высоким ценам на мировом рынке. 7. У меня нет желания помогать брату, который сам не прилагает никаких усилий для решения своих проблем.

11. Переведите диалог, предварительно ознакомившись с новой лексикой:

noti (-; ma-) бумажные деньги
mpango (mi-) план, программа
mwongo (wa-) лгун, обманщик
uongo, uwongo (ед.) ложь, неправда
pembe (-) угол; уголок
Ehee! Ну да!, Конечно!
Kaaa!, Ka! Бог мой! (*удивление или испуг*)
goli (ma-) 1)гол 2)ворота
-tupu пустой, порожний
mkia (mi-) хвост
-danganya обманывать
-panga 1)расставлять, размещать 2)планировать
-amini верить, доверять
-wamba обтягивать, натягивать (*что-л. на что-л.*)

Juma na Saidi

Juma na Saidi ni marafiki. Walimaliza shule ya msingi mwaka jana na sasa kazi yao kubwa ni kuchunga mbuzi na kondoo. Jumamosi iliyopita waliwapeleka wanyama wao malishoni mbali kidogo na kijiji chao. Jua lilipokuwa kali Juma na Saidi waliwakusanya mbuzi na kondoo wao chini ya mti mkubwa na wenyewe walipanda juu ya mti na kuanza kusimuliana habari mbalimbali. Mazungumzo yao yalikuwa hivi:

Juma: Ngoja nikuambie Saidi. Baba yangu ni tajiri sana. Ana noti za fedha ambazo zikiwashwa moto, zinaweza kuchemsha pipa la maji.

Saidi: Wacha bwana! Hata baba yako ni tajiri kiasi hicho, hawezi kumshinda mjomba wangu.

Juma: Unasemaje? Hawezi kumshinda mjomba wako?

Saidi: Hawezi. Mjomba wangu ana fedha za kutosha kuzipanga juu ya reli kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma.

Juma: *(Anacheka.)* Uongo huo Saidi. Hakuna mtu mwenye fedha kiasi hicho!

Saidi: Ni kweli Juma. Kwa nini nikudanganye? Au ulifikiri kuwa baba yako ndiye tajiri kuliko watu wote?

Juma: Basi haya. Ngoja nikueleze kitu kingine. *(Anawaza).*

Saidi: Unafikiria uwongo mwingine kunieleza?

Juma: Siyo uongo. Ehee! Nimekumbuka sasa. Baba yangu ana ngoma kubwa yenye miguu. Ikiwekwa chini magari makubwa yanaweza kupita chini ya miguu hiyo bila ya kuigusa.

Saidi: Kaaa!

juma: Juu ya hiyo ngoma, watu wanaweza kucheza mpira wa miguu na wengine wakikaa pembeni na kushangilia.

Saidi: Sioni ajabu, Juma.

Juma: Huoni ajabu? Umepata kusikia au kuona kitu kikubwa namna hiyo?

Saidi: *(Anacheka.).*

Juma: Mbona unacheka hivyo? Au huniamini?

Saidi: Nani, mimi? Wala sishangai Juma. Nimewahi kusikia na kuona vitu vingi vya ajabu katika maisha yangu. Unamfahamu babu yangu wa Iringa?

Juma: Namkumbuka sana.

Saidi: Basi yule babu yangu ana mbuzi mkubwa kweli kweli. Huyo mbuzi akitembea hagusi watu wala mapaa ya nyumba. Anakuwa juu ya vitu vyote.

Juma: Mwongo Saidi! Hakuna mbuzi mkubwa hivyo.

Saidi: Tulia rafiki yangu. Mimi nakueleza mambo niliyoyaona kwa macho yangu. Yule mbuzi akisimama kwenye kiwanja cha mpira, kichwa chake kinakuwa juu ya goli moja na mkia wake unagusa goli la pili.

Juma: *(Anacheka sana, karibu aanguke mtini).* Ha! Ha! Ha! Huo ni uongo kabisa Saidi.

Saidi: Ni kweli tupu!

Juma: Hakuna mnyama mkubwa kiasi hicho, bwana. Siwezi kuyakubali maneno yako.

Saidi: Sikiliza Juma. Wewe hutaki kuamini kuwa babu yangu ana mbuzi mkubwa kiasi hicho. Lakini unataka mimi nikubali kuwa baba yako ana ngoma kubwa kiasi kile. Kweli inawezekana?

Juma: Ni kweli, baba yangu ana ngoma kubwa kiasi kile.

Saidi: Basi sawa, mimi nakubali. Lakini kama hakuna mnyama mkubwa kama yule mbuzi wa babu yangu, ngozi ya kuwambia hiyo ngoma ilitoka wapi?

Juma hakujibu neno. Wote walitazamana, wakacheka tu.

Saidi: Bwana, jua linatua sasa, tutachelewa. Tena ninaona njaa sana.

Juma: Loo! Hata mimi. Nikifika nyumbani nitamwambia dada anipikie ugali mkubwa kama mlima Kilimanjaro. Nitaumaliza wote!

Wote waliteremka kwenye mti na kuwarudisha wanyama nyumbani.

Maelezo

1. Unafikiria uwongo mwingine kunieleza? "Обдумываешь очередную ложь?" Направительная форма глагола -fikiri "думать" может заменять предлог juu ya "о", "относительно", передавая такие значения, как "обдумывать что-либо", "размышлять о чем-либо" и т.п.: Umeshafikiria mpango wa kazi? "Ты уже обдумал план работы?"; Mabingwa walifikiria tatizo la njaa katika nchi hiyo "Специалисты размышляли о проблеме голода в этой стране". (Сравните: walifikiri juu ya tatizo).

2. Wala sishangai "А я нисколько и не удивляюсь". Слово wala "ни" в разговорной речи может употребляться для усиления отрицания: Wala hatujui "Мы даже и не знаем"; Wala sitaki kwenda huko" «Да я совсем не хочу туда ехать".

3. Karibu aanguke mtini «Он чуть не упал с дерева». Конструкция, в которой глаголу в желательно-побудительном наклонении предшествует слово karibu "близко", переводится с помощью таких выражений как "едва не", "чуть не", "почти" и т.п.: Karibu wazame ziwani humo "Они едва не утонули в том озере"; Mimi nilikuwa karibu niamini maneno yake "Я почти поверил его словам".

Mazoezi

12. Запомните следующие словосочетания:

uongo mtupu	явная ложь
maneno matupu	вздор, чепуха
mikono mitupu	с пустыми руками
miguu mitupu	босиком
[watu, wanyama...] watupu	только одни [люди, звери...]

13. Дайте русские эквиваленты:

-wa mwongo; -sema uongo mtupu; -amini habari za uongo; -amini Mungu; pembe nne; -kaa pembeni; pembe za dunia; pembeni mwa chumba; mkia wa panya; mkia wa nywele; -tikisa mkia; mpango wa maendeleo; mpango wa masomo; -tunga mpango; -panga viti; -panga shughuli; -zoea kudanganya; -danganya bila ya kuona haya; nyumba tupu; waliokuja masomoni ni wasichana watupu; -sema maneno matupu; -tembea miguu mitupu; -ja mikono mitupu; -wamba ngoma kwa ngozi; -wamba viti kwa kitambaa kipya; meza hii ni tupu?

14. Переведите:

1. Не доверяй ему, он привык нести чепуху и всех обманывать. 2. На кухне я обнаружил лишь пустые кастрюли. 3. Собака, виляя хвостом, радуется, а кошка сердится. 4. Его дядя большой мастер по обтяжке барабанов. 5. Язык суахили изучают в различных уголках земного шара. 6. Бумажные деньги начали использовать не так давно. 7. Дети любят бегать босиком. 8. Исключительно (*одни только*) женщины согласились участвовать во встрече, запланированной на воскресенье. 9. Почему ты пришел с пустыми руками? Ты же знаешь, что у твоей бабушки сегодня день рождения. 10. В этом ресторане нет свободных столиков.

15. Замените подчеркнутые словосочетания конструкцией желательно-побудительного наклонения со словом karibu:

1. Juma alikuwa tayari kuanguka chini. 2. Aliposikia hadithi hiyo alitaka kucheka sana. 3. Kijana huyo alikuwa tayari kumwamini mwenzake. 4. Noti za fedha zilikuwa tayari kuwashwa moto. 5. Magari yao yalikuwa tayari kugongana. 6. Mbuzi wote walitaka kukimbia. 7. Mpapai wangu ulitaka kuvunjika kwa matokeo ya upepo mkali.

16. Выберите из списка слов, приведенных ниже, подходящее по смыслу дополнение к глаголу -ona:

uchungu, kizunguzungu, baridi, wivu, njaa, haya, uchovu, kiu, ajabu, huruma.

1. Saidi hakuona ... kusikiliza hadithi za uongo kwa sababu alijua kuwa mwenzake anapenda kudanganya. 2. Wachezaji waliona ... kwa sababu ya kushindwa na timu ya Uingereza katika mchezo wa mpira. 3. Baada ya kurudi kutoka safari ndefu watalii waliona ... 4. Tulipofikia kilele cha Kibo tulianza kuona ... 5. Nilimwonea ... mwenzangu ambaye hakufaulu kufanya mtihani wa historia. 6. Baada ya kusikia kwamba mgonjwa anaona ... daktari alifahamu kuwa mgonjwa huyo ameanza kupona 7. Rajabu alimwonea ... jirani yake aliyejinunulia gari la mtindo wa kisasa. 8. Mwanamke alianguka njiani kwa kuona ... ghafula. 9. Mwizi hakuona ... hata kidogo alipokamatwa wakati wa kuiba vitu vya thamani dukani. 10. Kila asubuhi tembo walizoea kufika ziwani huko kwa sababu ya kuona ...

17. Подтвердите или опровергните следующие утверждения в соответствии с содержанием диалога из упражнения 11. Используйте выражения: Ni kweli tupu; Ni sawa kabisa; Ndivyo hivyo; Ni uongo mtupu; Si sawa hata kidogo; Haiwezekani kuwa hivyo:

1. Juma na Saidi walianza kuchunga mbuzi na kondoo wakati walipokuwa bado watoto wadogo. 2. Siku moja waliwakusanya wanyama wao chini ya mti mkubwa kwa sababu mvua kali ilianza. 3. Juma na Saidi walisimuliana hadithi wakiwa wamekaa juu ya mti. 4. Vijana hao hupenda sana kuelezana hadithi za kweli. 5. Saidi aliwahi kumwona mbuzi mkubwa kama nyumba au hata kushinda nyumba. 6. Saidi aliamini kuwa baba wa mwezake ana ngoma kubwa yenye miguu. 7. Juma na Saidi walishindana kwa uwezo wao wa kudanganyana na kujitapa. 8. Mtu anaweza kuwa na fedha kiasi cha kutosha kuzipanga juu ya reli iendayo kutoka kusini mpaka

kaskazini. 9. Mwishowe wakafahamu kwamba hadithi zao za ajabu zilikuwa uongo mtupu.

18. Предположите, чем еще могли бы похвастаться Джума и Саиди, придумывая малоправдоподобные истории. Расскажите об этом на суахили.

19. Перескажите в косвенной речи содержание диалога из упражнения 11.

20. Переведите:
1. Ребенок упал и чуть было не расплакался, но быстро успокоился, увидев маму. 2. Водитель ехал с большой скоростью, и его грузовик едва не наехал на людей, стоявших на автобусной остановке. 3. Дождей не было несколько месяцев, и наш колодец чуть не пересох. 4. Я почти поверил тому нищему, но тут же понял, что он просто лгун, пытавшийся обмануть меня. 5. Корабль едва не пошел ко дну *(утонул)* во время сильной грозы. 6. Обдумывая план поездки, мы чуть не забыли купить билеты.

* * *

Mazoezi ya kujiandaa kusikiliza hadithi

Maneno mapya

kando, kandokando (-) 1) край, сторона 2) берег
kando ya сбоку, скраю, у
tawi (ma-) ветвь, ветка
bawa (ma-) крыло (*птицы, насекомого*)
-dondosha ронять; сбрасывать

Mazoezi

21. Дайте русские эквиваленты:
kando ya mto; kando ya barabara; -tua paani; -ruka bila ya kutua; -tua kwenye tawi; matawi ya mwembe; tawi lenye maua; -pata hamu ya kusafiri; -kosa hamu ya kula; -beba mzigo; -beba kuni; -zaa matunda; -zaa mtoto; mabawa ya mbayuwayu; mabawa ya mdudu; -dondosha mpira; -dondosha mbegu; kwa njia ya ajabu; kwa njia maalum.

22. Дайте эквиваленты на суахили:
стоять на краю дороги; гулять у реки; срезать ветку дерева; сломанные ветви; большие крылья; крылья коршуна; сильно сожалеть; плодоносящие деревья; уронить пакет молока; сбросить камень в реку.

23. Замените синонимами подчеркнутые слова:
1. Wenyeji <u>walisimuliana</u> habari za mambo ya kale. 2. Wanyama huja kupumzika kivulini mwa matawi ya mti. 3. Gari limesimama <u>kando ya</u> njia. 4. <u>Tulipata hamu</u> ya kuogelea mtoni. 5. Nilimkuta mwanamke <u>akimbeba</u> mtoto wake mgongoni. 6. Mbegu za mimea ile zimeota kila <u>mahali</u> kwenye bustani.

24. Переведите:
1. Inasemekana kwamba miaka mingi iliyopita kulikuwa na mlima mkubwa tena mrefu sana. 2. Watalii wa kila pembe ya nchi walipata hamu ya kuukwea mlima ulio simuliwa. 3. Tulipenda sana kusikiliza ndege wakiimba kwenye matawi ya mwembe. 4. Mgomba ukawa unatoa maua na kuzaa matunda kila miezi sita. 5. Wanafunzi walielekea maktaba wakibeba kamusi na vitabu mikononi. 6. Walielezana habari za mahali walipotembelea mnamo siku za likizo. 7. Kwa bahati mbaya hawakuwa na wakati wala pesa za kutosha. 8. Kila walipofika waliona majumba ya ajabu.

25. Закончите предложения:
1. Nyumba ile haina madirisha wala ... 2. Hatuna hamu ya kucheza mpira wala ... 3. Simwamini kaka yangu wala ... 4. Hawataki kujifunza maneno wala ... 5. Huwezi kuimba wala ... 6. Hana akili wala ...

26. Переведите:
1. Когда-то очень давно существовал красивый город. 2. Услышав об этом городе, многие загорелись желанием увидеть все, о чем рассказывалось. 3. Но они не могли поехать туда, так

как не знали дороги и не имели ни денег, ни запасов еды. 4. Один юноша попросил отца отвезти его в удивительный город. 5. Отец отказался, сказав, что путь туда очень труден и долог. 6. Однако юноша не отчаялся, собрался с силами и отправился один искать тот город. 7. Он взял в дорогу немного хлеба, но сам питался только плодами лесных деревьев. 8. Повсюду, где он проходил, он бросал куски хлеба, чтобы птицы клевали его. 9. Птицы решили отблагодарить юношу, они полетели впереди, показывая ему дорогу. 10. Вскоре он добрался до города своей мечты таким удивительным образом.

Kusikiliza hadithi

- Прослушайте текст полностью.
- Повторите в паузах фразы вслед за диктором.
- Закончите предложения вместо диктора.
- Задайте друг другу вопросы на суахили по содержанию прослушанного текста и дайте на них ответы.
- Ответьте на суахили на вопросы диктора.
- Изложите письменно на суахили содержание текста.

* * *

Mazoezi

27. Переведите следующий диалог и выучите его наизусть:

Chenga na Selina

Siku moja msichana aitwaye Selina alitumwa na mama yake sokoni. Alikuwa peke yake njiani. Alikutana na Chenga, mvulana mwenzake aliyempenda sana Selina.

Chenga: Hujambo Selina?
Selina: Sijambo, wewe hujambo?
Chenga: Mimi sijambo kabisa, wewe je?
Selina: Usiwe na wasiwasi, mimi mzima tu.
Chenga: Ni furaha kubwa leo kukutana nawe peke yako sasa hivi. Unakwenda wapi?
Selina: Ninakwenda sokoni, mama amenituma peke yangu leo.
Chenga: Je, inawezekana niende pamoja nawe? Sina kazi sasa.

Selina: Ukitaka twende. Ninaogopa kwenda peke yangu.
Chenga: Ni bahati kwangu kupata nafasi hii.
Selina: Bahati gani? Tunaonana kila siku.
Chenga: Ndiyo, lakini leo ni tofauti na siku nyingine.
Selina: Tofauti gani? Mimi naona sawa tu kama jana na juzi na siku zote.
Chenga: Iko tofauti, nitakwambia sasa hivi. Twende tu.
Selina: Haya, niambie basi. Kitu gani hicho? Siri au nini?
Chenga: Usiwe na haraka, nitakwambia tu, ngoja kidogo.
Selina: Ningoje nini? Niambie tu, niko hapa, sitakukimbia.
Chenga: Nilitaka kukwambia zamani lakini sikuwa na nafasi.
Selina: Mbona unazidi kuzunguka tu, wala husemi cho chote cha maana.
Chenga: Ni hivi. Ningependa wewe na mimi tukisha kuwa wakubwa, tuoane, unasemaje? Hupendi kuwa mke wangu wa maisha?
Selina: Maneno yako hayana maana. Kama umekosa la kusema, bora usiseme lo lote.
Chenga: Najua, huwezi kukubali mara moja, nenda ukafikiri polepole.
Selina: Sina cha kufikiria, inafaa tuongee mambo mengine. Unaona basi lile?
Chenga: Twende upesi, tutachelewa. Mabasi hapa ni shida sana siku hizi.

28. Найдите в диалоге из упражнения 27 суахилийские эквиваленты следующих выражений. Составьте свой диалог, используя некоторые из них:
как приятно встретить тебя; не волнуйся; можно мне пойти с тобой?; как мне повезло!; в чем же разница?; это что, секрет?; не забегай вперед; ну говори же; у меня не было случая; почему ты ходишь вокруг да около?; так вот; что скажешь?; твои слова лишены смысла; согласиться сразу; мне нечего обдумывать; поговорим о чем-нибудь другом.

29. Переведите:

1. Где здесь можно пообедать? 2. Извините, здесь разрешено курить? 3. Нельзя оставлять машину около входа. 4. Где можно послать электронную почту? 5. В самолете запрещено пользоваться мобильным телефоном. 6. Как можно вызвать такси? 7. Не стоит его ждать, он вернется поздно. 8. На сегодня хватит работать, можете отдыхать. 9. Было решено встретиться еще раз.

30. Объясните на суахили смысл пословицы:

Njia ya mwongo ni fupi.

SOMO LA NANE

Лексическая тема "Стихийные бедствия"

Грамматика

Аналитические глагольные временные конструкции. Такие конструкции состоят из двух личных глагольных форм: на первом месте стоит вспомогательный глагол -wa "быть", второе место занимает смысловой глагол. При этом вспомогательный глагол обычно оформляется одним из временных показателей (-na-, -li-, -ta-), а смысловой глагол – одним из видо-временных показателей (-na-, -me-) или показателей некоторых наклонений (-ki-, -e) и т.п.

Теоретически количество подобных аналитических конструкций может достигать 200, но практически наиболее употребительными являются следующие сочетания (общее значение аналитической временной конструкции складывается из суммы значений составляющих ее грамматических формантов):

-li-...-ki- – длительный характер действия в прошлом: tu***li***kuwa tu***ki***cheza "мы играли (долго)";

-li-...-na- – точечный характер действия в прошлом: tu***li***kuwa tu***na***zungumza "мы разговаривали (в тот момент)";

-li-...-me-/-mesha- – завершенность действия к моменту речи в прошлом: tu***li***kuwa tu***me***soma, tu***li***kuwa tu***mesha***soma "мы (уже) прочитали";

-ta-....-ki- – длительный характер действия в будущем: tu**ta**kuwa tu***ki***jenga "мы будем строить";

-ta-....-me- – завершенность действия в будущем, уверенность в его завершении: tu***ta***kuwa tu***me***jenga "мы уже (конечно, обязательно) построим".

Вспомогательный глагол может быть также оформлен показателем нарратива (так называемой "повествовательной/ рассказывательной" формы) -ka-, который придает аналитической конструкции значение начала или повторяемости действия смыслового глагола в ряду предшествующих действий ("и было..., и было..., и, наконец, стало..."):

-ka-...-na- wafanya kazi wa***ka***wa wa***na***pata mshahara mwisho wa mwezi "рабочие (теперь) получают зарплату в конце месяца";

-ka-...-me- dada a***ka***wa a***me***safiri sana baada ya kuhitimu katika chuo kikuu "сестра стала (начала) много путешествовать после окончания университета".

Mazoezi

1. Переведите предложения и проанализируйте употребление аналитических глагольных форм:

1. Mkuu wa shule alipoingia darasani wanafunzi walikuwa wakichora ramani ya bara la Afrika. 2. Kabla ya mkutano kuanza viti vyote chumbani vitakuwa vimepangwa. 3. Wakati wazazi walipokuwa wanazungumza, watoto wao walikimbilia msituni. 4. Mume aliporudi kazini chakula cha usiku kilikuwa kimeshaandaliwa mezani. 5. Nadhani kuwa ufikapo mwisho wa msimu huu tutakuwa tumepata zao kubwa la maharage. 6. Mwandishi yule alikuwa ametunga hadithi zake maarufu zaidi hata kabla ya kuiacha nchi hii. 7. Nilishindwa kumpata kaka kazini kwa sababu simu yake ilikuwa inatumika wakati wote. 8. Kila mara alipokutana na msichana yule, moyo wake ulikuwa umejaa furaha. 9. Mvua ilikuwa kali sana na nguo zangu zote zikawa zimelowa. 10. Ndege akawa anadonoa chakula kidogo baada ya kupata nafuu. 11. Mama akawa ametulia alipopigiwa simu na binti yake.

2. Вместо точек вставьте в смысловой глагол один из показателей -na-, -me-, -ki-:

1. Daktari alipokuja bibi alikuwa a...lala kitandani. 2. Ukienda kuchukua pesa baada ya kazi, posta itakuwa i...fungwa. 3. Kabla ya panya hajakimbia mtego ulikuwa u...fyatuka. 4. Nilikataa kula kwa sababu nilikuwa ni...shiba. 5. Mkulima alikuwa a...kata kuni alipositikia ngurumo ya simba. 6. Mbwa walikuwa wa...bweka usiku kucha.

3. Поставьте смысловой глагол в следующих аналитических конструкциях в отрицательную форму:

1. Usiku ukiingia nguo zako zitakuwa zimekauka. 2. Dereva alipozungumza na polisi injini yake ilikuwa ikiwaka. 3. Utakaporudi kutoka safarini kitabu chako kitakuwa kimepigwa chapa. 4. Nilipomwangalia mtu yule alikuwa anacheka. 5. Mama alipoingia chumbani mwetu asubuhi ile tulikuwa tumeshaamka. 6. Alikuwa anafanya kazi mnamo siku za Jumapili.

4. Переведите предложения, употребив конструкцию с аналитическими глагольными формами:

1. Всю ночь ребенок очень сильно кашлял. 2. Когда преподаватель вошел в класс, все уже сидели на своих местах. 3. Когда мы приехали в аэропорт, самолет уже приземлился. 4. Если вы пойдете возвращать книги после занятий, библиотека будет закрыта. 5. Когда отец пришел с работы, старший сын ремонтировал компьютер. 6. Эта фабрика была построена еще до начала войны. 7. Я разговаривал по телефону, когда услышал стук в соседней комнате.

5. Составьте предложения со следующими глаголами, употребив их в аналитических конструкцих:

-ondoka, -cheza, -simama, -choka, -tafsiri, -lima

Maneno mapya

mashua (-) лодка; шлюпка
mtumbwi (mi-) лодка (*долбленка*)
merikebu (-) корабль; теплоход
chombo (vy-) судно; корабль
kasia (ma-) весло
-piga makasia грести
poromoko (ma-) лавина; поток
poromoko la maji водопад
gogo (ma-) ствол срубленного дерева; пень; бревно
-epesi 1)легкий (*по весу*) 2)быстрый, скорый
[kwa] taratibu 1)осторожно, осмотрительно 2)постепенно
mviringo (mi-) 1)круг, окружность 2)шар
kapteni (ma-) капитан
tanga (ma-;-) парус
baharia (ma-) моряк, матрос
anasa (-) роскошь, комфорт
dobi (ma-) прачка
bidhaa (-) товар
karne (-) век, столетие
-sokota 1)крутить, скручивать 2)плести
-chonga строгать, обтесывать
-unda строить, сооружать, конструировать
dizeli (-) 1)дизельный двигатель 2)дизельное топливо

Safari za baharini

Tangu zamani watu walikuwa wanatembea katika mito na maziwa na kando kando ya pwani wakivua samaki na kuchukua vitu vyao, lakini hawakuenda mbali kwa sababu hawakujua kuna nini mbele yao. Mashua na vyombo walivyotumia vilikuwa vidogo vya kutosha mahitaji yao tu. Watu wengine walitengeneza namna ya mashua kwa kusokota matete mfano wa vikapu vikubwa, wakayapeleka majini kwa kutumia mikono yao mfano wa makasia. Wengine walikata miti mikubwa wakafanya mitumbwi, wakachonga mbao na kufanya makasia.

Watu wa makabila mengi walikuwa wakitumia mitumbwi kwa kuvuka mito na kuvua samaki kando kando ya pwani. Wengine waliokaa katika nchi ambako kuna mito yenye maporomoko ya maji, walitengeneza namna ya mashua kwa maganda ya miti kwa kuyashona, maana waliona kuwa mitumbwi ya magogo ya miti ni mizito sana. Walipofika penye maporomoko ya maji walikuwa hawana budi kuutoa mtumbwi katika maji na kuuchukua mpaka kuyapita maporomoko yale, ndipo wangaliweza kuuweka majini tena na kupiga makasia. Lakini mashua zilizotengenezwa kwa kushona maganda ya miti zilikuwa nyepesi sana na watu waliweza kuzichukua bila shida.

Baadaye watu walianza kutembea baharini, wakaona ya kuwa vyombo vya namna hizo vilikuwa haviwafai, wakatengeneza vyombo vikubwa zaidi. Lakini hata hivyo hawakuweza kutembea mbali, maana wakati ule walifikiri kuwa dunia ni mfano wa meza, wakaogopa kufika mwisho wa dunia na kuanguka chini na kupatwa na mambo yasiyoweza kufikirika. Kwa taratibu wakazidi kutembea wasiuone mwisho wa dunia, wakatengeneza vyombo vikubwa zaidi, maana waliona vitu vingine katika nchi nyingine, wakapenda kuvichukua nchini kwao.

Basi mambo yakaendelea na watu wakazidi kusafiri katika bahari ili wafike nchi nyingine, wakapata moyo wasiogope. Watu wakafahamu ya kuwa dunia si kama meza ila ni mviringo mfano wa chungwa kubwa. Mnamo kame ya 18 Kapteni Cook alijulikana kama msafiri mkubwa. Alikufa katika mwaka 1779, lakini kabla hajafa alikuwa ameizunguka dunia mara tatu.

Wakati huo vyombo vyote viliundwa kwa miti, vikawa na matanga vikapelekwa kwa nguvu ya upepo. Safari walizozifanya watu hao zilikuwa na taabu, kwa sababu upepo ulipoacha kuvuma vyombo vilisimama, na mara nyingi watu wakawa na njaa na kiu kwa sababu ya kuishiwa na chakula na maji. Lakini watu hawakuchoka, wakaendelea kutengeneza vyombo vya aina nyingine. Mwishowe merikebu zilianza kuundwa kwa chuma.

Naam, watu wameendelea sana. Merikebu za siku hizi zimekuwa nyepesi na kubwa sana. Zinachukua abiria wengi sana pamoja na mabaharia na watumishi wafanyao kazi melini. Tena abiria wanakaa kwa anasa ndani ya meli, wamepata vyumba vizuri vya kulala, vyumba vikubwa vya kulia chakula, na vyumba vya mazungumzo na vya michezo. Pia wanahudumiwa na wapishi wengi na lazima wawe na madobi.

Lakini meli huchukua si abiria tu. Ziko meli nyingi zaidi za kuchukua bidhaa mbalimbali. Merikebu hizi hufanya safari katika kila mahali duniani zikichukua kila namna ya bidhaa. Meli nyingi za kisasa ni zile zenye dizeli. Nani ajuaye kama binadamu atakuwa ameendelea kiasi gani hapo mwisho wa kame yetu? Labda kwa wakati huo meli zake zitakuwa za aina isiyofikirika kabisa.

Maelezo

1. ...mfano wa vikapu, ...mfano wa makasia, ...mfano wa meza – подобные выражения со словом mfano “пример” могут переводиться сравнительными оборотами, такими как “что-то вроде корзин”, “в качестве, взамен весел”, “похожий на стол” и т.п. Вспомните синонимичные конструкции: sawa na vikapu, kama makasia, -enye kufanana na meza.

2. Словосочетание hata hivyo (*букв.* “даже так”) имеет русские эквиваленты “тем не менее”, “все-таки”.

3. ...na kupatwa na mambo yasiyoweza kufikirika “...и угодить в непредсказуемую ситуацию”. Пассивная форма глагола -pata имеет свою особенность: она употребляется там, где речь идет о каком-либо несчастье, аварии и т.п.: Walipatwa na ajali ya ndege “Они попали в авиакатастрофу”; Alipatwa na

ugonjwa mbaya “Он сильно заболел”; Tulipatwa na balaa “Нас постигла беда”.

4. ...wakazidi kutembea wasiuone mwisho wa dunia “они продолжали продвигаться дальше и не обнаружили конца света”; ...wakapata moyo wasiogope “они обрели новые силы и перестали бояться”. Обратите внимание на то, что отрицательная форма глагола на -e в подобных случаях переводится соответствующим временем изъявительного наклонения.

5. Словосочетание -pata moyo (*букв*. “получать сердце”) имеет значения “получать стимул”, “обретать новые силы”.

Mazoezi

6. Найдите в тексте суахилийские эквиваленты следующих выражений:
передвигаться вдоль побережья; не знать, что у вас впереди; удовлетворять лишь собственные потребности; обрабатывать древесину; пересекать реки; реки с водопадами; изготовлять лодки; сшивать кору деревьев; лодки из бревен; вытаскивать лодку на сушу; такие суда не годились; край земли; свалиться вниз; что-то невообразимое; великий путешественник; прежде, чем он умер; трижды объехать земной шар; двигаться силой ветра; у них вышли запасы еды и питья; жить со всеми удобствами; комфортабельные каюты; холлы и спортивные залы; их обслуживает множество поваров; их надо обстирывать; грузовые суда; кто знает?; к концу нашего столетия.

7. Дайте русские эквиваленты:
vyombo vya baharini; -safiri kando kando ya pwani; mashua yenye matanga; kituo cha mashua; mashua ya anasa; hoteli ya anasa; chumba cha anasa; -ishi kwa anasa; poromoko la mawe; poromoko la theluji; -unda chombo; -unda darubini; kiwanda cha kuunda ndege; -chonga mbao; -chonga mti; -chonga jiwe; mabaharia wa merikebu; kapteni wa merikebu na timu yake; -enda taratibu; -fikiria tatizo kwa taratibu; -acha magogo matupu; gogo la mti; treni nyepesi; mtu mwepesi; mzigo mwepesi; -peleka nguo kwa dobi; nyumba ya dobi; meli ya bidhaa; -badilishana bidhaa; bidhaa za namna mbalimbali; injini ya dizeli; mafuta ya dizeli; lori lenye kutumia dizeli.

8. Дайте антонимы следующих слов и выражений:
-teremka chini; -vuta mashua; kapteni mnene; -washa injini; -sikitika; mtumbwi mzito; -poteza vyeti; mjomba maskini; maji matamu; mazoezi magumu; kame ijayo.

9. Замените подчеркнутые слова синонимичным выражением со словом mfano:
1. Mabaharia wa kwanza walitumia vipande vya mbao badala ya makasia. 2. Watu wa zamani walidhani kuwa dunia yetu ilikuwa imefanana na meza. 3. Honi ya gari lake inalia sawa na chura. 4. Shangazi yetu anajua kupika vitoweo vitamu kama mpishi hodari. 5. Ghafula tumesikia sauti yenye kufanana na sauti ya fisi. 6. Punde si punde mvua ilianza kunyesha kwa nguvu ikionekana kama poromoko la maji.

10. Переведите:
1. Walijitahidi kulima shamba lao kabla ya kuanza masika, wakafanya kazi tangu asubuhi mpaka usiku wasiwahi. 2. Nilipokuwa safarini mume wangu alijifunza kujipikia mwenyewe asifaulu. 3. Polisi akipita darajani alimwona mtu aliyekuwa karibu azame, akavua haraka nguo zake akapiga mbizi asimwokoe yule mtu. 4. Timu yetu ilipambana moto moto na timu ya majirani ikafunga goli moja isishinde. 5. Mwanafunzi alijaribu kufanya vizuri mtihani mgumu, akatumia uwezo wake wote asiweze kujibu maswali ya mwalimu.

11. Закончите предложения в соответствии с текстом:
1. Watu walioishi zamani hawakujua kwamba dunia yetu ni mfano wa mviringo, kwa hivyo ... 2. Vyombo vya kwanza vilivyokuwa vikiundwa na binadamu vilitengenezwa kwa ... 3. Mashua zilizokuwa na matanga zilipata shida kusafiri mbali kwa sababu ...

4. Watu wakifika kwenye poromoko la maji, walikuwa hawana budi ... 5. Mashua zilizoshonwa kwa maganda ya miti ziliweza kuchukuliwa bila shida kwa sababu ... 6. Wasafiri waliona vitu vingine katika nchi za mbali, wakapenda kuvichukua nchini kwao, kwa hivyo ... 7. Abiria wa merikebu wanaosafiri siku hizi hustarehe sana shukrani kwa ... 8. Licha ya merikebu za abiria kuna meli nyingine ambazo ...

12. Передайте коротко на сухили содержание текста.

13. Переведите:

1. Гуляя вдоль берега, мы наблюдали за рыбаками, которые вытаскивали из моря свои сети, полные рыбы. 2. Парусные лодки были видны далеко в море и походили на белых птиц с большими крыльями. 3. Местные мастера сооружали небольшие судна из стволов срубленных деревьев, но такие лодки были очень тяжелые. 4. Приближаясь к водопаду, мы стали грести очень осторожно. 5. Капитан корабля не разрешил морякам спускаться на берег, тем не менее, некоторые их них ему не подчинились. 6. В наш век многие автомобили используют дизельное топливо, например, грузовики, перевозящие различные товары и грузы. 7. У меня есть мечта совершить кругосветное путешествие на большом теплоходе с комфортабельными каютами, кинозалами и ресторанами.

14. Переведите следующий текст, предварительно изучив новую лексику:

Maneno mapya

gharika (-) потоп, наводнение
mzee (wa-) старый человек, старик
-zee старый; пожилой
mwananchi (wananchi) житель, гражданин [страны]
kipepeo (vi-) бабочка; мотылек
umeme (ед.) 1)молния 2)электричество
kijia (vi-) дорожка, тропинка
-thibitisha подтверждать, уточнять
-tabiri предсказывать, прогнозировать
-enea распространяться
-ng'oa вырывать, выдергивать; корчевать

hekima (-) мудрость; знание
-bovu плохой, негодный; неисправный
hafifu слабый, хилый; скудный
-vuja протекать; пропускать воду
-furika переливаться через край, выходить из берегов (*о реке*)

Gharika

Mvua ya masika ilikuwa imechelewa sana. Mashamba yote makubwa na madogo yalikuwa yametayarishwa na wakulima. Wazee ambao wanajua kutabiri hali ya hewa waliwaambia wananchi kuwa walikuwa wamekwishaona dalili za mvua.

Wazee hao walieleza dalili walizoziona hivi, "Ukiona ardhi imekauka na mimea imeanza kukauka pia, ujue kuwa mvua iko karibu sana. Ukiona jua ni kali sana, ufahamu mvua yakaribia kunyesha. Ukiona vipepeo weupe au ndege wa angani wakiruka kuelekea upande mmoja, ufahamu kuwa wamekwishasikia harufu ya mvua."

Watu waliamini wazee wao, maana wameona mengi katika maisha yao na wana hekima ya kuweza kutambua dalili za mvua. Punde si punde wote wakaona wingu dogo la kwanza mbinguni. Mzee mmoja akathibitisha, "Ni kweli, wingu lile ni la mvua kwa sababu ni jeusi. Yaonekana kuwa mvua yaweza kunyesha wakati wo wote usiku wa leo au kesho." Wakati mzee alipokuwa akisema watu waliona umeme kwa mbali, kisha wakaona kuwa mawingu ya mvua yalikuwa yakiongezeka. Upepo ukavuma na ngurumo ya radi ikasikika. Saa za jioni mvua ilinyesha, ikaenea kila mahali. Mapaa ya nyumba yaliyokuwa mabovu yakaanza kuvuja.

Mvua ilinyesha usiku wote na asubuhi ilikuwa bado inanyesha. Mvua iliendelea kunyesha kwa wiki nzima. Miti hafifu iling'olewa na maji ya mvua. Mashamba mengi yakafunikwa kwa maji ya mvua. Kwa vile mvua iliendelea watoto waliambiwa wasiende shule wakae nyumbani mpaka mvua itakapopungua.

Mambo yalizidi kutisha kwani mvua ambayo wananchi walikuwa wanaingojea kwa muda mrefu, sasa iligeuka kuwa gharika. Mahali pa mvua kusaidia, ilikuwa inaharibu. Mito ilifurika sana na madaraja yakachukuliwa na maji. Barabara na vijia vikageuka mito. Mvua ikaanza kuharibu mashamba na nyumba za

watu mahali pa kuwasaidia. Lakini baada ya majuma mawili mvua ilianza kupungua. Hali ya kawaida ikarudi nchini.

Maelezo

1. Yaonekana/inaonekana может переводиться вводными словами, такими как "очевидно", "видимо", "по всей вероятности" и т.п.

2. Kwa vile "так как", "поскольку", "потому что": Kwa vile tiketi zote za ndege zilikuwa zimeuzwa ilitubidi kwenda kwa treni "Поскольку все билеты на самолет были проданы, мы вынуждены были ехать поездом". Сравните синонимы kwa sababu, kwa kuwa.

3. Выражение mahali pa употребляется в значении "вместо того чтобы", "вместо (*кого-л./чего-л.*): Mahali pa kujiandaa kwa mitihani alikwenda mpirani "Вместо того чтобы готовиться к экзаменам, он пошел на футбол; Walitumia mishale mahali pa bunduki "Они использовали стрелы вместо ружей". Сравните синоним badala ya.

Mazoezi

15. Дайте русские эквиваленты:

hasara iliyoletwa na gharika; -pambana na gharika; -patwa na gharika; -wa na hekima; uamuzi wa hekima; mzee mwenye hekima; wazazi wazee; wananchi wa Tanzania; hiari ya wananchi; nguvu za umeme; birika la umeme; vyombo vya umeme; ngurumo na umeme; afya hafifu; maendeleo hafifu; mimea hafifu; udongo hafifu; -tabiri hali ya hewa; -tabiri maisha ya baadaye; hali isiyotabirika; -thibitisha habari; -thibitisha faida ya biashara; -thibitisha matokeo ya kazi; kuenea kwa habari; kuenea kwa ugonjwa; mashua inayovuja; paa lenye kuvuja; -ng'oa jino; -ng'oa mizizi; balaa ya kufurika kwa mto; redio mbovu; chakula kibovu; tunda bovu.

16. Составьте предложения со следующими словосочетаниями:

-tabiri maendeleo ya nchi; -tumia akili na hekima; -thibitisha habari za televisheni; kuenea kwa uwongo; kwa vile; yaonekana; mahali pa kusaidia; mfano wa kipepeo.

17. Найдите в тексте из упражнения 14 предложения с аналитическими глагольными формами. Прокомментируйте их употребление.

18. Ответьте на вопросы по содержанию текста из упражнения 14:

1. Wazee hutabiri mvua namna gani? 2. Kwa nini wananchi huwaamini wazee wao? 3. Dalili zipi ziliwaonyesha watu kwamba mvua inakaribia? 4. Mvua iliendelea kwa muda gani? 5. Matokeo ya mvua yalikuwa yapi? 6. Je, mvua huleta faida au hasara?

19. Переведите:

1. Специалисты предсказывают большое наводнение на этой территории. 2. Неизвестная болезнь быстро распространилась по всей области. 3. Обычно мы гуляем по тропинке вдоль реки, но после сильных дождей река вышла из берегов. 4. Мой электрический чайник стал протекать, пора (*пришло время*) покупать новый. 5. Все население понесло убытки в результате той войны. 6. Поскольку двигатель вашего автомобиля неисправен, я заменю его. 7. Вы можете подтвердить слова, сказанные вами на прошлой встрече? 8. По всей вероятности, дождь будет продолжаться не менее суток.

* * *

Mazoezi ya kujiandaa kusikiliza hadithi

Maneno mapya

nungunungu (-) дикобраз
kucha (ma-) коготь
-jivuna 1)хвастать[ся] 2)важничать, кичиться
-tafuna 1)жевать 2)есть
-simamisha ставить прямо; выпрямлять; устанавливать

20. Запомните следующие выражения:

-lala na njaa	остаться голодным
-tokwa na damu	истекать кровью
-zunguka huku na huko	бродить повсюду

21. Дайте русские эквиваленты:

mtu apendaye kujivuna; -tafuta kitu fulani huku na huko; -winda kwa kutumia makucha; -tafuna pole pole; nyama kisichotafunika; -simamisha kiti kilichoanguka; -choma kidole na kutokwa na damu; -dhani moyoni; -sema moyoni; -kimbiza mnyama; -rukia mtu kwa ghafula; -lia kwa uchungu; ngoja nimwulize.

22. Дайте эквиваленты на суахили:

иметь острые когти; поймать любого зверя; бродить тут и там; подскочить к кому-либо; сказать себе; сжевать весь хлеб; установить новогоднюю елку; подойти поближе; гоняться за кошками; кричать от боли; дай-ка я его съем.

23. Закончите предложения:

1. Mnyama mkali ni mnyama ambaye ... 2. Kujivuna maana yake ni ... 3. Kusema moyoni ni sawa na ... 4. Kusimamisha kitu fulani, maana yake ni ... 5. Kutafuna chakula kuna maana ....

24. Ответьте на следующие вопросы:

1. Chui ni mnyama wa aina gani? 2. Chakula chake ni nini? 3. Ulipata kumwona nungunungu kwa macho yako mwenyewe? 4. Nungunungu ana sura gani? 5. Nani ni mkali zaidi, chui au nungunungu? 6. Je, nungunungu anaweza kumshinda mnyama ambaye ni mkubwa kuliko yeye?

25. Соедините предложения с помощью союза ingawa. Переведите полученные предложения:

1. Mzee amekula pudini yote. Anaona shida kutafuna kwa vile ana meno machache tu. 2. Tutaondoka kesho asubuhi. Wataalamu wanatabiri kuharibika kwa hali ya hewa. 3. Tembo hawindi wanyama wengine. Yeye mwenyewe ni mnyama mkubwa kuliko wengine. 4. Msichana yule hujivuna ya kuwa yeye ni mrembo sana.

Watu wengine wanashangaa na kusema kwamba sura yake ni ya kawaida tu. 5. Simba yule ameshakuwa mzee, hawezi kukimbiza tena mnyama ye yote. Makucha yake bado ni makali ya kutosha.

26. Составьте предложения по образцу:

mimi, -nunua, kamusi > sikununua kamusi hata moja

1. mzee, -lala, dakika. 2. wanafunzi, -fanya, mtihani. 3. mbona, wewe, -leta, kibiriti? 4. mtoto, yule, -wa na, jino, bado. 5. msituni, huu, hamna, kijia. 6. sisi, -kuta, mtalii.

27. Переведите:

1. Это очень свирепый лев, хотя он уже старый, и его когти не такие острые, как раньше. 2. В этом заповеднике мы не встретили ни одного леопарда. 3. Если ты не пойдешь в магазин, я не смогу ничего приготовить, и ты останешься голодным. 4. Дикобраз умеет защитить себя благодаря острым иголкам (*колючкам*), которые он расправляет (*выпрямляет*) при виде врага. 5. Когда врач вырывал мне зуб, я плакал от боли. 6. Он сказал себе: "Даже это старое ружье пригодится мне". 7. Мы подошли поближе к кустам и обнаружили там человека, истекавшего кровью.

Kusikiliza hadithi

- Прослушайте текст полностью.
- Повторите в паузах фразы вслед за диктором.
- Закончите предложения вместо диктора.
- Задайте друг другу вопросы на суахили по содержанию прослушанного текста и дайте на них ответы.
- Ответьте на суахили на вопросы диктора.
- Изложите письменно на суахили содержание текста.

* * *

Mazoezi

28. Переведите диалог и перескажите его на суахили в косвенной речи:

Njaa

Miaka mingi iliyopita njaa kubwa ilitokea nchini. Watu na wanyama wengi walikufa kwa sababu ya kukosa chakula. Siku moja wazazi waliwasimulia watoto wao habari ya njaa hiyo.

Baba: Wanangu, balaa kubwa ilitokea nchini mwetu mwaka fulani.

Rehema: Balaa gani hiyo baba?

Baba: Kulikuwa na njaa kubwa.

Amani: Njaa gani hiyo baba? Kwani mama alikuwa hapiki chakula?

Baba: Sio hivyo mwanangu.

Rehema: Sasa baba, kwa nini unasema kulikuwa na njaa?

Baba: Siyo njaa ya kukosa chakula siku moja tu.

Amani: Basi, ni njaa gani hiyo?

Baba: Aa! Wanangu. Watu walilima lakini hawakuvuna. Mvua haikunyesha kwa muda mrefu. Jua lilikuwa kali sana. Mimea yote ilikauka.

Rehema: Lo! Ulikuwa mwaka mbaya sana huo.

Baba: Ndio mwanangu. Pia watu walikuwa hawaweki akiba ya chakula. Shida ilikuwa kubwa. Watu, wanyama na ndege wengi walikufa kwa njaa.

Amani: Sasa tutafanyaje ili njaa isitokee tena?

Baba: Hatuna budi kulima mimea inayoweza kusitawi bila ya kujali jua kali.

Mama: Ni kweli. Tena tukivuna chakula lazima tuweke akiba katika ghala.

Baba: Mwaka huu tutalima shamba kubwa zaidi. Tutatia mbolea. Tutapanda mimea inayofaa na bila shaka tutapata mazao mengi.

Rehema: Na tutaweka akiba ya chakula ghalani tusipate njaa tena.

Mama: Sawa mwanangu.

29. Переведите следующий рассказ, используя аналитические глагольные формы в подчеркнутых конструкциях:

Несколько лет назад я жил в маленьком южном городе. Каждый день по пути на работу я <u>покупал</u> себе пару

апельсинов у пожилой женщины, <u>сидевшей</u> на перекрестке с большой корзиной фруктов.

Однажды я пригласил своих коллег в гости. В этот день я решил купить у женщины все фрукты.

Услышав мою просьбу, она рассердилась.

- Вот ваши два апельсина! - сказала женщина.
- Но я хочу купить все ваши фрукты.
- Я не могу продать вам всё.
- Почему? - удивился я.
- А что же я <u>буду делать</u> целый день без фруктов?

30. Переведите следующую шутку. Перескажите ее на суахили от лица жены:

Maneno ya kusaidia tafsiri

mpenzi [wangu]	дорогой/ любимый
hivyo basi; ndiyo maana	значит (*вводное слово*)

После работы муж вернулся домой очень голодным. Он спросил жену:

- Ужин готов?
- Нет, – ответила жена.
- Ничего, дорогая, я пойду в кафе и там поужинаю.
- Подожди немного.
- Значит, ужин сейчас будет готов? – обрадовался муж.
- Нет, я буду готова пойти поужинать вместе с тобой.

31. Ответьте на следующие вопросы:

1. Mtu anaweza kukaa siku ngapi akiwa na njaa? 2. Je, mtu anaweza kufa anapoishiwa na maji ya kunywa? 3. Je, wewe hupenda kujipikia mwenyewe? 4. Unafanya nini usipotaka kulala na njaa? 5. Ungalifanya nini ungalipatwa na jambo mfano wa yule mtu aliyeachwa peke yake kwenye kisiwa kisichokuwa na mtu hata mmoja?

32. Объясните на суахили смысл пословицы:

Si kila mwenye makucha huwa simba

SOMO LA TISA
Лексическая тема “Аренда автомобиля”

Грамматика

Выражение модальных значений. Модальность можно передать тремя способами:

1) Модальные значения можно выразить при помощи вспомогательных глаголов *-pasa, -bidi, -lazimu, -faa*. Если расположить их по степени категоричности, жесткости побуждения к выполнению действия смыслового глагола, то эти модальные глаголы выстроятся следующим образом: -lazimu “быть необходимым, быть должным”, -pasa “следовать, надлежать”, -bidi “надлежать, приходиться”, -faa “следовать, годиться”.

Все названные глаголы употребляются в безличной форме (т.е. оформляются показателем 5-го класса i-), за вспомогательным глаголом следует смысловой глагол в инфинитиве или желательно-побудительном наклонении, например:

Inalazimu ***ku***maliza somo mnamo saa 5 “Надо/необходимо закончить урок в 11 часов”.

Ilipasa miti ipandw***e*** mbele ya nyumba “Следовало/надо было посадить деревья перед домом”.

Itabidi ***ku***rudi nyumbani mapema “Надлежит/надо будет вернуться домой пораньше”.

Inafaa wasichana wava***e*** nguo ndefu “Девушкам следует/годится носить длинные платья”.

Вспомогательный глагол может включать в свой состав объектный показатель лица, совершающего действие, выраженное смысловым глаголом:

Itakulazimu kununua ramani ya mji “Тебе надо будет купить карту города”.

Ilimpasa kupika chakula cha mchana “Ему следовало приготовить обед”.

Imenibidi nikutane nao jana “Мне надо было встретиться с ними вчера”.

Inatufaa kukusanyika hapa “Нам следует собраться здесь”.

Глагол -pasa может употребляться в личной форме, но обязательно в пассивном залоге, сравните:

Iliwapasa kununua/wanunue kitabu = Walipaswa kununua kitabu “Им следовало/надо было купить книгу”.

Отрицание модальных конструкций образуется за счет отрицательных форм вспомогательных глаголов:

Haiwalazimu kurudi kazini “Им не надо возвращаться на работу”.

Haikumbidi asome kitabu hiki “Ей не следовало читать эту книгу”.

Hatutapaswa kujenga nyumba “Нам не придется строить дом”.

2) Модальные значения могут передаваться также при помощи модальных слов *lazima* и *budi*, за которыми следует смысловой глагол в инфинитиве или желательно-побудительном наклонении:

Lazima kunawa mikono kabla ya chakula “Надо мыть руки перед едой”.

Lazima (=ni lazima) wote wakusanyike uwanjani “Надо всем собраться на площади”.

Budi miti ipandwe leo “Деревья необходимо посадить сегодня”.

Отрицание подобных модальных конструкций образуется за счет отрицательной связки si или отрицания смыслового глагола в желательно-побудительном наклонении:

Si lazima wote wakusanyike uwanjani “Необязательно всем собираться на площади”.

Budi miti isipandwe leo “Не стоит/ не надо сажать деревья сегодня”.

3) Еще один из способов выражения долженствования, (о котором уже говорилось – см. часть 1, урок 11), – личная отрицательная форма глагола *-wa na* “иметь” и существительного *budi* “выход, избавление”, за которыми следует инфинитив (или реже желательно-побудительное наклонение) смыслового глагола:

Hawana budi kujenga nyumba mpya “Они должны/обязаны построить новый дом”.

Simu haina budi kupelekwa leo “Телеграмму надо послать сегодня”.

Tulikuwa hatuna budi kumsaidia (или менее употребительная конструкция – hatukuwa na budi.... “Мы должны были ему помочь”.

Utakuwa huna budi kunisaidia (hutakuwa na budi...) “Ты должен будешь помочь мне”.

Mazoezi

1. Переделайте предложения, придав им модальные значения с помощью глаголов -lazimu, -bidi, -pasa, -faa.
Образец: *Fundi alitengeneza gari letu haraka >*
Ilimpasa fundi kutengeneza gari letu haraka

1. Wazazi wanatunza vizuri watoto wao. 2. Mganga anatumia ujuzi wake wote kutibu magonjwa ya hatari. 3. Nitanunua kompyuta mpya. 4. Tulipiga makasia kwa nguvu. 5. Utapeleka nguo zako kwa dobi. 6. Mwandishi alikaa katika maktaba kwa siku nyingi.

2. Соедините слова в предложения по образцу:
-bidi, vijana, vizuri, -soma > Inawabidi vijana kusoma vizuri

1. -pasa, wewe, deni, -lipa, ijayo, wiki. 2. -lazimu, ndege, wa, rubani, shambani, -tua. 3. -bidi, mimi, kesho, -amka, asubuhi, mapema, na. 4. -faa, sisi, -tano, sentensi, -tunga. 5. -paswa, dada, kila, ugali, -songa, siku. 6. -bidi, majirani, wao, -acha, ugomvi. 7. -lazimu, mfugaji, kazi, -angalia, zote. 8. -faa, nyinyi, kamusi, -rudisha, darasani.

3. Замените личную форму глагола безличной и наоборот:

A/ 1. Mnapaswa kuweka akiba ya chakula kwa msimu ujao. 2. Tulipaswa kuitayarisha vizuri safari yetu. 3. Ninapaswa kufungua akaunti kwenye benki. 4. Mwana alipaswa kuomba msamaha kwa baba yake. 5. Unapaswa kutenda kwa utaratibu katika hali kama hii.

B/ 1. Iliwapasa wauguzi kuwahudumia wagonjwa bila ya kupumzika hata dakika moja. 2. Inatupasa kulinda vizuri mashamba yetu. 3. Inakupasa ufunge duka lako kabla ya giza halijaingia. 4. Itanipasa nimpigie simu ofisini mwake mume wangu. 5. Itampasa kufanya tena mtihani wa Kifaransa.

4. Сделайте предложения отрицательными:

1. Daktari ilimbidi kumpasua haraka mgonjwa yule. 2. Itakulazimu kuthibitisha maneno yako. 3. Tunapaswa kutekeleza masharti yote. 4. Inawabidi wakulima wapande mahindi mwezi huu. 5. Ilinipasa kubadili simu yangu ya mkononi. 6. Dereva alipaswa aende mbio ili kuiwahi treni ya asubuhi.

5. Измените конструкцию предложений, используя другие формы модальности, и переведите их:

1. Hatuna budi kujenga banda jipya la kuku. 2. Wote watakaoshiriki mkutanoni lazima wakusanyike mnamo saa nne. 3. Watu wa zamani walikuwa hawana budi kubadilishana vitu ili kupata mahitaji yao. 4. Mwongo yule budi athibitishe habari zote alizozitoa. 5. Ukitaka kuwa rafiki yangu huna budi kuyaacha majivuno yako. 6. Nilikuwa sina budi kumsaidia kaka yangu aliyepatwa na balaa kubwa.

6. Переведите:

1. Местные жители должны были строить свои дома около рек и озер. 2. Людям этого племени необходимо постоянно искать новые пастбища для своих животных. 3. Тебе следует пойти к зубному врачу незамедлительно. 4. Мы должны хорошо обдумать план нашей поездки на водопады. 5. Им не обязательно выполнять эту работу сегодня. 6. Туристам надо взять теплую одежду, так как ночью в горах очень холодно. 7. Сначала вам надлежит заполнить эти бланки. 8. Если хочешь, чтобы тебя встретили в аэропорту, тебе надо дать телеграмму. 9. Нам необходимо починить загон для скота до наступления сезона дождей.

Maneno mapya

usalama (ед.) безопасность
uchumi (ед.) экономика; хозяйство
ngamia (-) верблюд
tahadhari (-) предосторожность
-tahadhari быть осторожным, остерегаться

farasi (-) лошадь, конь
imara крепкий, прочный, устойчивый
ujenzi (ед.) стройка, строительство
mjenzi (wa-) строитель
-angalifu внимательный, бдительный
pundamilia/ punda milia зебра
kivuko (vi-) 1)переправа 2)переход 3)паром
wazi 1)открытый 2)ясный, понятный
mtaa (mi-) 1)район (*города*) 2)улица
msururu/ msululu (mi-) цепь, ряд; серия
-dumu 1)продолжаться, длиться 2)быть прочным, постоянным
-babaika теряться, мешкать
tukio (ma-) случай, событие
-egesha ставить на стоянку, парковать
-jitokeza появляться, показываться
-hakikisha 1)убеждать[ся], удостоверять[ся] 2)обеспечивать, гарантировать
-wasiliana общаться, контактировать, связываться

Usalama barabarani

Hapo zamani hapakuwa na barabara wala magari. Watu walitumia njia nyembamba na walisafiri kwa miguu. Walipotaka kusafirisha mazao na vitu vingine walitumia wanyama kama punda, farasi, ngamia na wengine. Na siku hizi vipo vyombo mbalimbali vya usafiri vinavyotumika kama magari, mashua au meli, reli au ndege.

Njia rahisi ya usafiri na inayotumika sana katika kila nchi ni barabara. Barabara ni kitu muhimu kwa uchumi wa nchi. Serikali inapaswa kuwahakikishia watu wote barabara safi, imara na za kudumu. Mahali pengine wananchi inawabidi wenyewe kushirikiana ili kujenga barabara zao. Lakini kutengeneza barabara si kazi rahisi. Kwa hivyo ni wataalamu wanaopaswa kushughulika na ujenzi wa barabara. Barabara ikiwa tayari, magari ya aina zo zote huruhusiwa kuitumia. Kwa kuwa magari ni mengi sana siku hizi, wajenzi wa barabara hutengeneza njia ndogo pembeni inayotumiwa na watu waendao kwa miguu na wenye kupanda baisikeli. Tahadhari hii inachukuliwa ili kupunguza ajali kwa watu. Kila wakati usalama wa watu unatiwa maanani sana.

Kila mtu anayetumia barabara inamlazimu kuwa mwangalifu. Unapotaka kuvuka barabara, vuka mahali penye alama za pundamilia. Hapo ndipo mahali panapotumika kama kivuko cha barabara kwa watu waendao kwa miguu. Kama unavuka mahali ambapo hakuna kivuko maalum au taa za kuongoza magari, inakubidi kwanza kuangalia kulia ili kuona kama hakuna magari, pili angalia kushoto. Kisha angalia tena kulia kwako, halafu vuka barabara. Unapovuka, vuka upesi na usibabaike.

Mahali panapofaa kutumia unapovuka barabara ni pale ambapo unaweza kuona wazi magari yanayokuja kushoto na kulia kwako. Si vizuri kuvuka mahali ambapo gari dogo au kubwa limeegeshwa karibu yako. Wanaoendesha magari hawataweza kukuona utakapojitokeza ghafula nyuma ya gari lililoegeshwa karibu yako. Kila mara hupaswa kuhakikisha kuwa unaona bila shida magari yote yanayokuja kulia na kushoto kwako.

Zipo baadhi ya barabara ambazo zina sehemu maalum katikati. Sehemu hizo hupandwa maua au miti. Barabara za aina hiyo si nyingi na zinapatikana zaidi katika miji mikubwa kuliko katika miji midogo au nje ya miji. Ikiwa unavuka mahali ambapo ipo nafasi tupu katikati ya barabara, basi unapaswa kuvuka na kusimama kwa muda katika sehemu hiyo kabla hujavuka sehemu ya pili. Ukiona kuwa sehemu ya pili kuna usalama pande zote, angalia kulia, kushoto kisha kulia, halafu vuka.

Miji mingi ina barabara nyingi. Barabara hizo zinapita katikati ya mitaa mingi yenye misururu mirefu ya majumba. Kwa vile barabara hizo ni nyingi, mara nyingi zinapewa majina ya watu maarufu au matukio muhimu yaliyowahi kutokea nchini. Wengi wetu tunazitumia barabara hizo na huwa rahisi kwetu kutambua mitaa mbalimbali na kupata anwani inayotakiwa. Kama isingekuwa hivyo, watu waishio mjini wangepata taabu kuwasiliana.

Maelezo

1. Watu walitumia njia nyembamba "Люди ходили по узким дорожкам", ...magari huruhusiwa kuitumia (*barabara*)"машинам разрешено по ней (*дороге*) ездить". Выражение -tumia barabara "пользоваться дорогой" часто употребляется в значении "ходить/ездить по дороге".

2. Слово pembeni "в углу" также имеет значение "скраю", "в стороне" и т.п.: -kaa pembeni "сидеть в сторонке"; -simama pembeni mwa barabara "стоять на обочине дороги"; -sogea pembeni "отойти в сторону".

3. В Танзании правостороннее движение на дорогах, и руль в транспортном средстве расположен справа, а не слева, как принято в России. Поэтому пешеходу при переходе улицы рекомендовано в первую очередь посмотреть направо.

4. Порядковые числительные [la/ya] kwanza, [la/ya] pili, [la/ya] tatu и т.д. переводятся на русский язык такими вводными словами, как "во-первых", "во-вторых", "в-третьих" и т.д.

Mazoezi

7. Найдите в тексте эквиваленты следующих выражений: ходить пешком; разнообразные виды транспорта; доступный и популярный способ передвижения; гарантировать чистоту, надежность и долговечность дорог; строить дороги совместными усилиями; заниматься прокладкой дорог; тротуар; пешеходы и велосипедисты; принимать меры предосторожности; придавать большое значение безопасности; переход-зебра; пешеходный переход; светофор; переходить улицу не мешкая; четко видеть приближающийся транспорт; внезапно появиться из-за припаркованной машины; слева и справа от тебя; разделительная полоса; островок безопасности посреди улицы; длинные ряды зданий; присваивать имя; важные события в жизни; найти нужный вам адрес; испытывать затруднения при нахождении друг друга.

8. Дайте русские эквиваленты:
-enda kwa farasi; -fuga farasi; mfugaji wa farasi; -panda ngamia; maziwa ya ngamia; uchumi wa taifa; uchumi imara; uchumi hafifu; maendeleo ya kiuchumi; ujenzi wa kuta imara; ujenzi wa daraja; wajenzi wa nyumba; usalama wa kudumu; anwani ya kudumu; -dumu kwa muda mrefu; -hakikisha usalama wa nchi; -hakikisha maendeleo; mtu mwangalifu; askari mwangalifu; -acha mlango

wazi; swali wazi; -fahamu wazi; msururu wa magari; msururu wa milima; msururu wa watu; -ishi mtaa mmoja; mitaa ya mji; -jitokeza mtaani; -jitokeza ghafula; kivuko cha pundamilia; -safirisha gari kwa kivuko; tukio la hatari; matukio ya maisha; msururu wa matukio; mtu mwenye kubabaika; bila ya kubabaika; usibabaike; -wasiliana bila ya taabu; -wasiliana kwa njia ya kompyuta; -egesha gari mahali pa usalama; mahali pa kufaa kwa kuegesha magari; -kataza kuegesha gari; -chukua hatua za tahadhari; -tahadhari daima; taa za kuongoza magari.

9. Запомните следующие выражения и составьте с ними предложения:

-shuka juu ya farasi	спешиваться, слезать с лошади
-dumu daima	быть вечным
-wa/-kaa macho	быть бдительным, быть настороже
maegesho [ya magari, meli n.k.]	стоянка [автомобилей, судов и т.п.]

10. Замените подеркнутые слова синонимами:
1. Huyu ni <u>mtaalamu</u> mkubwa wa <u>kuunda</u> vyombo vya usafiri. 2. Karibu na pwani ya Zanzibar unaweza kuona wavuvi <u>chungu nzima</u> wakiwa ndani ya <u>mitumbwi</u> yao <u>mikuukuu</u>. 3. Watu wa <u>kabila</u> hili wana <u>uwezo</u> mkubwa wa <u>kusokota</u> nyavu za kuvua samaki. 4. Bandarini humu mna <u>mahali maalum pa kuweka</u> meli kubwa. 5. Unapoendesha gari katika <u>mitaa</u> ya mji mkubwa <u>inakubidi</u> kuwa mwangalifu kila dakika. 6. Barabara kijijini humu ni mbovu kabisa, unapaswa kuendesha gari kwa <u>taratibu</u>. 7. Mwalimu wetu wa historia anatumia lugha <u>inayofahamika vizuri</u>, hababaiki kama baadhi ya waalimu wengine. 8. Somo la hesabu lilidumu kwa saa mbili <u>badala ya</u> saa moja na nusu.

11. Замените конструкцию с предлогом kabla ya и инфинитивом личной формой глагола с показателем -ja-:
1. Kabla ya kuvuka barabara uhakikishe kuwa hakuna magari upande wa kulia wala kushoto kwako. 2. Kabla ya kulazwa

kitandani watoto walipewa maziwa ya moto. 3. Kabla ya mawingu meusi kujitokeza upepo mkali ulianza kuvuma. 4. Kabla ya barabara kutengenezwa mahali hapa palikuwa na kijia tu. 5. Kabla ya kivuko kujengwa ilikuwa haiwezekani kufikia ng'ambo ya pili ya mto huu. 6. Walikodi gari kabla ya kwenda safarini. 7. Kabla ya kuegesha motokaa yangu nilihakikisha kuwa sehemu hiyo ni yenye usalama.

12. Найдите в тексте предложения с модальными конструкциями и замените их синонимичными и формами.

13. Задайте 10 вопросов на суахили по содержанию текста и ответьте на них.

14. Переведите:

1. Работая на верхних этажах, строители обязаны принимать все меры предосторожности. 2. Крестьянам приходится быть бдительными, чтобы, во-первых, охранять свои поля от бабуинов и, во-вторых, защищать домашних животных от хищников. 3. Полицейские должны обеспечивать безопасность на дорогах и днем, и ночью. 4. Вам следует более четко назвать адрес друга, которого вы разыскиваете. 5. Строительство музыкальной школы в нашем районе должно завершиться до нового года. 6. Мы не обязаны принимать участие в этом событии. 7. Я не смог связаться с братом по телефону, и мне пришлось ехать к нему домой.

15. Переведите следующий текст, предварительно изучив новую лексику:

Maneno mapya

uhalifu (ед.) правонарушение, преступление
tabia (-) 1)характер, натура 2)привычка
hitilafu (-) дефект, недостаток; неисправность
tope (ma-) грязь; трясина, болото
bima (-) страхование
fidia (-) [денежное] возмещение, компенсация
kitendo (vi-) действие, поступок
utelezi (ед.) 1)скольжение 2)скользкое место
-teleza 1)быть скользким 2)скользить, поскальзываться
-ponda 1)раздавливать, разминать 2)переехать (*кого-л.*)
-laumu 1)упрекать, критиковать 2)обвинять
-jeruhi ранить
-elemisha учить, обучать, давать образование
-sababisha/ -sabibisha становиться причиной, вызывать
-kwama застревать, завязать
-kwepa/ -epa избегать, уклоняться
-onya предостерегать, предупреждать
-pisha давать дорогу, пропускать; уступать (*место*)

Ajali barabarani

Ingawa siku hizi watu hawafi sana kwa magonjwa kama hapo zamani, lakini wanakabiliwa na ajali za magari barabarani. Kila siku watu wengi hupondwa na magari na kujeruhiwa au kufa.

Mara nyingi ajali zinatokea kwa sababu magari yanaendeshwa mbio na madereva. Kuendesha gari kwa mwendo wa kasi sana ni uhalifu kwa sheria za usalama barabarani. Inaibidi serikali itoe adhabu kali kwa watu wanaovunja sheria hizo. Lakini adhabu kali peke yake haitoshi. Ni lazima wananchi waelemishwe juu ya sheria za usalama barabarani ili wao wenyewe wawakaripie madereva wenye tabia hizo. Dereva anaweza kuendesha gari au basi kwa mwendo wa kasi lakini abiria wamekaa kimya tu.

Baadhi ya madereva huwa wamelewa wanapoendesha magari. Hata hitilafu kwenye injini inaweza kusababisha ajali kubwa. Hata kuzidi kwa idadi ya abiria na mizigo katika vyombo vya usafiri kunaweza kusababisha ajali. Gari lililobeba abiria wengi kuliko uwezo wake linapopata ajali, watu wengi hupoteza maisha na wengine hujeruhiwa vibaya.

Vile vile wapandao baisikeli na wanaokwenda kwa miguu wanafaa kulaumiwa. Wapandao baisikeli mara nyingine huendesha baisikeli zao barabarani bega kwa bega bila kujali magari au watu wanaotumia barabara kama wao. Na watu wanaokwenda kwa miguu mara nyingi huwa si waangalifu.

Sababu nyingine zinazoleta ajali barabarani ni njia mbovu. Siku moja Doto, mke wa rafiki yangu aliamua kwenda shambani kuwatazama wazee wake. Doto ni dereva hodari, haendeshi mbio

maana anajua kuwa kukimbiza gari ni hatari. Njiani aliuliza habari za barabara kwa sababu mvua ilikuwa inanyesha usiku. Madereva wengine walimwonya kuwa njia ni mbaya sana, yenye matope mengi na utelezi. Basi Doto aliendesha polepole sana. Alikutana na lori moja ambalo dereva wake alikuwa akiendesha mbio. Doto alikwenda pembeni kumpisha na hapo alikwama vibaya sana. Kwa bahati nzuri lori lile lilikuwa na watu wenye nguvu. Walisaidia kusukuma gari la Doto na kulitoa kwenye matope. Basi ajali barabarani huletwa na sababu na vitendo kama hivyo.

Jambo muhimu vilevile ni kuelemisha wananchi wasikwepe kulipia magari yao bima. Wasipolipa bima ya magari, hawalipwi fidia ya magari yao yanapopata ajali.

Maelezo

1. Наречное слово vibaya "плохо" в зависимости от контекста может иметь различные эквиваленты в русском языке: -jeruhiwa vibaya "быть тяжело раненым"; -kwama vibaya "глубоко завязнуть"; -umwa vibaya "сильно болеть"; -piga vibaya "жестоко избивать".

2. Выражение bega kwa bega "плечом к плечу" имеет как прямой, так и переносный смысл: -enda bega kwa bega "ехать в одну линию/ рядом друг с другом"; -fanya kazi bega kwa bega "работать сообща/ дружно".

3. Слово mzee "старик" также может употребляться в значении "родитель" (чаще по отношению к отцу) или "почтенный человек" и как форма уважительного обращения: wazee wangu "мои родители"; mzee Juma "почтенный Джума"; mzee, niambie tafadhali "[уважаемый], скажите, пожалуйста".

Mazoezi

16. Дайте русские эквиваленты:
-fanya uhalifu mbaya; -tenda kitendo cha uhalifu; tabia nzuri; -jenga tabia; -acha tabia mbaya; -kagua hitilafu; -ondoa hitilafu; -kwama matopeni; -anguka topeni; njiani pamejaa matope; -kwama kazini; -teleza juu ya barafu; njia yenye utelezi; mahali panapoteleza;

-fanya bima ya gari; bima ya maisha; shirika la bima; cheti cha bima; -lipa fidia; -taka fidia; -ponda mboga; viazi vya kupondwa; -sababisha ajali; -sababisha ugonjwa; -kwepa ajali; -kwepa kulipa deni; -kwepa kazi ngumu; -laumiwa na rafiki; -laumiana; -onya juu ya hatari; -onya kwa wakati; -pisha lori; -pishana njiani; -pisha mtu kiti; -fuata sheria za usalama barabarani; -jeruhiwa vibaya; -umizwa vibaya; magari yamegongana vibaya.

17. Переведите:
1. Вас предупредили, что здесь очень грязно и скользко? 2. Все неисправности в нашей машине устранили еще до поездки. 3. В новом году все владельцы автомашин обязаны будут оформлять (*делать*) страховку. 4. Поступок нашего менеджера вызвал много вопросов, хотя нас и предупреждали о его скверном характере. 5. Водитель, который стал причиной аварии, уклоняется от уплаты компенсации и обвиняет нас в этом преступлении. 6. Детей с раннего возраста учат уступать место в транспорте пожилым людям. 7. Если водители и пешеходы будут соблюдать правила уличного движения, то можно будет избежать многих дорожных аварий.

18. Ответьте на вопросы по содержанию текста из упражнения 15:
1. Je, siku hizi kuna mambo gani yanayosababisha kufa kwa watu wengi? 2. Nini sababu muhimu zaidi za kutokea ajali barabarani? 3. Je, kitendo cha kutia adhabu peke yake kinatosha kwa kuzikwepa ajali barabarani? 4. Kwa nini Doto alipatwa na ajali njiani? 5. Nani alimsaidia katika balaa hiyo? 6. Kwa nini inafaa watu walipe bima za magari yao au bima za aina nyingine?

19. Перескажите текст из упражнения 15 от лица Дото.

20. Составьте на суахили небольшой рассказ на тему "Ajali barabarani". Используйте следующие слова и выражения: -sababisha utelezi; -onya juu ya hatari; -chukua tahadhari; -pisha; motokaa mbovu; -kwepa ajali; -egesha gari; kivuko cha pundamilia;

-kwama njiani; -angalifu; taa za kuongoza magari; -wasiliana na kituo cha polisi; -thibitisha; -laumu; -hakikisha kulipa bima.

* * *

Mazoezi ya kujiandaa kusikiliza hadithi

Maneno mapya

-paka накладывать (*краску*), мазать
-twanga толочь; молотить
-chubuka слезать (*о коже, шкуре*); получать ссадину
teke (ma-) удар ногой; пинок
-piga teke пинать, брыкаться
-a kijani зеленый
brashi, burashi (-) кисть, кисточка, щетка
-piga brashi чистить щеткой
kobe (ma-) черепаха
roho (-) 1)душа, жизнь 2)нрав, характер

Mazoezi

21. Запомните следующие выражения и составьте с ними предложения:

dawa ya kupaka	мазь
-paka mtu matope	обливать (*кого-л.*) грязью, (*перен.*) пятнать
-kata roho	лишаться жизни, умирать

22. Дайте русские эквиваленты:
-paka kuta rangi ya kijani; -paka dawa kwenye jeraha; -ondoa rangi; -twanga mbegu; -twanga majani; -changanya dawa na maji; -changanya rangi tofauti; -chubuka ngozi puani; -chubuka mkono; tabia ya kupiga teke; -pigwa mateke matatu; mwendo wa kobe; umri wa kobe; kisiwa cha kobe; -piga brashi nguo; -chora kwa brashi; -wa na roho mbaya; mtu mwenye roho njema; -tupa jiwe; -jitupa majini; -baki na kidonda; -baki na madoadoa machafu.

23. Дайте эквиваленты на суахили:
красить; покрасить дом масляной краской; смывать краску; купить мазь в аптеке; растолочь таблетку и смешать с водой; у него ссадины на ладонях; упасть с дерева и ободрать плечо; иметь дурную привычку обливать грязью других людей;

получить неожиданный пинок; зеленые глаза; зеленые полосы; хорошая кисть; выбросить старые кисти в мусорный бак; маленькая кисточка; человек с доброй душой; постоянно ссориться со всеми из-за плохого характера.

24. Переведите:
1. Pundamilia ana mistari mingi mwilini mwake, myeusi imechanganyika na myeupe. 2. Tunatamani nyumba yetu ipakwe rangi ya kijani ipendeze kwa vile rangi ya zamani imeshatoka. 3. Mwendo wako ni kama wa kobe, naomba twende mbio tusichelewe. 4. Mganga alitwanga dawa fulani ya majani akampaka mbwa wetu aliyepata vidonda kadhaa wakati akimfukuza kenge. 5. Mkulima anataka kumwuza punda wake apendaye kupiga teke. 6. Jirani yetu ana roho mbaya sana ingawa sura yake inapendeza. 7. Kijana alijitupa mtoni ili apate baridi kidogo.

25. Раскройте скобки, употребив желательно-побудительное наклонение. Образец:
Umwite daktari (-pa dawa, wewe) > Umwite daktari akupe dawa
1. Tunapaswa tufuge kuku (-patia mayai, sisi). 2. Inafaa tumlaze mjomba hospitalini (-pona, haraka). 3. Inakupasa umfunge pembeni mbwa wako (-topigwa teke, punda wetu). 4. Inanibidi kuondoa mafuta haya (-toharibu, ngozi yangu). 5. Hamna budi kuacha ugomvi wenu (-shirikiana, kazi hii). 6. Mwizi huyu lazima apelekwe kwenye kituo cha polisi (-pata, adhabu kali).

26. Образуйте сложно-подчиненные предложения по образцу и переведите их:
Nilimwona paka. Alimtafuna panya. >
Nilimwona paka akimtafuna panya.
1. Tulimwona nyoka. Alipanda mtini. 2. Nilimwangalia nyani. Alikula ndizi. 3. Unawaona tembo wale? Wanakunywa maji ziwani. 4. Nilimsikia mwenzangu. Alijitapa kwa kuwa na pesa nyingi. 5. Tulikuona dirishani. Ulichora picha ya mamako. 6. Tulimsikia shangazi. Alimkaripia mpishi jikoni. 7. Mama alijitokeza kwenye mlango. Alikuwa na pudini mikononi.

27. Раскройте скобки, употребив сравнительный оборот.
Образец: *Ngozi yake chafu (nguruwe) >*
Ngozi yake chafu kama ya nguruwe.
1. Roho yake mbaya (fisi). 2. Meno yake makali (simba). 3. Muziki huo ni mtamu (ndege). 4. Umri wake mkubwa (kobe). 5. Nywele za msichana ni ndefu (farasi). 6. Shamba lake kubwa (tajiri). 7. Mwendo wako mwepesi (mbuni). 8. Sumu yake kali (nyoka). 9. Mateke yake yana nguvu (farasi).

28. Переведите, используя желательно-побудительное наклонение подчеркнутых глаголов:
1. Я попросила родителей покрасить стены в моей комнате в другой цвет. 2. Они решили пойти на речку, чтобы немного поплавать. 3. Нам сказали остаться в классе и сделать все упражнения. 4. Я хочу, чтобы ты надела то зеленое платье, и мы пойдем в ресторан. 5. Я прошу тебя купить мне новые кисти, и я буду писать твой портрет. 6. Девочка мечтала, чтобы у нее были золотые серьги, как у бабушки.

Kusikiliza hadithi

- Прослушайте текст полностью.
- Повторите в паузах фразы вслед за диктором.
- Закончите предложения вместо диктора.
- Задайте друг другу вопросы на суахили по содержанию прослушанного текста и дайте на них ответы.
- Ответьте на суахили на вопросы диктора.
- Изложите письменно на суахили содержание текста.

* * *

Mazoezi

29. Переведите и выучите наизусть диалог:

Maneno mapya

gereji (ma-;-) гараж
mzunguko (mi-) оборот; поворот
njia ya mzunguko окольный путь, объезд, обход
tanki, tangi (ma-;-) бак
leseni (-) лицензия, удостоверение; права (*водительские и т.п.*)

Kukodi gari

Mtalii: Ninaweza kukodi motokaa hapa?
Mwenye gereji: Unataka uendeshe mwenyewe au unataka dereva akuendeshe?
Mtalii: Nina leseni, hivyo nataka niendeshe mwenyewe.
Mwenye gereji: Una safari ya kwenda wapi?
Mtalii: Nataka kwenda Mombasa.
Mwenye gereji: Unaitaka kwa muda gani?
Mtalii: Nitalirudisha gari baada ya siku tatu. Kukodi gari pamoja na petroli, bei yake nini?
Mwenye gereji: Itakubidi kulipa si chini ya shilingi laki moja na elfu hamsini.
Mtalii: Nini bei ya petroli hapa Nairobi?
Mwenye gereji: Galoni moja kwa shilingi 900.
Mtalii: Tafadhali jaza tanki.
Mwenye gereji: Ulipata kwenda Mombasa?
Mtalii: Hii ni mara yangu ya kwanza kwenda huko.
Mwenye gereji: Kama hivyo itakulazimu upate ramani ya njia.
Mtalii: Je, wewe una ramani hiyo?
Mwenye gereji: Hapana. Bora upite njia hii. Ni ya mzunguko kidogo, lakini haina magari mengi. Utalikuta duka kwenye njia panda.
Mtalii: Asante!
Mwenye gereji: Safari njema!

30. Переведите:
1. Я могу арендовать машину на два дня? 2. Я сам сяду за руль. 3. Сколько мне надо будет заплатить? 4. Сколько стоит литр бензина? 5. Залейте полный бак. 6. У вас есть дорожная карта? 7. Вам лучше выбрать объездной маршрут. 8. Ты должен поставить машину в гараж. 9. Вы можете припарковаться на обочине. 10. Покажите ваше водительское удостоверение. 11. Я еду туда впервые. 12. Спасибо, что пропустили меня. 13. Счастливого пути!

31. Запомните пословицу и подыщите ей русский эквивалент: **Tahadhari kabla ya hatari**

SOMO LA KUMI
Лексическая тема "Досуг и развлечения"

Грамматика

1. Глаголы **-zuia, -kataza.**
2. Недостаточный глагол **-ngali.**

Особенности функционирования глаголов *-zuia* "мешать, сдерживать, препятствовать, не разрешать" и ***-kataza* "запрещать, не позволять"**. После данных глаголов, как и в русском языке, может следовать инфинитивная форма:

Ugonjwa utawazuia kutembelea Afrika "Болезнь помешает им поехать в Африку".

Mwalimu alinikataza kusoma kitabu hiki "Учитель запретил мне читать эту книгу".

Как видно из приведенных примеров, глаголы -zuia и -kataza обычно требуют употребления объектных показателей. За этими глаголами может следовать **отрицательная** форма желательно-побудительного наклонения. При этом лицо и число субъектного показателя глагола в желательно-побудительном наклонении совпадают с лицом и числом объектного показателя:

Mvua ili***m***zuia ***a****s****i***ende disko "Дождь помешал ему пойти на дискотеку".

Mama ali***wa***kataza watoto ***wa****s****i***toke bustanini "Мать запретила детям выходить из сада".

Объектный показатель не употребляется лишь в пассивных формах глагола -kataza:

Imekatazwa watu kuingia hapa. = Imekatazwa watu wasiingie hapa "(*Людям*) входить сюда запрещено".

Недостаточный глагол *-ngali* имеет ограничительное значение: "еще/ все еще/ до сих пор/ пока еще быть (*в каком-либо состоянии*)". Как и другие недостаточные глаголы в суахили (например, -na, -li), этот глагол имеет ограниченную сферу спряжения и функционирования. Он спрягается **только** по лицам и сочетается:

а) с именем существительным или субстантивированным прилагательным:

Angali mgonjwa (для 3-го лица ед. числа возможен вариант ***yu***ngali mgonjwa) "Он все еще болен".

Tungali wepesi "Мы до сих пор легки (*на подъем*)";

б) в аналитических конструкциях предшествует смысловому глаголу, оформленному видо-временными показателями -na- или -me-, а также показателем условного наклонения -ki- (все три показателя передают значения определенного состояния: состояние в настоящий момент -na-, результатив -me- и длительность -ki-):

Kakangu wangali wanachunga ng'ombe "Мои братья пока еще пасут коров".

Baba angali amelala usingizi "Отец все еще спит".

Mbona mngali mkinywa chai? "Почему вы до сих пор пьете чай?"

Примечание: *Следует различать недостаточный глагол -ngali и его омоним – показатель нереального условного наклонения -ngali-: Angalikuja angalinikuta hapa "Если бы он пришел, он бы встретил меня здесь".*

Mazoezi

1. Замените инфинитив после глаголов -zuia и -kataza конструкцией желательно-побудительного наклонения и наоборот:

A/ 1. Polisi aliwazuia wezi kuingia dukani usiku. 2. Mvua ilituzuia kupanda mbegu jana. 3. Mwalimu aliwakataza wanafunzi kuingia darasani na simu za mkononi. 4. Homa ilinizuia kwenda disko mnamo Jumamosi iliyopita. 5. Kaka alinikataza kutumia gari lake. 6. Baba alimkataza mwanawe kusoma katika chuo cha wanahewa.

B/ 1. Hitilafu za simu zilinizuia nisisikie vizuri sauti ya rafiki yangu. 2. Kiongozi wa benki alikataza watumishi wasivute sigara ofisini. 3. Kelele nyingi za watoto zilimzuia babu asipate usingizi. 4. Mbona imekatazwa watu wasivue samaki ziwani humu? 5. Alijizuia asinywe pombe nyingi kupita kiasi. 6.

Mtumishi wa jumba la makumbusho alitukataza tusiguse vitu vya thamani.

2. Сделайте предложения отрицательными. Образец:
Alinizuia nisiende huko > Hakunizuia niende huko
1. Utelezi njiani ulinizuia nisiendeshe mbio motokaa yangu. 2. Watalii walikatazwa wasiingie katika eneo la kiwanda cha kupasua mbao. 3. Mtoto alizuiliwa asimpande ngamia yule. 4. Jirani alitukataza tusiweke basi letu kwenye gereji lake. 5. Vita ilimzuia dada yangu asihitimu katika chuo cha ualimu. 6. Balozi aliwakataza wasaidizi wake wasiende livu wakati huu.

3. Переведите, используя глагол -zuia или -kataza:
1. Наводнение помешало крестьянам подготовить свои поля к посадочному сезону. 2. Полицейский не позволил им припарковаться у здания музея. 3. В самолете нам запретили пользоваться фотоаппаратом. 4. Родственникам не разрешили навестить молодого человека, попавшего в автокатастрофу. 5. Тебе следовало бы удержать своего брата от поездки в этот опасный регион. 6. Почему нам запрещают пользоваться словарем на экзамене? 7. Я не могу удержаться от смеха, когда вспоминаю вашу свадьбу. 8. Если тебе не позволят заплатить наличными, придется выписать чек.

4. Переведите:
1. Wangali wanafanya kazi katika ujenzi wa njia ya reli. 2. Rashidi yuko wapi? - Angali anachunga mbuzi wake malishoni. 3. Wasichana hawa wangali na ubishi mwingi kati yao. 4. Bibi yungali mgonjwa, mpikie ubwabwa apate kula kidogo. 5. Mbinguni kungali na mawingu mengi meusi. 6. Makaburi ya askari waliokuwa wakilinda uhuru wa nchi hii, yangali yanatembelewa na wenyeji. 7. Tungali tukila. 8. Naona mamako yungali mzuri wa sura ingawa ameshakuwa mzee. 9. Mchezaji yule angali mwepesi na lazima atashinda katika mashindano yanayokuja. 10. Wageni wanachelewa kwa sababu wangali wamesimama katika msululu wa magari. 11. Nyumba zingali zikijengwa.

5. Замените подчеркнутые конструкции сказуемым с показателем -ngali:
1. Salum bado ni mtoto mdogo. 2. Bado nina matatizo yale yale. 3. Tunaendelea kuzipaka rangi kuta za nyumba yetu. 4. Amina anategemea wazazi wake mpaka leo. 5. Bwana yule bado ana majivuno mengi. 6. Hata leo wanaishi katika nyumba kuukuu. 7. Je, baba ameshaamka? - Hapana, bado ana usingizi. 8. Mbona unaendelea kuwa mjinga kama zamani?

6. Переведите, используя показатель -ngali:
1. Моя дочь все еще учится водить машину, но я надеюсь, что в марте она получит права. 2. Он все еще толстый, как и раньше, хотя перестал есть булочки, сливочное масло и свинину. 3. Праздник уже закончился, а разноцветные флаги до сих пор развеваются на центральной площади. 4. Мои братья пока еще маленькие, и пойдут в школу только в будущем году. 5. Я все еще помню запах тех цветов, которые росли в нашем саду много лет назад. 6. У нас до сих пор есть старые банкноты, которые были в ходу (*использовались*) после войны. 7. Ты все еще продолжаешь изучать китайский язык?

Maneno mapya

mfalme (wa-) правитель, царь, король
upole (ед.) 1)доброта 2)жалость, сострадание
ukarimu (ед.) радушие, гостеприимство
-kirimu 1)угощать 2)оказывать гостеприимство
bure 1)даром, бесплатно 2)напрасно, зря 3)бесплатный
kito (vi-) драгоценный камень
upenzi, upendo (ед.) любовь, расположение
jahazi (-; ma-) парусное судно
unga (ед.) 1)мука 2)порошок
chungu chungu в большом количестве, во множестве
mkubwa (wa-) 1)начальник, директор 2)предводитель
kuhusu о[б], относительно
-husu относиться, иметь отношение, касаться
-simamia 1)наблюдать, контролировать 2)управлять
-lisha кормить, давать пищу
-saga молоть, размалывать, толочь
jiwe la kusagia жернов
-ng'aa/-ng'ara блестеть, сверкать

jeshi (ma-) армия; войско
tamaa(-) страстное желание, страсть
isipokuwa исключая, кроме, за исключением
-pindua переворачивать, опрокидывать
-dai 1)требовать 2)утверждать, заявлять

Namna bahari ilivyotiwa chumvi

Zamani sana palikuwa na mfalme aliyejulikana pote kwa upole na ukarimu wake. Furaha yake ilikuwa katika kuwatunza na kuwalisha wageni maskini waliofika katika jumba lake.

Siku moja alipewa zawadi kutoka nchi nyingine na zawadi hiyo ilikuwa mawe ya kusagia mawili makubwa sana. Kumbe yalikuwa makubwa mno hata hapakuwa na mtu katika nchi yake aliyeweza kuyatumia, yakakaa bure. Lakini kwa kweli mawe yale yalikuwa ya ajabu sana, maana yakitumiwa, badala ya kusaga unga, hutoka furaha na fedha na dhahabu na upenzi na vito vya thamani. Lakini ya nini? Hakuna mtu aliyeweza kusaga kwa mawe yale.

Ikatokea siku moja mfalme alikuwa akitembea akakutana na wanawake wawili waliokuwa wakubwa mno, akawakaribisha wafuatane naye jumbani mwake. Walipoingia jumbani akawauliza, "Je, nyinyi ni wanawake wakubwa wenye nguvu nyingi, mnaweza kusaga kwa mawe haya?" Akawaonyesha yale mawe, wakajibu, "Ndiyo, tunaweza. Unataka tukusagie kitu gani?" Mfalme akajibu, "Nisagieni dhahabu nipate kuziona." Basi wanawake wakaanza kusaga, na dhahabu nyingi zikatoka, ziking'aa sana. Mfalme alipoziona dhahabu ziking'aa, macho yake yakabadilika, akalia, "Haya sageni, sageni dhahabu chungu chungu." Na wale wanawake wakazidi kusaga.

Yule mfalme alidai wanawake hawa wazidi kusaga mchana kutwa kwa siku nyingi. Aliwakataza wasiache kazi kabisa, isipokuwa nafasi kidogo wapate kula upesi. Ikawa moyo wake ulikuwa mgumu kwa choyo ya kupata dhahabu nyingi, wala hana nafasi ya kuwatunza na kuwakirimu watu wake. Kazi yake yote ilikuwa kuwasimamia wale wanawake wazidi kumsagia dhahabu chungu chungu, akasahau kuwa mawe yale yanaweza kutoa furaha na upenzi, akafikiri kuhusu dhahabu tu.

Basi wanawake walichoka sana, na ingawa walikuwa na nguvu ya ajabu, lakini walishindwa kuendelea, na wakati wote walizuiliwa wasipumzike. Kwa bahati wakati waliposaga yule mfalme alikuwa ameshikwa na usingizi, na wanawake hao walipoona hivi, wakafikiri namna ya kujiokoa katika mikono yake. Wakaanza kusaga, kumbe walitoa askari jeshi zima katika mawe yale. Wakamshika mfalme angali na usingizi wake, wakamwua, wakayachukua yale mawe wakaenda pwani.

Walipofika pwani waliona jahazi, wakaingia ndani pamoja na mawe yale. Walipokwenda kiasi, mkubwa wa askari alifikiri kuwa watu wake watapenda kuona namna yale mawe yanavyoweza kufanya kazi, akawaita wanawake wale, akasema, "Chumvi ni kitu kizuri, basi tusagieni chumvi nyingi, na tukifika mjini tutaiuza kwa bei nzuri."

Basi wale wanawake walianza kusaga chumvi chungu chungu, na yule mkubwa wa askari alipoona chumvi nyeupe namna ilivyong'aa, alishikwa na tamaa ya fedha, akawahimiza na kudai wazidi kusaga chumvi chungu chungu.

Jioni ikaja na wanawake wale walisema, "Haya bwana, lazima tupumzike sasa. Tumechoka mno." Lakini mkubwa aliwakataza wasiache kazi yao, aliwalazimisha wazidi kusaga chumvi, akasema, "Haya, haya, sageni! Nyinyi wanawake wavivu! Hamwezi kukaa bure katika jahazi letu."

Basi wale wanawake wakasaga, wakasaga mpaka uzito wa chumvi ulipopindua jahazi, likazama mpaka chini ya bahari. Lakini hata hivyo wanawake hawakupumzika, maana askari wale walikufa kwa maji, kwa hivyo hapakuwa na mtu kuwaambia waache kusaga. Basi, sasa maji ya bahari yana chumvi nyingi, na wale wanawake wangali wanaisagia chumvi.

Maelezo

1. Слово namna "вид", "род" в сочетании с релятивным показателем -vyo- вводит придаточное предложение образа действия: Mwalimu alipenda namna tulivyoitafsiri sentensi ile ngumu "Преподавателю понравилось, как мы перевели то трудное предложение"; Sijui namna awezavyo kuwahi kila kitu "Я не знаю, каким образом он все успевает". Сравните

употребление местоимения vile: ...vile tulivyotafsiri...; ...vile awezavyo...

2. Walipokwenda kiasi ... "Немного отъехав ..." Слово kiasi "мера", "количество" может употребляться в качестве наречия со значением "немного", "умеренно", "недолго" и т.п.: Anakula kiasi "Он питается умеренно"; Tuliwasubiri kiasi tukaenda zetu "Мы подождали их недолго и поехали домой".

Mazoezi

7. Найдите в тексте суахилийские экиваленты следующих выражений:
известный своей добротой и радушием; жернова лежали без дела; но какой от них толк?; позвал их к себе; его глаза преобразились; круглые сутки в течение многих дней; запретить прекращать работу; кроме небольшого перерыва на еду; единственной его заботой было наблюдать за ними; все его мысли были только о золоте; обладать удивительной выносливостью; думать о том, как спастись; пока он спал; целая армия; продать по высокой цене; быть охваченным жаждой денег; находиться в лодке; лодка опрокинулась под тяжестью соли; пойти на дно; утонуть.

8. Запомните следующие выражения и составьте с ними предложения:

jeshi la anga	военно-воздушные силы
-kata tamaa	отчаиваться, падать духом
-jidai	притворяться, прикидываться

9. Приведите русские экиваленты:
-wa na choyo kupita kiasi; choyo ya mfalme; jeshi la mfalme; mkubwa wa jeshi; -kusanya jeshi; nguo ya kijeshi; jeshi la usalama; mkubwa wa maktaba; mkubwa wa kiwanda; tabia ya upole na ukarimu; -pokea wageni kwa ukarimu; -kirimu watu maskini; -lisha mtoto; -lisha wanyama; mawe ya kusaga; -saga mahindi; unga wa mahindi; unga wa sabuni; sukari ya unga; -pindua kiti; -pindua bakuli; jahazi lililopinduka; jahazi lenye raha; -dai madeni; -dai mali; -dai uhuru; -dai kuongezewa mshahara; -jidai kuwa mgonjwa; -jidai kuwa mkubwa; -wa na tamaa ya fedha; -kosa tamaa; elimu bure; kazi bure; -jitahidi bure; vito chungu chungu; kito chenye thamani isiyopimika; -ng'aa kama dhahabu; -ng'aa juani; -ng'aa gizani; macho yenye kung'aa; -simamia askari; -simamia ujenzi; -simamia wafanya kazi; yote yanayohusu afya; sheria zihusuzo jeshi; maswali yenye kuhusiana.

10. Замените синонимами подчеркнутые слова и выражения:
1.Mganga huyu ana huruma nyingi kwa wagonjwa wake. 2. Mkubwa wao hukaa macho daima, huwakataza wajenzi wasikae ovyo. 3. Hamu yake ya kupata pesa nyingi mno haina kiasi. 4. Kwa bahati mbaya hatujui mengi juu ya mabaharia waliosafiri na jahazi lile. 5. Mkulima alikwenda kwa jirani kutwanga mahindi yake ili apate unga. 6. Baada ya kushindwa mtihani wa mwisho alikufa moyo kabisa. 7. Mbona unapenda kujifanya mjinga? 8. Wageni walikaribishwa vizuri katika ubalozi wa Tanzania. 9. Mtu anayekagua kazi yao yungali likizoni sasa.

11. Подтвердите или опровергните следующие утверждения в соответствии с содержанием текста:
1. Mfalme aliyeishi zamani sana alijulikana kwa upole na ukarimu wake kwa wote isipokuwa watu maskini tu. 2. Zawadi aliyopewa siku moja ilimfanya mfalme huyo kubadilika kabisa roho na tabia zake. 3. Mawe ya kusagia yalikuwa yakikaa bure kwa muda mrefu kwa sababu mfalme huyo hakujua kuwa ni mawe ya ajabu. 4. Siku moja wanawake wawili walikuja jumbani mwake na kumweleza mfalme kuhusu siri ya mawe yale. 5. Mawe ya kusagia yaliweza kutoa kila kitu isipokuwa upenzi tu. 6. Mfalme aliwalazimisha wanawake kumsagia dhahabu mchana kutwa siku nyingi bila ya kuwaruhusu kupumzika. 7. Mfalme aliacha kuwatunza na kuwakirimu watu wake kwa sababu ya kushikwa na tamaa ya kupata dhahabu nyingi. 8. Wanawake walimwua mfalme yule kwa kumpiga kichwani kwa jiwe la kusagia. 9. Mkubwa wa askari aliamua kupata chumvi chungu chungu ili kuiuza kwa bei nzuri. 10. Jahazi lilizama kwa sababu ya uzito wa mawe ya kusagia na unene

wa wanawake wale. 11. Wale wanawake wangali wanasaga chumvi baharini kwa sababu hakuna mtu kuwazuia wasiendelee na kazi hiyo.

12. Передайте коротко на суахили содержание текста.

13. Ответьте на следующие вопросы:
1. Ungalikuwa mfalme ungalisimamia watu wako kwa mtindo gani? 2. Ungalipata mawe ya ajabu ungalitumia mawe hayo kwa kujisagia kitu gani? 3. Je, kama ungalipata fedha chungu chungu tabia yako ingalibadilika namna gani? 4. Nini maoni yako, tabia ya binadamu hutegemea hali yake ya kuwa maskini au tajiri? 5. Je, ungependa kuwa mkubwa wa jeshi la askari?

14. Переведите:
1. Кто здесь начальник? У меня есть важные новости о строительстве вашей лаборатории. 2. Посмотрите, как истощали животные в вашем загоне. Когда их кормили в последний раз? 3. Судно перевернулось и пошло ко дну из-за большого количества пассажиров и грузов. 4. Он все еще руководит этим предприятием и требует, чтобы все ему подчинялись. 5. Студентам не позволили пользоваться компьютером бесплатно. 6. Мой брат загорелся страстью пойти учиться в военное училище, а родители всячески ему препятствуют. 7. Хозяин лавки все такой же скупой, как и раньше, и не перестает утверждать, что все покупатели мечтают о том, как украсть его драгоценные камни. 8. Исторический музей открыт все дни за исключением воскресенья. 9. Ты видел, как горят глаза у кошки в темноте?

15. Переведите следующий текст:

Maneno mapya

kisa (vi-) история, рассказ, сказка
jamii (-) 1)общество, коллектив 2)род, семейство
mkonga (mi-) хобот
yowe (ma-) крик, вопль
-piga yowe кричать, вопить
-tangulia идти впереди; опережать (*кого-л., что-л.*)

desturi (-) 1)обычай, традиция 2)привычка, обыкновение
mfuko (mi-) 1)карман 2)сумка, портфель, кошель
sarafu (-) 1)монета, мелочь 2)валюта
kundi (ma-) группа; отряд
hatima (-) конец; результат; заключение
mkasa (mi-) случай, приключение; просшествие
jinsi (-) способ; метод, манера

Tembo barabarani

Mwezi wa Agosti mwaka uliopita tulikwenda sote jamii yetu kumwamkia mjomba wangu ambaye anafanya kazi ya serikali mjini Voi. Kwa hivyo tulikuwa tukifuata ile barabara kuu inayokwenda kutoka Nairobi mpaka Mombasa. Karibu saa nne tulikuwa tukipita sehemu iitwayo Tsavo. Ghafula tuliona tembo wengi mbele yetu barabarani. Baba yangu alisimamisha motokaa ili afikiri tuwapiteje. Barabarani hakukuwa na nafasi yo yote kwa sababu tembo walikuwa wengi sana. Baba alizungumza na mamangu, wakakata shauri kungoja tu. Baada ya dakika tano au kumi tembo wote walitoka barabarani, wakaingia msituni, ila mmoja mkubwa aliyebaki katikati ya barabara.

Babangu alitia moto motokaa, akaiendesha pole pole, mbele kidogo. Yule tembo alitikisa kichwa chake kikubwa, akainua mkonga wake akalia kwa sauti ya juu mno. Babangu alirudisha motokaa nyuma. Tukangoja. Tembo hakuenda.

Baada ya robo saa lilifika hapo lori kubwa sana, likasimama nyuma yetu. Lori hilo lilikuwa la petroli. Dereva alimwona tembo barabarani, akaanza kucheka. Alitoka katika lori, akaja na kusimama mlangoni pa motokaa yetu, akamwuliza babangu, "Nikusaidie bwana?" Babangu alimjibu, "Ndiyo. Yule tembo anatuzuia tusipite, lakini sijui tutamfukuza jinsi gani". Dereva wa lori alisema, "Mimi hupita hapa mara nyingi kila wiki. Kwa desturi barabarani huku tembo wanapenda kuvuka. Lakini mimi siwajali maana najua tembo huogopa lori kubwa kama langu. Tufanye hivi. Mimi nitatangulia katika lori langu nawe uje nyuma yangu."

Babangu alikubali, dereva alianza kurudi kwenye lori lake. Kabla hajaingia ndani, alitia mkono wake mfukoni kutoa ufunguo wa lori na kwa bahati sarafu tatu au nne zilianguka kutoka mfukoni

mwake. Sauti yake ilikuwa ndogo, lakini ilimfanya tembo kukasirika, akaanza kutukimbilia. Tulipomwona tembo akija, sisi sote tulipiga mayowe, dereva akarukia ndani ya lori akalitia moto upesi. Tembo alipos ikia sauti ya lori ikinguruma, alisimama.

Dereva aliendesha lori pole pole kumwelekea tembo. Tembo akafanya makelele mengi. Dereva alisukuma lori mbele zaidi. Tembo hakuenda hata hatua moja. Mara dereva alipiga honi ya lori lake ambayo ina sauti ya juu kabisa. Alipos ikia sauti hii, tembo aligeuka upesi, akakimbilia msituni kufuata tembo wengine wa kundi lake.

Sisi tulifuata lori hilo nyuma mpaka tukapapita mahali pale penye tembo, baadaye tukalipita lori lile. Hatukuona tembo wengine wo wote, wala hatukuwa na mikasa mingine njiani. Hatimaye tukafika mjini Voi.

Maelezo

1. Sauti yake ilikuwa ndogo... "Их (*монет*) звук был негромкий...". Следует иметь ввиду, что притяжательное местоимение мн. числа -ao "их" обычно употребляется только с одушевленными существительными, а также с неодушевленными существительными, являющимися "частью", "собственностью" одушевленных: tembo na watoto wao "слоны и их детеныши", watu na sauti zao "люди и их голоса". Для неодушевленных предметов следует употреблять местоимение ед. числа -ake даже в том случае, когда их "часть", "собственность" стоит во мн. числе: malori na madereva wake "грузовики и их водители", maduka na bidhaa zake "магазины с их товарами".

2. Tembo akafanya makelele mengi "Слон издавал громкие звуки". Замещая исходные префиксы префиксом 3-го класса, существительные других именных классов (в данном случае 5-го класса – kelele "шум") приобретают увеличительное значение. Например: lango "ворота" < mlango "дверь"; jitu "великан" < mtu "человек"; jiji "мегаполис" < mji "город". Уменьшительное же значение некоторые слова могут

приобретать, попадая в 4-ый именной класс: kijia "тропинка" < njia "дорога"; kitoto "младенец" < mtoto "ребенок".

3. Hatimaye – слитная форма hatima yake. Переводится как "наконец", "в конце концов", "в заключение" и т.п.

Mazoezi

16. Дайте русские эквиваленты следующих выражений и составьте с ними предложения на суахили:
-piga yowe la hofu; -toa pesa mfukoni; -tangulia kuja; -fuata desturi; sarafu za kigeni; elimu (ya) jamii; visa vya kutisha; uamuzi wa hatimaye.

17. Закончите предложения:
1. Mkono wa tembo unaitwa ... 2. Kutangulia maana yake ni ... 3. Neno "kisa" lina maana ya ... 4. Kusema "kwa desturi" ni sawa na kusema ... 5. Pesa za chuma zinaitwa ... 6. Neno la "hatimaye" lina maana sawa na neno ... 7. Kupiga mayowe kuna maana ya ... 8. Kundi la watu linaitwa ... 9. Watu hubeba pesa zao au vitu vyao ndani ya kitu kiitwacho ...

18. Переведите:
1. В конце концов, мы благополучно выбрались из болота за исключением того, что все устали и промокли. 2. Я все еще дрожу от страха после того случая. 3. Группа полицейских, которая шла впереди, сдерживала людей и не давала им приблизиться к центру города. 4. Возможно, ты потерял ключ от чемодана, когда искал мелочь в кармане. 5. Многие африканские народы до сих пор следуют своим родовым традициям. 6. Сначала все услышали крики радости, а потом увидели группу студентов, направлявшихся к стоянке машин. 7. Обычно результатом любого правонарушения является наказание.

19. Перескажите на суахили рассказ из упражнения 15.

20. Вставьте вместо точек соответствующее притяжательное местоимение:
wakulima na mashamba ...; meli za mizigo na mabaharia ...; miti na matawi...; mito na kingo ...; wanafunzi na juhudi ...; ndege wa porini na mabawa ...; makoti na mifuko ...; mfalme na majumba ...; miji na mitaa...; wazee na shida ...; maduka na bidhaa ...; majengo na mapaa ...; viwanda na wafanya kazi ...; viongozi na kundi ...; kazi za ujenzi na matokeo ...

* * *

Mazoezi ya kujiandaa kusikiliza hadithi

Maneno mapya

-eneza распространять; разносить
fujo (-) путаница, неразбериха; беспорядок
swala (-) импала (*антилопа*)
hasira (-) гнев, ярость, злоба

21. Дайте русские эквиваленты:
-eneza uongo; -eneza ukweli; -eneza habari; -eneza ugonjwa; -fanya fujo; fujo kubwa; -leta fujo; -maliza fujo; -zuia fujo; tabia ya kupenda fujo; -shikwa na hasira; -jizuia na hasira; -jibu kwa hasira; tembo aliyepatwa na hasira; -vunja shingo; -vunja mkono; -wa na wivu; -kalia kiti; kiti cha kukalia mfalme; -wamba kiti kwa ngozi.

22. Дайте эквиваленты на суахили:
внести путаницу; полная неразбериха; устранить причину беспорядков; распространять газеты; разносить еду; насекомые, распространяющие малярию; разъяренный зверь; разгневанный человек; почувствовать злобу; лживые слова; поверить в ложь; сломать ногу; свернуть шею; переломать кости.

23. Составьте предложения со следующими словосочетаниями:
kwa hasira; kwa upole; kwa amani; kwa hofu; bila kusita; bila ya kuona huruma; bila upendo.

24. Переведите:
1. Wafugaji walikutana mara kwa mara kuzungumza kuhusu shida za kukosa malisho mahali pao. 2. Mtoto huyu anaona wivu kwa sababu hana mpira mkubwa kama watoto wenzake. 3. Mbona unaeneza uongo ukidai kuwa mamako anakuzuia usicheze nasi? 4. Ngozi ya mamba inafaa kutengenezwa mifuko na kanda nzuri, ingawa sheria za nchi fulani zinakataza wanyama hawa wasiuawe. 5. Tulimwona chui akimrukia swala, kumvunja shingo na kumtafuna mifupa yake. 6. Jamaa walipokutana tena kila mmoja alikuwa na furaha na upendo na kusahau hasira yake. 7. Kaka yangu alivunjika mguu alipokuwa na hasira na kulipiga teke kwa nguvu gari lake bovu.

25. Закончите предложения, подобрав подходящий вариант из тематического ряда, в который входит подчеркнутое слово:
1. Jamii yangu yote ilikusanyika mnamo siku ya uhuru isipokuwa ... 2. Fundi ameleta vifaa vyote vya ujenzi isipokuwa ... 3. Usiku ule wezi walituibia mali zote za nyumbani isipokuwa ... 4. Kila asubuhi wanyama wote hukutana penye ziwa isipokuwa ... 5. Duka hili la zawadi liko wazi siku zote isipokuwa ... 6. Funguo za vyumba vyote vya ofisini ziko hapa isipokuwa ...

26. Переделайте предложения по образцу и переведите их:
walianza kucheka > wakawa wanacheka > wangali wanacheka
1. Tulianza kuishi kwa hofu na hasira. 2. Walianza kukutana kila siku. 3. Fisi alianza kueneza uongo. 4. Wanyama walianza kupigana kwa nguvu na kuuana. 5. Kitoto cha swala alianza kutunzwa zizini. 6. Maisha yao yalianza kuwa na fujo kubwa. 7. Hasira ya kudumu ilianza kuiharibu tabia yake.

27. Переведите:
1. Молодые люди начали регулярно встречаться после работы и ходить на дискотеку. 2. Многие испытывали зависть, глядя на их радостные лица. 3. Следует помешать ему в распространении этой грязной лжи. 4. Кожа бегемота очень жесткая и не годится для изготовления сумок или пошива

одежды. 5. Жители деревни подскочили к вору и стали избивать его, не останавливаясь ни на секунду. 6. Они были охвачены гневом и переломали ему все кости.

Kusikiliza hadithi

- Прослушайте текст полностью.
- Повторите в паузах фразы вслед за диктором.
- Закончите предложения вместо диктора.
- Задайте друг другу вопросы на суахили по содержанию прослушанного текста и дайте на них ответы.
- Ответьте на суахили на вопросы диктора.
- Изложите письменно на суахили содержание текста.

* * *

Mazoezi

28. Переведите следующий диалог:

mjanja (wa-) 1)обманщик, плут 2)хитрец, ловкач
ncha (-) 1)остриё 2)оконечность
kamba (-) веревка, канат
-tania 1)шутить, подшучивать 2)дразнить

Sungura mjanja

Siku moja simba alikuwa na njaa sana. Bahati nzuri alimwona sungura akipita. Alimrukia akamkamata. Sungura alimwomba simba asimwue. Mazungumzo yao yalikuwa hivi:

Sungura: Rafiki yangu simba, vipi, mbona unanikamata?
Simba: Nina njaa sana. Nataka kula nyama yako.
Sungura: Sikiliza mfalme wa wanyama, mimi ni mdogo sana. Ukinila huwezi kushiba.
Simba: Sisemi maneno mengi. Kusema kunalisumbua tumbo langu na kuniongezea njaa.
Sungura: Ni kweli mfalme wetu. Ehee, mfalme, nimekumbuka.
Simba: Umekumbuka nini?
Sungura: Nilimkuta ng'ombe mkubwa njiani. Ukimpata huyo utakula mpaka ushindwe.
Simba: Yuko wapi?

Sungura: Subiri mfalme wetu, nitakuonyesha mahali pake.
Simba: Nionyeshe upesi!
Sungura: Mimi ninaona huna nguvu za kumkamata kwa sababu una njaa. Huyo ng'ombe ni mnene sana. Mimi nitamkamata.
Simba: Usinitanie! Wewe una nguvu gani?
Sungura: Ndiyo bwana, mimi sina nguvu, bali nitamfunga miguu, halafu wewe utamvuta.

Sungura alisokota kamba ndefu sana. Alimpa simba ncha moja ya kamba hiyo. Ncha ya pili sungura akajifunga kiunoni. Alimwambia simba kwamba akisikia sauti, avute kwa nguvu. Sungura akaanza safari ya kumfuata ng'ombe. Alipoingia vichakani akakutana na fisi. Wakaanza kuzungumza.

Sungura: Ndugu fisi, ninamvuta ng'ombe mkubwa sana. Sasa ananishinda.
Fisi: Wewe huna nguvu. Nifunge mimi hiyo kamba.

Sungura alimfunga fisi kamba kiunoni. Fisi alishukuru sana. Sungura akapiga kelele akasema, "Vuta! Vuta! "Simba alivuta na fisi akavuta. Simba aliendelea kuvuta kwa nguvu zake zote. Hatimaye alimshinda fisi na kumtoa vichakani. Simba alishangaa kuona kwamba alichokuwa anavuta hakikuwa ng'ombe bali ni fisi. Simba akapandwa na hasira isiyosemeka kwa sababu sungura alimdanganya. Basi, simba alimpiga fisi makofi na kisha kumwachia kwenda zake.

29. Найдите в диалоге из упражнения 28 сухилийские эквиваленты следующих выражений:
царь зверей; как же так; почувствовать сытость; быть многословным; усиливать голод; наесться до отвала; не шути со мной!; связать ноги; плести веревку; другой конец веревки; завязать себе на талии; тянуть со всей силой; прийти в неописуемую ярость; отшлепать кого-либо; отпустить кого-либо восвояси.

30. Выучите наизусть диалог из упражнения 28 и разыграйте его в лицах.

31. Переведите следующий рассказ и перескажите его на суахили:

Maneno ya kusaidia tafsiri

kwa kituo; kwa kirefu	подробно
Sana tena!	Еще бы!
Isipokuwa (kitu kimoja tu)...	Вот только ...
kila mmoja na (*mpira wake, kitu chake n.k.*)	каждому по (*мячу, предмету и т.п.*)

Однажды молодой человек пригласил любимую девушку на футбольный матч. Так как девушка никогда до этого не была на спортивных соревнованиях, юноша подробно объяснил ей правила игры в футбол. Во время игры девушка, как и все другие зрители, прыгала, кричала, апплодировала.

После окончания матча юноша спроил девушку:

- Ну как, тебе понравилась игра?

- Еще бы! – ответила девушка. – Все было очень интересно. Вот только мне кажется, что напрасно игроки гоняли по полю всего один мяч. Разве нельзя дать им двадцать два мяча: каждому по мячу?

32. Переведите вопросы и задайте их друг другу:

1. Что ты любишь делать в выходные дни? 2. Обычно ты отдыхаешь один или в обществе друзей и родных? 3. Какой вид спорта ты предпочитаешь - футбол, волейбол, баскетбол? 4. Может быть, ты любишь плавать? 5. Какие развлечения ты любишь? 6. Ты ходишь на дискотеку? 7. Какая музыка тебе нравится больше, современная или традиционная? 8. Ты предпочитаешь быстрые танцы или медленные? 9. Ты любишь разыгрывать своих друзей? 10. Какие интересные приключения случались в твоей жизни?

33. Запомните пословицы и подыщите им русские эквиваленты:

А/ **Hasira [ni] hasara**

В/ **Kamba hukatika pembamba**

SOMO LA KUMI NA MOJA
Лексическая тема “В гостинице”

Грамматика

Словообразование имен существительных. Существуют несколько способов именного словопроизводства, из них более продуктивные способы представлены именным отглагольным словообразованием и словосложением.

При помощи именных словообразовательных суффиксов ***-i, -ji, -o, -e, -u*** можно образовать огромное количество производных существительных. Наиболее продуктивными являются суффиксы ***-i, -ji, -o,*** которые могут сочетаться практически с любым из именных префиксов-показателей класса, но более часто встречаются следующие словообразовательные модели (в скобках приведены основные значения дериватов, складывающиеся из суммы значений именного префикса и суффикса):

m-...-ji (агент действия): -sikiliza “слушать” > msikilizaji “слушатель”, -soma “читать” > msomaji “читатель”;

m-...-i (агент действия, профессионал, специалист): -pika “готовить еду” > mpishi “повар”, -soma “читать, учиться” > msomi “ученый”;

m-...-o (результат действия): -panga “планировать” > mpango “план”, -kutana “встречаться” > mkutano “собрание”;

0...-o (результат действия): -soma “учиться” > somo “урок”, -chagua “выбирать” > chaguo “выбор”;

ma-...-o (результат действия): -endelea “продолжать, идти вперед” > maendeleo “прогресс», -patana “договариваться” > mapatano “договор”;

ki-...-o (результат действия или предмет): -lia “кричать” > kilio “крик”, -funika “закрывать” > kifuniko “крышка”.

Суффиксы ***-i, -ji, -o*** могут сочетаться с префиксом ***u-***, который придает деривату абстрактное значение агентивности, процессуальности, результативности (в зависимости от лексической семантики исходного глагола): -shinda “побеждать” > ushindi “победа”, -shona “шить” > ushonaji

"процесс шитья", -shirikiana "сотрудничать" > ushirikiano "сотрудничество".

Суффикс ***-ji*** присоединяется непосредственно к корню/основе глагола, оканчивающемуся на -a: -nywa "пить" > kinywaji "напиток", -piga > -pigana "бить > бороться за что-либо" > mpiganaji "борец".

Суффикс ***-o*** вытесняет конечный гласный -a: -enda "идти" > mwendo "ход, движение", -badilika "изменяться" > mabadiliko "изменение, реформы".

Примечание: *разница в значениях суффиксов -i и -ji не значительна, но хорошо прослеживается на таком примере как: Nani ni mpikaji leo? Mpishi Juma "Кто сегодня готовит еду? Повар Джума".*

Суффикс ***-i*** вытесняет конечный гласный -a, но при этом, как правило, происходят следующие чередования конечного согласного глагола:

d, g > z: -linda "охранять" > mlinzi "сторож", -jenga "строить" > mjenzi "строитель";

k > sh: -pika "готовить еду" > mpishi "повар";

t > s: -fuata "следовать" > mfuasi "последователь, сторонник".

Если глагол оканчивается на два гласных, то при присоединении суффикса ***-i*** последний вытесняет конечный -a и происходит чередование интервокального l > z (этот интервокальный согласный опускается в суахили, но восстанавливается при образовании направительной и пассивной форм глагола):

-k***aa*** "жить, пребывать" > makazi "место жительства, жилье",

-chag***ua*** "выбирать" > uchaguzi "выборы",

-said***ia*** "помагать" > msaidizi "помощник",

-l***ea*** "воспитывать" > mlezi "воспитатель",

-koh***oa*** "кашлять" > kikohozi "кашель".

Словосложение. Самой продуктивной моделью словосложения является "существительное + (посессив) + существительное: mbwa wa mwitu > mbwa mwitu "волк". Большая серия названий людей по их профессии, роду занятий, принадлежности к партиям, обществам и т.п. образуется в том случае, когда в роли первого существительного используется слово ***mwana*** "сын": mwanachama "член партии", mwanahistoria "историк", mwanamji "горожанин".

Место первого существительного могут занимать также такие слова как bwana "господин", fundi "мастер", askari "солдат" или mwenye "хозяин, собственник": bwanashamba "помещик", fundiumeme "электрик", askari polisi "полицейский", mwenyekiti "председатель". Как видно из примеров, значение производного слова складывается из суммы значений его составляющих.

Значительной продуктивностью отличаются также сложные слова, в которых первое место занимают отглагольные существительные, образованные только префиксальным способом от переходных глаголов. Переходный глагол сохраняет управление и в производном существительном, присоединяя к нему другое существительное – дополнение: -fanya "делать что-либо" > mfanyakazi "рабочий", -fungua "открывать что-либо" > kifungua kinywa "первый завтрак" (*букв.* "что-то, открывающее рот"), -pita "проходить по чему-либо" > mpita njia "прохожий" и др.

Примечание: *в силу отсутствия четких правил орфографии в суахили сложные слова могут писаться слитно или раздельно.*

Mazoezi

1. Образуйте существительные от основ следующих глаголов по заданным моделям. Определите значение новых слов:

A/ *-chunga > mchungaji:* -endesha, -tunga, -kimbia, -pasua, -ua, -kwea;

-tumia > *utumiaji:* -imba, -ogelea, -unda, -chora, -shona, -tafuta, -zima;

B/ *-jenga* > *mjenzi*: -kaa, -kagua, -amua, -jua, -okoa, -lea;
-teleza > *utelezi:* -chukua, -saidia, -vumbua, -tambua;

C/ *-vuna* > *vuno:* -pata, -tangaza, -gusa, -waza, -tisha, -chagua, -tegemea, -chubuka, -lalamika, -onya;
-panga > *mpango:* -sema, -ruka, -ita, -tetemeka, -alika, -cheka, -kataza, -elekea;
-kaanga > *kikaango:* -pamba, -funga, -soma, -pata, -imba, -lia, -ficha, -tisha, -lima; -pima;
-pumzika > *mapumziko:* -pendelea, -tengeneza, -tayarisha, -uliza, -lipa, -patana, -furika, -badilishana;

2. Определите значения следующих существительных, исходя из значений известных вам основ:

A/ msikilizaji, mzururaji, mtekelezaji, msomaji, mlipaji, ulimaji, upimaji, utoaji, uvunaji, usukaji, ukataji;

B/ maoni, mshindi, usemi, utumishi, ugunduzi, utangulizi, maandalizi, maongezi, masimulizi, matumizi; mapinduzi, kikohozi;

C/ msukumo, mwitikio, mgawanyiko, mgongano, hakikisho, jaribio, pambano, onyesho, uwezekano, uelewano, ushirikiano, makabiliano, masikilizano, mahusiano.

3. Назовите глаголы, от которых образованы следующие существительные и определите значения этих глаголов:
ngurumo, mdundo, uhusiano, fujo, ubaguzi, uchokozi, tatizo, mtego, ubishi.

4. Найдите русские эквиваленты словам на суахили. Вычлените корень слов левой колонки:

kijiji, ujaji, jioni, kijio,	ужин, рабыня, приезд, город,
njia, ujio, kijia, mjakazi,	большой город, вечер, дорога,
jiji, maji, mjaji, mji	пришелец, прибытие, деревня,
	тропинка, вода

kinywa, unywaji, kinyweo,	сосуд для питья, поить, лить,
mnywaji, kinywaji, -nyesha,	первый завтрак, способ питья,
-nywesha, kiamshakinywa	любитель выпить, напиток, рот
chakula, mlaji, mlo, ulaji,	еда, кормилец, правый,
-lisha, -a kulia, malisho,	потребление, кормить,
mlishaji	блюдо (*кушанье*), пастбище,
	потребитель (*едок*)
uzazi, zao, mzazi, uzao,	родитель, поколение, продукт,
kizazi, mzaliwa, -zaliana	рождение, уроженец,
	размножаться, производство

5. Предложите русские эквиваленты следующих словосочетаний:
nyumba ya uzazi; kizazi cha vijana; -fanya chaguo; -shiriki katika uchaguzi; mvumbuzi wa redio; mwundaji wa ndege; mapambano ya kivita; mgongano wa mawazo; mapatano ya muda mrefu; ofisi ya maulizo; mtetemeko wa ardhi; mwitikio wa haraka; malipo ya uzeeni; mahusiano kati ya mataifa; maabara ya majaribio; matengenezo ya kompyuta; -tega mtego; maoni tofauti; -onyesha mapendeleo; -andaa maonyesho; maandalizi ya mkutano; -fanya mapinduzi; kilio cha simu; kipimo kikubwa cha nguo.

6. Вспомните значения следующих сложных слов и проанализируйте, из каких компонентов они состоят:
mwanamke, mwanamume, mwanahewa, mwanakijiji, mwananchi, mwanafunzi, mfanya kazi, askari jeshi, askari polisi, gari moshi, mpitanjia, pundamilia, kifungua kinywa.

7. Приведите русские эквиваленты следующих существительных:
mwanamaji, mwanachuo, mwanachama, mwanahistoria, mwanajamii, mwanadiplomasia, mwanasheria, mwanaanga, mwanamapinduzi, mwanamuziki, bwana harusi, bibi harusi, bwanashamba, mfanya biashara, fundi umeme, mwenye benki, mwenyekiti.

Maneno mapya

kikosi (vi-) команда, бригада, отряд
zimamoto (-) 1)тушение пожара 2)пожарная команда
mzimamoto (wa-) пожарник
mwanadamu (w-) человек
madhara (мн.) вред, ущерб
makini (-) 1)внимательность, тщательность 2)внимательный
maskani, masikani (мн.) жилье, жилище
gharama (-) 1)трата, расходы 2)цена, стоимость
fukara (-; ma-) бедняк, нищий
kitambulisho (vi-) удостоверение, свидетельство, документ
mkataba (mi-) договор, соглашение; контракт
mkokoteni (mi-) тачка, тележка
kampuni (ma; -) компания, фирма
funzo (ma-) урок, наставление
sare (-) униформа
ndoo (-) ведро
shoka (ma-) топор
pampu (-) насос, помпа
nguzo (-) 1)опора 2)столб, колонна
kurunzi (-) большая лампа, фонарь; прожектор
oksijeni (-) кислород
iwapo [в том случае] если
ndoana (-) крюк, крючок (*рыболовный*)
-pumua дышать
-ungua гореть, пылать; сгорать, обгорать
-ajiri нанимать, брать на работу
-andikisha регистрировать
-tundika вешать, подвешивать; прикреплять
-maanisha значить, означать
-fikisha привозить, доставлять
-mudu 1)мочь 2)справляться 3)[о]владеть

Kikosi cha zimamoto

Moto ni kitu muhimu sana kwa maisha ya mwanadamu. Pamoja na hayo moto unaweza kuwa kitu cha hatari. Watu huogopa moto, kwani unaweza kutuletea madhara kama usipoangaliwa na kutotumiwa kwa makini. Nyumba nyingi za watu zinajengwa kwa miti na kuezekwa kwa majani, hasa katika sehemu za vijijini. Moto unapotokea katika mahali kama hapo, nyumba nyingi huungua na kuwaacha wanakijiji bila maskani.

Moto hutokea pia katika miji mikubwa. Hapo zamani wanamiji walitishiwa mno na moto, hata wakaamua kuajiri watu wa kuzima moto. Watu hao walilipwa mishahara yao na makampuni ya bima. Watu wenye maduka na wafanya biashara wote walilipa

fedha zao nyingi kwenye makampuni ya bima. Makampuni hayo yalilinda mali za wafanya biashara na kulipa fidia kwa wafanya biashara ambao mali zao ziliharibiwa na moto. Gharama za fidia hizo zilikuwa kubwa. Hivyo, makampuni ya bima yaliunda vikosi vya zima moto. Mishahara na gharama za kazi ya kuzima moto zililipwa na makampuni hayo. Lakini kikosi kilizima moto ulipotokea katika nyumba ya mtu aliyekuwa amejiandikisha na kampuni ya bima. Mwenye nyumba hiyo alitakiwa kuilipa kampuni kiasi fulani cha fedha kila mwaka. Ili kuwajulisha wazimamoto nyumba za watu wote waliokwisha kulipa kwenye makampuni ya bima, kila nyumba ilipatiwa kitambulisho chake. Kitambulisho hicho kilitundikwa mlangoni mwa nyumba hiyo. Moto ulipotokea, kikosi cha zimamoto kilitazama vitambulisho milangoni kwanza. Kama nyumba haikuwa na kitambulisho hicho, basi hiyo ilimaanisha kuwa mwenye nyumba huyo hakuwa na mkataba wo wote na kampuni ya bima. Maana yake ni kuwa nyumba hiyo haikushughulikiwa bali iliachwa iungue.

Vikosi hivyo vya zimamoto vya wakati huo vilitumia magari ya aina ya mikokoteni kuchukulia vifaa vyao vya kuzimia moto. Baadaye waliona kuwa magari hayo hayakuweza kuwafikisha haraka mahali penye tukio la moto. Walianza kutumia farasi kuvuta magari hayo. Vifaa vyao vilikuwa ndoo za ngozi na ndoana kubwa. Ndoana hizo walizitumia kuvuta mapaa ya hatari na kuta za hatari.

Watu wote hawakuweza kulipia gharama za vikosi vya zimamoto. Waliomudu kulipia gharama hizo walikuwa ni wafanya biashara na watu tajiri. Moto ulipotokea haukuchagua fukara au tajiri. Uliharibu mali zao wote. Hivyo, miji yote ilifikiria na kuona umuhimu wa vikosi vya zimamoto. Iliunda vikosi hivyo na vikaweza kuhudumia watu wote mjini bila kujali huyu ni tajiri au fukara. Wafanya kazi wa vikosi hivyo walilipwa mishahara yao na miji iliyohusika.

Askari zimamoto kabla hajaajiriwa hupata mafunzo maalum kuhusu uzimaji moto katika shule maalum. Muda mwingi wa mafunzo hayo unatumika katika kufanya mazoezi ya kujifunza kuzima moto katika hali mbalimbali. Vilevile hufanya mazoezi kuhusu utumiaji wa magari na injini za kuzima moto.

Kila askari zimamoto anapatiwa sare ya kazi pamoja na nguo maalum zinazovaliwa wakati wa kuzima moto. Kengele inapogonga askari zimamoto hukimbilia magari yao haraka. Magari hayo yanakuwa na sehemu maalum ya kuwekea maji, pampu, nguzo, kurunzi maalum, hewa ya oksijeni na vyombo vya kupumulia hewa hiyo. Vilevile wanakuwa na misumeno ambayo wakati mwingine hutumika kukatia vyuma au mbao kama ni lazima kufanya hivyo.

Maelezo

1. Magari yanakuwa na ... "в машинах имеется ..."; wanakuwa na ... "у них есть ...". Глагол -wa употребляется с показателем настоящего времени -na- в случаях, когда речь идет о постоянном или регулярном действии или состоянии. Например: Bibi anakuwa na wasaidizi anapoitunza bustani yake "У бабушки всегда есть помощники, когда она ухаживает за садом". (Сравните: Bibi ana wasaidizi ...). Anakuwa mkali sana anapoambiwa uongo "Он бывает очень суров, когда ему говорят неправду". (Сравните: Yeye huwa mkali ...).

Mazoezi

8. Найдите в тексте суахилийские эквиваленты следующих выражений:
вместе с тем; наносить ущерб; неосторожное обращение; крыть крышу соломой; оставить без крова; огонь представлял большую угрозу; охранять собственность торговцев; имущество пострадало при пожаре; компенсационные расходы; пожарные бригады; дом, поставленный на учет; страховая компания; владелец дома; ставить в известность; вывешивать свидетельство на двери; иметь договор с компанией; позволить дому сгореть; использовать специальные тележки; пожарный инвентарь; сбрасывать огнеопасную кровлю; огонь не выбирает бедного или богатого; получать зарплату в том или ином городе; получить специальную подготовку; тренировочные занятия по тушению огня; рабочая форма; водонепроницаемая обувь; жаростойкий головной убор; когда раздается сигнал; резервуар с водой; кислородный аппарат.

9. Дайте русские эквиваленты:
gari ya zima moto; kikosi cha polisi; kikosi cha usalama; -pata madhara; -leta madhara; -pima ukubwa wa madhara; mtu makini; -sikiliza kwa makini; -kagua kwa makini; -kosa maskani; -achwa bila maskani; -jitafutia maskani; maskani isiyofaa; kampuni ya kibiashara; kampuni ya kitaifa; kampuni ya kigeni; gharama za safari; -lipa gharama; -punguza gharama; -gharama za maisha; kitambulisho cha askari zimamoto; -onyesha kitambulisho; mkataba wa kazi; mkataba wa biashara; -fanya mkataba; -pata funzo; mafunzo ya kijeshi; mafunzo ya udereva; -ezeka nyumba; -ezeka banda la kuku; -ezeka zizi la ng'ombe; nguzo ya paa; nguzo ya simu; -weka nguzo imara; -ungua motoni; -ungua juani; -ajiri wajenzi; -ajiri vibarua; -andikisha gari; -jiandikisha kabla ya mkutano; -andikisha kampuni; -tundika picha ukutani; -tundika tangazo; -tundika kurunzi kandani; -mudu kazi ngumu; -mudu lugha ya kigeni; -mudu kuzivuka taabu zote; ndoo ya chuma; -beba ndoo; -teka maji kwa ndoo.

10. Замените подчеркнутое слово или выражение синонимом из текста:
masomo ya kutumia kompyuta; mapatano ya amani; shirika la ndege; -pata kazi; -wa na maana; -leta mzigo; taa kubwa; -pata cheti; bei ya petroli; nyumba kuukuu; mtu mwangalifu; -sababisha hasara; maendeleo ya binadamu; kundi la wajenzi.

11. Выпишите из текста существительные, образованные путем словосложения.

12. Ответьте на вопросы по содержанию текста:
1. Moto unaweza kuleta madhara gani kwa mwanadamu? 2. Wazimamoto wa kwanza walilipwa na nani mishahara yao? 3. Kwa nini watu maskini walikuwa wakiachwa bila ya maskani moto ulipotokea? 4. Mwenye nyumba alipaswa kufanya nini ili kuzuia nyumba yake isiungue? 5. Vifaa vya askari zimamoto wa zamani vilikuwaje? 6. Kwa nini hatimaye nyumba za watu wote zilianza kuhudumiwa na zimamoto? 7. Askari zimamoto inamlazimu kupata

mafunzo gani? 8. Nguo za askari hao zinakuwaje? 9. Vikosi vya leo vya zimamoto hutumia vifaa gani?

13. Перескажите коротко на суахили содержание текста.

14. Назовите на суахили профессии, соответствующие данному описанию:

1. Mtu huyu anatunga hadithi na vitabu au hushughulika na utoaji wa habari mbali mbali. 2. Huyu anapenda kuruka angani kama ndege na kuiangalia dunia na watu toka juu. 3. Kazi yake ni kuandaa karatasi na vyeti, kujibu simu, kuwahudumia wageni na kutumwa kazi ndogo. 4. Ni mtu ambaye kazi yake ya kawaida ni upandaji wa mbegu, upaliliaji wa shamba, uvunaji wa mazao. 5. Mtu huyu huajiriwa kwa ajili ya kuwasaidia watu kufika mahali fulani kwa haraka au kufikisha mizigo mahali panapotakiwa. 6. Kazi ya mtu huyu ni kuwasaidia watu wapate maskani bora na kuishi kwa raha.

15. Объясните на суахили значения следующих слов:

mwanamaji, fundi, meneja, mtumishi, mwuzaji, mwuguzi, askari polisi, dobi, mlinzi, mhandisi, kibarua.

16. Переведите:

1. Горожане и особенно жители сельской местности должны очень осторожно и внимательно обращаться с огнем. 2. Все расходы по предотвращению и тушению пожаров несут городские власти (*руководители*). 3. Не забудьте взять свое удостоверение, когда поедете регистрировать дом в нашей фирме. 4. Ты уже заключил договор со страховой компанией? 5. В этом году мы хотим сделать ремонт, покрыть крышу жестью и поставить новые опоры. 6. Нам придется нанимать строителей, так как самим не справиться с этой работой. 7. В результате сильного наводнения многие люди остались без крова, но весь ущерб еще не подсчитан. 8. Специальные отряды доставляют продовольственную помощь в районы, пострадавшие от этого бедствия.

17. Переведите следующий текст:

Maneno mapya

jogoo (ma-) петух
kimoyomoyo в сердце, в душе, про себя
yaani 1)а именно; то есть 2)так сказать
tundu (ma-) 1)дыра, отверстие 2)впадина, углубление
hila (-) 1)хитрость, уловка 2)коварство, обман
heri, kheri (-) 1)счастье; удача, успех 2)лучше, предпочтительнее
-wika петь (*о петухе*)
-chungulia наблюдать, выглядывать (*украдкой*), подглядывать
-konyeza подмигивать
-okota 1)подбирать 2)[случайно] находить
-angusha 1)ронять 2)бросать 3)сбивать, валить

Sarafu yenye thamani

Siku moja Kassim aliamka asubuhi na mapema, wakati jogoo alipokuwa akiwika. Kassim alikuwa amefurahi kwa sababu ilikuwa Jumamosi naye haendi shule siku hiyo. Yeye na kaka yake Yohana walipanga kwenda mtoni. Walisikia kwamba chura mkubwa sana anaishi chini ya daraja mtoni humo.

Walifika huko kabla jua halijakuwa kali. Walisimama darajani, wakaanza kuchungulia majini kumtafuta chura mkubwa. Wakati huo huo Suleiman na Hassan ambao nyumba yao iko karibu na mto huo, walifika mahali waliposimama Kassim na Yohana. Suleiman akauliza, "Mnatafuta nini? Kuna kitu mmeangusha mtoni?" Kassim akajibu, "La. Tunataka kumwona chura mkubwa sana aishiye chini ya daraja hili." Suleiman aliposikia maneno hayo alicheka kimoyomoyo, akamkonyeza Hassan, yaani kama kusema, "Angalia nitakavyofanya!"

Alikwenda na kusimama karibu na Kassim, akasema, "Ninamfahamu sana chura huyo. Ni mkubwa kama paka. Yeye hukaa humu majini katika tundu lile." Alionyesha mahali fulani kwa mkono wake, lakini Kassim na Yohana hawakuweza kuona tundu lo lote. Hassan hakujisumbua kwa sababu alijua kuwa Suleiman amesema uwongo kwa hila fulani.

Kassim alisema, "Sioni tundu wala chura mwenyewe." Suleiman akamwambia, "Inama kidogo, karibu uone." Kassim

aliinama, akachungulia chini, akasema tena, “Sioni tundu wala chura.” Suleiman akamwambia, “Inama zaidi.” Hapo Kassim aliinama sana, huku akitazama chini mtoni. Ghafula Suleiman alimsukuma, Kassim akaanguka majini.

Suleiman na Hassan walicheka sana. Walitazama chini wakamwona Kassim amesimama. Na ingawa alikuwa amelowa kabisa, hakuonyesha kukasirika hata kidogo, bali alikuwa akitazama kitu alichokishika mkononi. Baada ya muda mfupi aliangalia juu, akasema, “Nimeokota sarafu, yaonekana kuwa ya kizamani sana.” Kassim aliondoka mtoni, akarudi darajani, akawaonyesha wale wengine sarafu yake. Suleiman akauliza, “Kuna maneno yo yote juu yake?” Kassim akasema, “Ndiyo. Lakini maneno yenyewe ni ya lugha ya kigeni. Siwezi kuyafahamu.” Hassan akauliza, “Kuna tarehe yo yote?” Kassim akaangalia, akasema, “Ndiyo, ni mwaka wa 1780.” Hassan na Suleiman wakasema, “Ooo!” Kwa muda wa dakika chache wavulana hawa waliangalia sarafu hiyo. Halafu waliendelea tena kumtafuta chura mkubwa, lakini hawakumwona chura ye yote. Mwishowe Kassim alisema, “Yohana, heri turudi nyumbani sasa. Mama hajui tuko wapi.”

Suleiman akauliza, “Kassim, utafanya nini na sarafu uliyoigundua?” Kassim alifikiri kidogo, halafu akasema, “Nitaipeleka shule siku ya Jumatatu nimwulize mwalimu kama ina thamani yo yote.” Basi watoto hao waliagana wakarudi nyumbani kwao.

Siku ya Jumatatu Kassim alichukua sarafu yake akaenda shule akamwonyesha mwalimu wake. Mwalimu akaiangalia kwa makini, kisha akamwambia Kassim, “Mimi siwezi kuitambua sarafu hii, lakini nina rafiki yangu mmoja ambaye hupenda kuweka sarafu za zamani. Ukipenda nitampelekea sarafu hii yako ili atujulishe habari yake.” Kassim akakubali bila kusita.

Baada ya wiki moja mwalimu alimrudishia Kassim sarafu yake, akamwambia, “Rafiki yangu alifurahi kuona sarafu yako. Aliniambia kuwa sarafu za namna hiyo zilikuwa zikitumiwa sana katika pwani ya Afrika ya Mashariki na hata katika nchi za Waarabu miaka zaidi ya mia mbili iliyopita. Alisema watu huokota sarafu kama hii mara kwa mara pwani, lakini hakuelewa sababu ya sarafu yako kuwa mbali na pwani. Inawezekana kuwa msafiri fulani wa

zamani aliipoteza mtoni alipokuwa akivuka mto. Rafiki yangu alisema nikuambie ya kuwa ikiwa huna haja na sarafu hii, atainunua kwa bei nzuri.” Kassim alifurahi kwa kusikia habari ya thamani ya sarafu yake, akakubali kuiuza.

Maelezo

1. Глагол -weka “ставить” имеет дополнительные значения “хранить”, “складывать” и т.п.: -weka sarafu “собирать монеты”, -weka fedha “откладывать деньги”, -weka akiba “оставлять про запас”.

2. Alikubali bila kusita “Он согласился не раздумывая”. Глагол -sita “останавливаться” также имеет переносные значения “колебаться”, “медлить”, “не решаться”.

Mazoezi

18. Дайте русские эквиваленты:

-chungulia dirishani; -chungulia nje; -chungulia kwenye tundu la ufunguo; tundu la sindano; -toboa tundu; -fanya hila; mtu mwenye hila; -tumia hila; -okota sarafu; -okota kuni; -okota mfuko; mwokotaji; uokotaji; -enda mbele bila kusita; -jibu bila kusita; kutosita kumsaidia rafiki; -waza kimoyomoyo; -cheka kimoyomoyo; maisha ya heri; mtu wa heri; -takia mtu heri; heri kuwa na afya nzuri kuliko na mali nyingi; -konyeza kwa jicho; konyezo la siri; -konyezana; -angusha kalamu chini ya meza; -angusha matunda kwenye mti; -angusha mawe mtoni.

19. Переведите следующие вопросы и задайте их друг другу:

1. Почему Кассим проснулся рано в ту субботу несмотря на то, что ему не надо было идти в школу? 2. Как Сулейман решил подшутить над Кассимом и его братом? 3. Почему Кассим нисколько не рассердился на то, что Сулейман толкнул его в воду? 4. Какую монету юноша нашел в реке? 5. Ребятам удалось увидеть огромную лягушку, живущую под мостом? 6. Что сделал Кассим с найденной монетой? 7. Что рассказал ему учитель про эту находку? 8. Как эта монета могла попасть в

реку? 9. Почему юноша решил продать свою монету? 10. Какой характер был у Кассима? 11. Что вы думаете о характере Сулеймана?

20. Найдите в тексте из упражнения 17 предложения со аналитическими глагольными формами и проанализируйте их употребление.

21. Переведите:
1. Мальчики спали мертвым сном, даже не слышали, как кричали петухи. 2. Они поздно пришли на речку и напрасно вглядывались воду в надежде увидеть живущую там огромную лягушку. 3. Стоя на мосту, я уронил в реку часы, но решил, что лучше не утруждать себя и не лезть в холодную воду, а купить себе новые часы. 4. Заглянув в кабинет директора, секретарь увидел, что гости еще пьют чай. 5. Хасан сразу понял, что его брат решил обмануть приятеля, так как знал его коварный нрав. 6. Ныряя в воду, Кассим подобрал старинную монету и показал ее друзьям, но они не могли определить, имеет ли она какую-либо ценность. 7. Даже преподаватель не понял, что означают буквы, написанные на монете, и посоветовал показать ее специалисту, коллекционирующему старинные вещи. 8. Подобные монеты люди часто находят на берегу океана.

* * *

Mazoezi ya kujiandaa kusikiliza hadithi

Maneno mapya

-bishana спорить
-zoa подбирать; сгребать, сметать
-shikilia удерживать, поддерживать
-jipepea обмахиваться
kifungo (vi-) застежка (*пуговица, крючок и т.п.*)
zamu (-) очередь, очередность; смена
jasho (ma-) пот; испарина

23. Запомните следующие выражения:

-shika zamu	дежурить
-toka (-tokwa na) jasho	покрываться потом
jasho jembamba	холодный пот
kazi ya jasho	тяжелая работа

24. Дайте русские эквиваленты:
-fungua vifungo; -funga mfuko kwa ufunguo; amefunguliwa mlango; amefungiwa mlango; -bishana na rafiki; mabishano makali; ubishi mkubwa; -zoa majani barabarani; mzoaji wa takataka; -zoa karatasi; -shikilia kofia wakati wa upepo; -shikilia mzee kwenye njia ya utelezi; -shika zamu ya kila siku; zamu ya usiku; -pumzika kwa zamu; -acha kazi ya jasho; -toka jasho jingi; -jipepea kwa kupunguza joto; -jipepea kufukuza mbu; -jipepea kwa upepeo; -shinda; ushindi; mshindi; mashindano.

25. Дайте антонимы следующих выражений:
-ongeza nguvu; -ona joto; -vaa koti; -angusha kiti; -anza ubishi; -pata ushindi; -shikilia kamba.

26. Переведите:
1. Kila walipobishana walipiga kelele nyingi. 2. Juma alidai kwamba yeye anamzidi mwenzake kwa uwezo wa kuruka mbali. 3. Kwa bahati mbaya hawakuweza kumpata mtu wa kuwaamua. 4. Wasafiri walizidi kushikilia makasia kuzuia nguvu za poromoko la maji. 5. Tuliona ni heri kushuka chini kuliko kulala milimani wakati wa mvua kali. 6. Joto lilipozidi kila abiria akawa anatafuta kitu cha kujipepea. 7. Mama alimvua mwanawe koti lake kwa sababu jua liliwaka kwa nguvu sana. 8. Yule mzee aliendelea kuzoa takataka zote shambani mwake mpaka akatoka jasho jembamba. 9. Hatimaye nimepata kitu cha kuvaa niende kwenye harusi ya dadangu.

27. Преобразуйте предложения по образцу:
Ana nguvu kuliko wewe > Anakuzidi kwa nguvu
1. Ana pesa kuliko babako. 2. Vijana hawa wana uwezo kuliko sisi. 3. Sungura ana akili kuliko simba. 4. Mimi ni mrefu kuliko wewe.

5. Timu yetu ina nguvu kuliko yenu. 5. Gari lake ni jepesi kuliko langu. 6. Ana mbuzi wengi kuliko wafugaji wale.

28. Замените показатель -ki- показателем -napo-. Образец:
Tukis afir i tw aona mengi > Kila tunapos afir i tw aona mengi

1. Akija kwetu hutuletea zawadi chungu nzima. 2. Tukionana tunazidi kubishana. 3. Wakishiriki katika michezo hupata ushindi. 4. Jirani akiniona baada ya kazi hunialika kunywa bia. 5. Upepo ukivuma kwa nguvu, ninaumwa kichwa. 6. Babu akitusomea visa, anapata usingizi upesi.

29. Переведите:

1. Он одержал победу в тех соревнованиях, потому что сильнее тебя. 2. Перестаньте спорить, лучше подберите все бумажки в своей комнате, скоро придет преподаватель английского языка. 3. Застегни все пуговицы и надень шапку, на улице сильный мороз. 4. Морякам пришлось крепче держать паруса, чтобы их лодка не перевернулась из-за сильного ветра. 5. Сейчас мы посмотрим, кто из нас сильнее. Твоя очередь тянуть канат, а я буду удерживать с другого конца. 6. Дети, вы найдете, что поесть, пока я буду на дежурстве?

Kusikiliza hadithi

- Прослушайте текст полностью.
- Повторите в паузах фразы вслед за диктором.
- Закончите предложения вместо диктора.
- Задайте друг другу вопросы на суахили по содержанию прослушанного текста и дайте на них ответы.
- Ответьте на суахили на вопросы диктора.
- Изложите письменно на суахили содержание текста.

* * *

Mazoezi

30. Переведите диалог:

-agiza заказывать; давать указания
agizo (ma-) заказ; распоряжение
orodha (-) список; перечень
bili(-) счет; чек
menyu (-) меню

Hotelini

Mwenye hoteli: Karibu bwana. Habari za safari?
Mgeni: Njema. Hujambo?
Mwenye hoteli: Sijambo. Nikusaidie nini?
Mgeni: Nataka chumba cha mtu mmoja. Vyumba wazi vipo? Ningependa chumba kinachoelekea baharini.
Mwenye hoteli: Ulituma maagizo tukushikie chumba?
Mgeni: Hapana, nilisikia kuwa kipindi hiki hakuna shida ya vyumba.
Mwenye hoteli: Kweli, lakini wakati huu kuna mkutano na vyumba karibu vyote vimechukuliwa na wageni wenye kushiriki katika mkutano huo.
Mgeni: Kumbe! Sasa nifanyeje? Nisaidie.
Mwenye hoteli: Ngoja nitazame katika orodha. Bahati yako! Kuna chumba cha watu wawili.
Mgeni: Nikichukua hicho nitalipa bili ya watu wawili?
Mwenye hoteli: Hapana. Jina lako nani?
Mgeni: Hebu, ngoja kwanza. Usiku mmoja pamoja na kifungua kinywa, ni shilingi ngapi?
Mwenye hoteli: Shilingi elfu sitini.
Mgeni: Ghali sana, lakini sina chaguo jingine. Jina langu Hassan Adam.
Mwenye hoteli: Utakaa hapa siku ngapi?
Mgeni: Natarajia kukaa mwezi mmoja. Je, nikila hapa mchana na usiku, itakuwaje?
Mwenye hoteli: Utadaiwa kama watu wengine wajao kula hapa. Bei za vyakula zimeandikwa kwenye menyu.
Mgeni: Je, naweza kuagiza vyakula niletewe chumbani mwangu?
Mwenye hoteli: Hakika. Orodha ya simu za hotelini na ya vyakula utaikuta katika chumba chako.
Mgeni: Asante sana.
Mwenye hoteli: Sasa mfuate huyu bwana, atakuonyesha chumba chako. Iache mizigo yako hapa, na utaletewa sasa hivi.

31. Найдите в диалоге из упражнения 30 суахилийские эквиваленты следующих выражений:
чем могу помочь?; одноместный номер; свободные номера; номер с видом на море; оформлять заказ; резервировать номер для кого-либо; ах вот как!; заглянуть в список; ваше счастье!; платить за двоих; у меня нет иного выхода; с вас возьмут, как и с других посетителей; заказать еду в номер.

32. Выучите наизусть диалог из упражнения 30.

33. Переведите следующий рассказ и перескажите его на суахили:

В незнакомом городе

Один человек приехал в незнакомый город. Он взял такси и поехал в гостиницу. Там он снял номер, оставил вещи и пошел осматривать город. По дороге он зашел на почту и дал жене телеграмму, где сообщил ей адрес и телефон гостиницы.

В этот день он много ходил по улицам, был в музеях, заходил в магазины, а вечером пошел в кино. Когда сеанс закончился, он решил ехать в гостиницу, но забыл ее адрес. Тогда он пошел на почту и послал жене еще одну телеграмму: "Немедленно сообщи мне адрес моей гостиницы".

34. Переведите:
1. У вас есть свободные номера? Я не успел оформить заказ. 2. Какой номер вам нужен, на одного или на двоих? 3. Мы зарезервировали для вас номер на втором этаже. 4. Какие удобства есть в вашей гостинице? 5. Я прошу постирать и погладить мои вещи. 6. Разбудите меня в половине седьмого и принесите завтрак в номер. 7. Когда будете уходить, оставляйте ключ у администратора (meneja), чтобы горничная смогла убрать ваш номер. 8. Где можно ознакомиться с меню вашего ресторана? 9. Вот ваш счет. 10. Как можно заплатить, наличными или чеком? 11. Лучше я заплачу чеком. 12. Вызовите мне такси, пожалуйста.

SOMO LA KUMI NA MBILI
Лексическая тема "Своими руками"

Грамматика

Сложно-подчиненное предложение в суахили можно образовать двумя способами: с помощью союзов или союзных слов, а также с помощью бессоюзной связи.

Придаточные ***определительные*** предложения вводятся при помощи релятивного союза amba-, согласованного с тем членом главного предложения, который определяется придаточным предложением:

Abiria wote ambao walipanda basi walielekea mji wa Kampala "Все пассажиры, которые сели в автобус, направлялись в Кампалу".

Бессоюзная связь выражается соответствующим релятивным показателем:

Abiria wote wali*o*panda basi walielekea mji wa Kampala.

Союзы kwamba, kuwa, ya kuwa вводят придаточные ***дополнительные*** предложения:

Sikufikiri kwamba atachelewa "Я не думал, что он опоздает".

Бессоюзная связь в этом случае выражается только способом примыкания: Sikufikiri atachelewa.

Придаточные предложения ***причины*** вводятся при помощи союзов kwa sababu, kwa kuwa, kwa vile, kwani, maana:

Amechelewa masomoni maana alikosa basi "Он опоздал на занятия, потому что не упел на автобус".

Watoto walirudi nyumbani kwa kuwa walitishwa na simba "Дети вернулись домой, так как их испугал лев".

После союза ***цели*** kwa ajili ya "ради того, чтобы" употребляется инфинитив:

Baba alinunua bunduki mpya kwa ajili ya kuwawinda wanyama wa porini "Отец купил новое ружье, чтобы охотиться на диких животных".

Союз цели ili требует употребления инфинитивной формы или же желательно-побудительного наклонения:

Watoto wanapaswa kusoma vizuri ili kuiletea usitawi (ili wailetee usitawi) nchi yao "Дети должны учиться хорошо, чтобы добиться процветания своей страны".

Инфинитивная форма глагола или желательно-побудительное наклонение могут передавать значение цели:

Baba alinunua bunduki mpya ***ku***wawinda = ***a***wawind***e*** wanyama wa porini.

Придаточные предложения ***следствия*** присоединяются к главному предложению с помощью союза kwa hivyo:

Sikusoma kitabu hiki kwa hivyo sikuweza kujibu maswali ya mwalimu "Я не прочитал эту книгу, поэтому не смог ответить на вопросы преподавателя".

Придаточные ***уступительные*** предложения вводятся с помощью союза ingawa:

Aliendelea na kazi ingawa amechoka sana "Он продолжал работать, хотя (несмотря на то, что) очень устал".

Условные придаточные предложения присоединяются к главному при помощи союзов kama, ikiwa, iwapo:

Ikiwa mwenzangu atakuja mapema tutawahi sinema "Если мой друг придет пораньше, мы успеем в кино".

Бессоюзная связь выражается с помощью показателя условного наклонения *-ki-*: Mwenzangu akija mapema tutawahi sinema.

Придаточные ***временные*** предложения вводит союз ambapo. Если такое придаточное предложение предшествует главному, то употребляется сложный союз wakati ambapo:

Wakati ambapo nilisoma taasisini, nilipenda kujifunza Kifaransa "Когда я учился в институте, мне нравилось изучать французский язык".

Релятивные показатели *-napo-*, *-lipo-*, *-takapo-* образуют бессоюзные временные придаточные предложения: Nilipo soma taasisini nilipenda kujifunza Kifaransa.

Mazoezi

1. Соедините предложения, выбрав союзное слово в соответствии с мотивацией, изложенной в скобках. Внесите

изменения там, где это необходимо: amba-, ambapo, kama, ikiwa, iwapo, ili, kwa ajili ya, kwani, ingawa, kwa hivyo, kwa sababu, maana, kwa vile, kwa kuwa, kwamba:

1. Zuhura humsaidia babake kulima na kupalilia shamba lao. Kazi hiyo inahitaji juhudi na bidii nyingi (*причина*). 2. Kusuka mikeka kunampendeza sana msichana huyu. Yeye ni hodari mno kwa kushughulika na kazi ya mikono (*определение*). 3. Nilifaulu kuondoka kwenye maji. Kingo za mto zilikuwa wima kabisa (*уступительность*). 4. Mtoto alikuwa akilia kwa sauti kubwa. Hakuweza kunijibu lo lote wala kutaja jina lake (*следствие*). 5. Bwana Musa alipewa kompyuta hii kama zawadi. Alisafiri Ulaya kwa shughuli za kazi (*время*). 6. Mnataka kuliona poromoko la maji kwa macho yenu wenyewe. Mnapaswa kujiandaa mapema kwa safari hiyo (*условие*). 7. Ufugaji wa kondoo hausitawi katika nchi hii. Mimea ya porini yenye miiba mingi inawaudhi kondoo na manyoya yao marefu (*причина*). 8. Mkubwa wetu huwakaripia watumishi mara kwa mara. Hawana budi kufanya kazi kwa makini zaidi (*цель*). 9. Nchi yetu itakosa mabingwa wa kutosha. Elimu haitaangaliwa vizuri (*условие*). 10. Maziwa yote yenye kuuzwa na wakulima hutiwa ndani ya mapipa ya chuma. Mapipa hayo yanazuia maziwa yasiharibike upesi (*причина*). 11. Inafaa uvimeze haraka vidonge hivi. Umeletewa vidonge hivyo na mganga kutoka mjini (*определение*). 11. Meneja hakuahidi cho chote. Atatupatia chumba hotelini mwake (*дополнение*).

2. Соедините предложения с помощью бессоюзной связи, внеся соответствующие изменения в придаточные предложения там, где это необходимо. Переведите их:

1. Jamaa zangu hufuga kuku, mbuzi na kondoo. Wanyama hawa huwapatia pesa na chakula (*определение*). 2. Wanakijiji hupeleka mayai na maziwa yao sokoni. Mazao hayo yanapatikana kwa kiasi cha kuzidi mahitaji yao (*условие*). 3. Fundi aliparamia paani. Anataka kubadilisha mabati kadhaa mabovu (*цель*). 4. Wachungaji huchukua bunduki pamoja nao. Wanapeleka malishoni ng'ombe wao (*время*). 5. Inakubidi kuiacha ile tabia ya kuvuta sigara. Hutaki kuidhuru afya yako (*условие*). 6. Mwaka uliopita nilitembelea Misri. Ilinivutia sana kwa makaburi na mahekalu yake ya kale

(*определение*). 7. Tuliwasha vibiriti. Tutaweza kuona gizani nyuso za wageni wale (*цель*).

3. Замените союзную связь в предложениях бессоюзной и наоборот:

A/ 1. Kama unapenda matunda mabichi kidogo nitakuangushia maembe yale ya juu. 2. Wakati ambapo Salum alitembea mtaani Kariakoo alimwokota mbwa ambaye alikuwa na madoadoa mengi mwilini mwake. 3. Watalii walimwomba dereva kusimamisha basi kwa ajili ya kuwapiga picha wanyama wa porini. 4. Ndege hazitaruhusiwa kutua chini iwapo ukungu utakuwa mnene. 5. Alisimamisha motokaa yake ambapo alisikia kishindo kikubwa na kufahamu kuwa ukanda wa injini umekatika. 6. Nilikiondoa kifuniko cha tanki ili kuona kama mna mafuta ya kutosha ndani yake. 7. Ikiwa wakuu wa nchi hawatatia maanani maendeleo ya ukulima nchi yetu itabaki kuwa maskini.

B/ 1. Itakubidi kuivunja safari ya Mikumi ukiona injini ya motokaa yako haishiki moto vizuri. 2. Habari nilizosikia redioni zilieleza juu ya watu waliopoteza maisha yao katika gharika hilo. 3. Usipojua kuogelea vizuri, heri usipige mbizi kutoka darajani hapa. 4. Tusipomaliza mitihani yetu mwezi huu hatutapata nafasi ya kushiriki katika mashindano ya mbio yatakayofanyika mnamo Julai. 5. Siku ile vijana wa kundi letu waliamshwa asubuhi na mapema wapate kukikwea kilele cha Kilimanjaro kabla ya jua kuwa kali. 6. Abiria wote wa ndege walijifungia kanda zao za usalama taa za rangi nyekundu zilipowaka. 7. Mwuguzi alimpa mgonjwa maji ya matunda apate nguvu kidogo.

4. Переведите с помощью бессоюзной связи:

1. Фатума выбежала на улицу, когда услышала громкие крики за домом. 2. Мы продолжали путь даже ночью, чтобы вовремя доехать до города. 3. Если тебе холодно, возьми то толстое одеяло, которое мы недавно купили на рынке. 4. Когда туристы спустились в пещеру, они обнаружили на ее сводах непонятные знаки и рисунки. 5. Дети спрятались в высокой траве, чтобы их не нашли родители. 6. Если ты не доверяешь этому банку, забери оттуда свои деньги и положи в другой. 7. Каждый

человек волен выбирать себе работу, которая ему больше нравится. 8. Если бы торговое соглашение было заключено раньше, нам удалось бы значительно снизить транспортные расходы.

5. Переведите, используя союзную связь:

1. Древние китайские книги, которые вы видите в этом музее, были привезены одним путешественником в начале прошлого века. 2. Хотя Александр купил самый дорогой мобильный телефон, он не любит хвастаться, как другие ребята. 3. Если ты не веришь мне, спроси у моего брата, который только что вернулся со стадиона, и сам наблюдал за этой игрой. 4. Поскольку в этой деревне до сих пор нет электричества, местным жителям приходится запасаться дровами в большом количестве. 5. Мы поняли, что вот-вот начнется проливной дождь, когда увидели черные тучи, закрывшие все небо над нашими головами. 6. Несмотря на то, что Рашид был хорошим спортсменом, он начал тонуть, так как вода в море была очень холодной. 7. Для того, чтобы попасть на тот берег, вам лучше воспользоваться паромной переправой. 8. Местные реки всегда выходят из берегов в это время, потому что снега в горах начинают быстро таять. 9. Первые морские суда, которые использовали люди в древние времена, изготавливались из стволов деревьев, поэтому были очень тяжелые. 10. В нашем парке все старые и хилые деревья были выкорчеваны с тем, чтобы на их место посадить новые деревья и украсить парк всевозможными цветами.

Maneno mapya

hai живой
uhai (ед.) 1)жизнь 2)существование
kiumbe (vi-) создание, творение; существо
mmomonyoko (mi-) 1)эрозия 2)оползень
-hama переселяться, переезжать
-hamahama переезжать с места на место, кочевать, мигрировать
rutuba (-) плодородие, плодородность

korongo (ma-) 1)овраг 2)канава, кювет
kadiri, kadri (-) величина; степень, мера
samadi (-) навоз
kunde (-) бобы
vumbi (ma-) пыль; *зд.* слой (*почвы*)
wajibu (ед.) долг, обязанность
lengo (ma-) цель, задача
mfereji (mi-) канал; траншея
bwawa (ma-) запруда, плотина
-zalisha 1)производить, создавать 2)выращивать
-oza портиться, гнить
-rutubisha удобрять
-tokana na происходить, брать начало
kutokana na из-за; исходя из, в соответствии с
-puliza 1)дуть (*с силой*) 2)надувать, накачивать
-chimba копать, рыть; выкапывать
-elekeza 1)показывать, указывать 2)направлять, наставлять
-kinga ставить преграду; предохранять, оберегать

Udongo ni uhai

Binadamu anategemea sana udongo. Maisha yake yapo kwa sababu udongo upo. Mimea mbalimbali huota shukrani kwa udongo. Baadhi ya mimea hiyo hutumiwa na binadamu kwa chakula chake. Hata wanyama wote wanategemea udongo. Majani wanayokula yanaota katika udongo. Kama udongo usipozalisha mimea tunayoiona, basi maisha ya viumbe wenye uhai yatakuwa hatarini.

Udongo unaweza kuharibiwa na watu, wanyama na upepo. Mtu anapolima vibaya anaweza kuleta mmomonyoko wa udongo. Mvua itakaponyesha, udongo utachukuliwa na maji na kuacha korongo mahali ulipokuwa kwanza.

Zamani watu wengi walipenda kuhamahama. Walijenga maskani na kuishi mahali kwa muda mfupi, halafu wakahamia pengine. Nafasi ya kuishi watu ilikuwa kubwa, kwa sababu watu walikuwa wachache. Sasa watu wameongezeka na kuwa wengi. Uwezekano wa kuishi kwa kuhamahama hapo tena. Watu wanaishi mahali pamoja kwa muda mrefu bila kuhama. Unapoishi mahali hapo, unalima mazao ya chakula chako mahali pale pale kila mwaka. Kuishi kwa wananchi katika vijiji kumewafanya waishi mahali pamoja bila kuhamahama.

Kwa vile tunaishi na kulima mashamba yetu kila mwaka, udongo wa mashamba hayo unachoka. Hauzalishi mazao kwa wingi kadiri miaka inavyopita. Unahitaji kurutubishwa tena ili mimea iweze kusitawi vizuri. Rutuba inayotakiwa ni mbolea, hasa mbolea ya samadi. Mbolea inayotokana na wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo inapotiwa shambani inaongeza rutuba nyingi udongoni.

Njia nyingine ya kuhifadhi udongo ni kubadili mazao tunayopanda. Mimea ya jamii ya kunde ni safi sana kwa kurutubisha udongo. Hii inamaanisha kuwa unapopanda mazao fulani kwa msimu fulani, huna budi kupanda mazao ya aina nyingine tofauti msimu mwingine.

Mara baada ya kuvuna mazao shambani, inafaa kutunza hali ya udongo. Mabaki ya mimea kama viazi, maharage na mboga yanapobakia shambani na kuozea humo husaidia sana kurutubisha udongo. Mara nyingi wakulima wanapotayarisha mashamba, wanakusanya mabaki ya mazao yaliyopita na kuyachoma. Hiyo si njia nzuri kwa sababu mabaki hayo yanapochomwa huacha shamba hilo wazi. Upepo unapovuma hupuliza vumbi la juu ambalo lina rutuba na kulitoa shambani. Vile vile jua linapowaka huchoma udongo na kusababisiha kudhoofu kwake.

Kuhifadhi udongo ni wajibu wa kila mtu. Inapaswa kuzuia makorongo yanayoanza yasizidi. Makorongo hayo yazibwe kwa mawe na matawi ya miti kisha vipandwe vichaka na nyasi kwa lengo la kuufanya udongo usichukuliwe na maji. Baada ya hapo maji yaelekezwe mahali yasikoweza kuharibu udongo.

Iwapo mahali unapovuna ni mteremko, punguza nguvu ya maji kwa kuchimba mifereji ili kulikinga shamba. Vile vile unaweza kutengeneza mabwawa mwanzo wa maji hayo. Mabwawa hayo yanaweza kufaa kwa wakati wa kiangazi.

Maelezo

1. Глагол -hama "переезжать" при указании направления движения обязательно употребляется в направительной форме: -hamia "переезжать, переселяться (*куда-л.*". При этом предлог может отсутствовать: Nimehamia mji mwingine "Я переехал в другой город"; Wanataka kuhamia orofa ya tano "Они собираются переселиться на пятый этаж".

2. Kuishi kwa wananchi katika vijiji kumewafanya waishi mahali pamoja "Проживание людей в деревнях привело их к оседлому образу жизни". ... kwa lengo la kuufanya udongo usichukuliwe na maji "... с целью предотвратить смывание почвы водой". Глагол -fanya "делать" плюс объектный показатель или дополнение перед последующим глаголом передает значение "заставлять, вынуждать (*что-л.*) делать". Такой оборот может иметь различные варианты перевода на русский язык, как видим на примерах из текста. Глагол, следующий за глаголом -fanya, стоит либо в желательно-побудительном наклонении, либо в инфинитивной форме. Другие примеры: Mvua kali ilitufanya turudi nyuma "Из-за сильного дождя мы вернулись назад" Ajali ya magari iliwafanya watu kadhaa kupoteza maisha yao "В результате дорожной аварии погибло несколько человек".

3. Hauzalishi mazao kwa wingi kadiri miaka inavyopita "С течением времени она (*земля*) перестает давать большие урожаи". Слово kadiri "степень" часто употребляется в сочетании с глаголом, имеющим релятив образа действия -vyo-: kadiri inavyotakiwa "в той мере, в какой это необходимо"; kadiri nijuavyo "насколько мне известно"; kadiri tulivyozidi kupanda juu "по мере того как мы поднимались все выше и выше".

Mazoezi

6. Найдите в тексте суахилийские эквиваленты следующих выражений:
окружающие нас растения; живые существа; быть в опасности; вызывать эрозию почвы; почва вымывается; вместо нее появляется овраг; переселяться на новое место; вести кочевой образ жизни; выращивать продовольственные культуры на одном и том же месте; иметь постоянное место проживания; ежегодное возделывание полей; земля требует восстановления плодородия; органические удобрения; повышать плодородие почвы; растения семейства бобовых; заботиться о состоянии почвы; растительные отходы; прошлый урожай; оголять поле; сдувать верхний слой почвы; истощение почвы; долг каждого;

заполнять овраги камнями и ветками; ослабить потоки воды; копать траншеи; ограждать поля; строить запруду.

7. Дайте русские эквиваленты:
mtu hai; kiumbe chenye uhai; uhai wa mtu; -leta mmomonyoko wa udongo; mmomonyoko wa hatari; -zuia mmomonyoko; kwa kadiri fulani; kadiri ya watu ishirini; kadiri ninavyojua; kadiri unavyofahamu; -anguka korongoni; miteremko ya korongo; mbolea ya samadi; utumiaji wa mbolea; -ondoa mavumbi; -geuka vumbi; njia zilizojaa mavumbi; vumbi tupu; -tekeleza wajibu; -wa na wajibu; -lengo la serikali; -tekeleza lengo; -jiwekea malengo makubwa; -chimba mfereji; -chimba shimo; uchimbaji wa kisima; -chimba viazi; -tengeneza bwawa; maji yenye kukusanyika bwawani; -zalisha mazao ya chakula; -zalisha mali; uzalishaji wa mboga; maisha ya kuhamahama; -hamia pengine; mhamiaji; -rutubisha ardhi; urutubishaji wa udongo; -ongeza rutuba ya udongo; balaa inayotokana na mteremeko wa ardhi; kutokana na sababu fulani; kutokana na mpango wetu; mabaki ya mimea iliyooza; kuoza kwa matunda; -puliza mpira; upepo unaopuliza kwa nguvu; -kinga mashamba; -kinga afya; -jikinga na ugonjwa wa kuambukiza; -elekeza njia; -elekeza mgeni mahali anapotaka; maelekezo muhimu.

8. Закончите предложения (по содержанию текста):
1. Udongo ni kitu cha mana sana kwa sababu ... 2. Maisha ya viumbe wote wenye uhai yatakuwa hatarini kama ... 3. Sababu zinazoweza kuufanya udongo uharibike ni ... 4. Kuhamahama maana yake ni ... 5. Udongo shambani mwa mkulima unachoka kwa sababu ... 6. Mkulima akitaka kuongeza rutuba ya udongo anapaswa ... 7. Njia nyingine ya kuhifadhi udongo ni ... 8. Inafaa kuacha mabaki ya mimea mashambani baada ya kuvuna mazao kwa ajili ya ... 9. Ni hatari kuliacha shamba wazi kwa sababu ... 10. Njia bora ya kuzuia udongo usichukuliwe na maji ni ... 11. Iwapo shamba la mkulima liko kwenye mteremko, inambidi mkulima ...

9. Перескажите коротко на суахили содержание текста.

10. Переведите:
1. Mwenye duka aliwafanya wateja wake walipe kwa fedha taslimu tu. 2. Mshahara mdogo ulinifanya niache kazi ya kiwandani nihamie jijini kujitafutia kazi nyingine. 3. Ulimaji wa ardhi kwa njia mbovu unaifanya ardhi hii kukosa rutuba yake. 4. Jua lenye kuwaka kwa ukali linaufanya udongo kudhoofu. 5. Kutoifahamu njia vizuri kulimfanya dereva kurudi nyuma na kulala hotelini. 6. Nguvu za maji ya mvua zinayafanya makorongo yapanuke zaidi. 7. Ni wajibu mkubwa wa wazazi kuwafanya watoto wao wapate elimu na ujuzi mwingi kwa kadiri inavyowezekana. 8. Kupanda kwa vichaka na nyasi kwenye miteremko kunayafanya maji yasielekee mahali yanakoweza kuharibu udongo.

11. Переведите предложения, используя конструкцию желательно-побудительного наклонения с глаголом -fanya:
1. Болезнь отца заставила меня поменять свои планы и переехать к нему. 2. Сильный ветер повалил все деревья вдоль нашей улицы. 3. Из-за обильных дождей в сезон "масика" почвы на склонах сильно вымываются. 4. Поломка автобуса вынудила пассажиров идти пешком до ближайшей станции. 5. Из-за множества рытвин на дороге мы вынуждены были ехать объездным путем. 6. Бабуины, не прекращавшие воровать кукурузу с полей, вынудили местных жителей обратиться за помощью к охотникам.

12. Переведите, выбрав из скобок соответствующий глагол:
1. Наши близкие друзья переехали в другой район города. Нам тоже придется переезжать, так как эта квартира (fleti) мала для нашей семьи (-hama, -hamia). 2. Куда ты идешь? Мастер придет с минуты на минуту (-ja, -enda). 3. Книги в библиотеке будут давать только после обеда. Дай мне пожалуйста твой словарь до завтра (-pa, -toa). 4. Мальчишки убежали с занятий. Они все побежали на аэродром посмотреть на новую модель самолета (-kimbia, -kimbilia). 5. Унеси это ведро с мусором и принеси чайник с кухни (-chukua, -leta). Ты слышал, что сказал отец? – Да, он сказал мне, что сначала я должен выучить наизусть

диалог, а потом могу погулять (-sema, -ambia). 7. Положите эти бумаги на стол. Не могу найти ключи от сейфа (sefu), хотя я хорошо помню, что положил их в карман (-tia, -weka).

13. Запомните пословицу и объясните на суахили ее смысл: **Akiba haiozi**

14. Переведите:
1. Все живые существа, и люди, и животные нуждаются в растениях, которые являются источником пищи. 2. Само существование человека будет в опасности, если он не будет заботиться о плодородии почвы, чистоте воздуха и воды. 3. В поисках новых пастбищ для своих животных некоторые племена постоянно кочуют. 4. Жители деревни поставили задачу вырыть канал и сделать запруду для того, чтобы у них всегда была резервная вода. 5. Сходи на рынок и купи фруктов и овощей, только не забудь положить их в холодильник, чтобы они не испортились. 6. Вот ваш гид, в его обязанности входит направлять туристов в самые интересные уголки нашего заповедника. 7. Насколько я знаю, эта дорога самая короткая, несмотря на то, что она узкая и пыльная. 8. По мере того как они поднимались все выше и выше, растительность на склонах становилась скудной.

16. Переведите следующий текст:

Maneno mapya

sanaa (-) 1)искусство, вид искусства 2)ремесло, мастерство
stadi (ma-) мастер своего дела, умелец
stadi искусный, умелый
ustadi (ед.) искусство, мастерство
mashine (-) машина, механизм; агрегат
fahari (-) гордость
seremala (ma-) 1)плотник 2)столяр
mwanasesere (w-) кукла
sanamu (-) скульптура; статуя; памятник
panga (ma-) длинный широкий нож; меч
samani (-) мебель, предметы обстановки
mfinyanzi (wa-) гончар
-finyanga лепить из глины
-unga соединять, присоединять

kadha wa kadha некоторые, кое-какие
laini 1) гладкий, ровный 2) мягкий
-jiunga na 1) присоединяться 2) поступать, вступать (*в организацию*)

Shule za sanaa

Shule za sanaa ni shule maalum ambazo lengo lake ni kuwafundisha vijana kazi za ufundi wa kila namna unaohitaji ustadi wa mikono na akili ya mtu. Vijana huweza kujiunga na shule kama hizo baada ya kumaliza shule ya kawaida. Katika shule za sanaa masomo mbali mbali hutolewa ambayo kwa jumla yangewapendeza wavulana na wasichana. Kwa mfano wasichana wangefurahia ufundi wa kushona nguo, kupiga chapa ofisini, upishi na kuwa watumishi wafanyao kazi mikahawani na nyumbani. Wavulana nao wangependelea kazi za ufundi wa mashine za kila namna, ujenzi, uendeshaji wa magari, useremala, upakaji wa rangi na kadhalika. Kazi za ukarani na za biashara labda zingependwa na wote.

Vijana wenye kuhitimu mafunzo kama hayo, wataajiriwa kufanya kazi katika viwanda kadha wa kadha na labda wengine wataajiriwa katika vituo mbali mbali vinavyoendeshwa na serikali au matajiri wa nchi. Baadhi ya vijana wakiwa na bahati wangeweza kuanzisha na kuendesha kazi zao wenyewe.

Watoto huanza kufundishwa kazi mbali mbali za mikono hata kwenye shule za msingi. Wakati wa somo la kazi za mikono watoto hugawanyika katika makundi tofauti kutokana na mapendeleo yao. Kila mwanafunzi anakuwa na vifaa vya kutengeneza vitu. Kwa mfano wanafunzi wa kundi la kwanza wanasuka na kushona mikeka, vikapu, vitu na mapambo mengine mbali mbali. Wanafunzi wa kundi jingine hufinyanga vyungu vya kupikia, vya maua na vikombe vya chai. Udongo wa mfinyanzi wanaoutumia hupondwa na kuchanganywa na maji ili kuwa laini. Vyungu vilivyofinyangwa hukaushwa kivulini kisha huchomwa kwenye moto mkubwa ili viwe imara.

Kundi la tatu ni la uchongaji. Wanafunzi wa kundi hili wanatumia mbao kutengeneza wanasesere, magari ya kuchezea watoto pamoja na sanamu za wanyama mbali mbali. Vifaa vyao ni visu, mapanga na mashoka madogo.

Pia kuna kundi la uchoraji. Vijana wa kundi hili hufanya maajabu! Wao wanatumia penseli, karatasi, rangi za maji na za mafuta kuchora picha mbali mbali, yaani picha za watu, wanyama, ndege, maua na vitu vingine kama nyumba, vyombo na samani.

Vitu vingine vinavyotengenezwa na wanafunzi katika somo la kazi za mikono vinapendeza sana hata wazazi na watu wengine wanaoishi karibu na shule huja kuvinunua. Wazazi huwaonea fahari watoto wao na kujaa furaha kubwa kuona jinsi wanavyoandaliwa kwa maisha yao ya baadaye.

Maelezo

1. ... katika vituo vinavyoendeshwa na serikali au matajiri wa nchi "в государственных учреждениях или частных структурах". Слово kituo "пункт', "остановка" также имеет значение "учреждение", "ведомство": kituo cha watoto "детское учреждение"; kituo cha kijamii "социальное ведомство".

2. Слово jinsi "способ", "манера" часто употребляется в сочетании с глаголом, имеющим релятив -vyo-: jinsi wanavyoimba nyimbo zao "их манера исполнения песен"; jinsi ninavyotafsiri "мой стиль перевода".

Mazoezi

16. Дайте русские эквиваленты:

shule ya sanaa; vitu vya sanaa; -jifunza sanaa mbali mbali; sanaa ya uchoraji; kundi la wanasanaa; -fanya kazi kwa ustadi; ustadi wa mikono; seremala stadi; useremala; mashine ya kutoboa; mashine za kompyuta; fundi wa kutengeneza mashine; kwa jumla; wanasesere kadha wa kadha; udongo laini; kitambaa laini; mbao laini; -kata nyasi kwa panga; -pigana kwa panga; -chonga sanamu; sanamu za wanyama; -simamisha sanamu; -unga kamba mahali ilipokatika; -ungana pamoja; -jiunga na klabu ya wanamichezo; -finyanga vikombe; -finyanga vyungu vya maua; mfinyanzi; ufinyanzi; -ponda udongo; -nunua samani mpya; -ondoa vumbi kwenye samani; -badilisha samani; -ona fahari; kuionea fahari nchi yako; jinsi wanavyochonga; jinsi tunavyochora.

17. Дайте эквиваленты на суахили:
мастерство плотника; умелые руки; мастер по производству мебели; различные виды искусства; развитие искусства; киноискусство; гончарное искусство; гончар; некоторые скульптуры; устанавливать монумент; памятник Пушкину; испытывать гордость; гордиться сыном; соединить два конца веревки; объединяться; вступить в клуб; поступить в школу искусств; мягкая глина; ровное шоссе; кое-какие детские игрушки; ваза для цветов; малярные работы; швейное дело; урок труда; творить чудеса; акварельные краски; масляные краски; детская манера рисования; огромный агрегат; электромеханизмы; детские учреждения; государственное ведомство.

18. Замените синонимами подчеркнутые слова или словосочетания:
1. Yeye ni fundi hodari wa kutengeneza visu virefu. 2. Binti yangu alijiunga na klabu ya wapandaji farasi. 3. Blanketi hili ni jororo sana, nadhani litampendeza bibi yetu. 4. Zana nyingi kiwandani humu ni kuukuu sana, sharti zibadilishwe upesi iwezekanavyo. 5. Ujuzi wa bingwa huyu ungefaa kuonewa fahari. 6. Seremala ameagiziwa kutengeneza samani kadha wa kadha.

19. Ответьте на вопросы по содержанию текста из упражнения 16:
1. Shule za sanaa zina lengo gani? 2. Wanafunzi wa shule hizo hupata mafunzo gani? 3. Baada ya kuhitimu shule za sanaa vijana hufanya nini? 4. Watoto wa shule za kawaida huwezaje kupata ujuzi wa kazi fulani? 5. Kundi la kwanza katika somo la kazi za mikono hufundishwa nini? 6. Kundi la ufinyanzi hushughulika na kazi gani? 7. Uchongaji ni sanaa ya aina gani? 8. Vitu gani hutengenezwa na vijana katika kundi la uchoraji? 9. Kwa nini wazazi huwafurahia na kuwaonea fahari watoto wao wenye kujifunza kazi za mikono?

20. Переведите:
1. Специальные школы мастерства существуют для того, чтобы дать возможность молодежи подготовиться к будущей жизни и получить определенную специальность. 2. Юноша или девушка, окончив школу, может поступить в такое учебное заведение и получить навыки швейного дела, малярного мастерства или кулинарного искусства. 3. Таких специалистов с готовностью возьмут на работу на любое предприятие или в государственное учреждение. 4. Те, кому повезет, смогут добиться быстрых результатов и впоследствии открыть свое собственное дело. 5. Уроки труда проводятся в каждой школе с целью научить детей делать что-либо своими руками, например, лепить из глины цветочные горшки или чайную посуду, делать игрушки или различные украшения. 6. У каждого есть полное право выбрать себе занятие в зависимости от своих собственных предпочтений.

* * *

Mazoezi ya kujiandaa kusikiliza hadithi

Maneno mapya

-chuma собирать, рвать (*цветы, плоды и т.п.*)
-nenepa жиреть, толстеть
kima (-) обезьяна

21. Дайте русские эквиваленты:
-kutana chini ya mti; kando ya mto; ukingoni mwa ziwa; katikati ya ziwa; kando ya njia; -chuma matunda; -chuma malimau; -nenepa upesi; -nenepa kupita kiasi; -tamani kula; -tamani kuogelea; maembe mabivu; maembe ya leo; maembe yaliyooza; -beba mzigo; -beba mtoto mgongoni; dawa ya ugonjwa wa mgongo; dawa ya moyo; -acha mzigo; -rudisha mzigo; -panda juu ya mti.

22. Дайте суахилийские эквиваленты следующих выражений и составьте предложения с каждым из них:
собирать урожай; собирать мусор; собирать цветы; собирать людей; собирать монеты; собирать машины; собираться что-либо делать; собираться вместе; собираться в дорогу; собираться с силами; собирается дождь.

23. Переведите:

1. Michenza mirefu iliota kando ya njia yetu, na watoto walikuwa wakiyachuma matunda yake mara kwa mara. 2. Mwisho hata watu wazima walitamani kula machenza yale. 3. Chakula changu cha asubuhi ni matunda kidogo na kikombe cha chai ya maziwa tu, maana sitaki kunenepa. 4. Bandarini mwa mji ule tuliwaona wafanya kazi wakibeba mabunda makubwa ya katani migongoni mwao. 5. Waganga wanadai kuwa dawa ya ugonjwa huu wa hatari haijapata kuvumbuliwa. 6. Kama ungeliniambia mapema kwamba hupendi kusafiri na mashua, ningelikurudisha pwani mara moja. 7. Kima walipoona gari letu waliogopa sana, wakaruka wakapanda juu ya miti iliyokuwa ukingoni mwa njia. 8. Chui alifahamu kuwa hataweza kumpata tena sungura yule mjanja, akaenda zake.

24. Замените предлоги локативной формой существительного:

katika mti ule; kwenye ukingo wa ziwa; katika kijiji chetu; juu ya mgongo wa mama; ndani ya mfuko wake; katika moyo wangu; kutoka ziwa lile; kati kati ya matawi ya mti; ndani ya meza hii; katika nyumba yako; ndani ya kichwa cha kima; katika maji haya.

25. Вместо точек поставьте местоимение -pi:

1. Kuna maembe ya leo na ya kesho kwa mwuzaji yule, ninunue ...? 2. Sikufahamu tukutane kwenye mtaa ...? 3. Unamwona kima anayembeba mtoto mgongoni mwake? – Nionyeshe kima ... 4. Unajua, niliwaona mamba wengi kwenye kingo za mto huu. – Uliwakuta kwenye ukingo ..., wa kushoto au wa kulia? 5. Kuna dawa za tumbo za aina nyingi dukani kwetu. Unataka dawa ...? 6. Naomba niletee kisu, nataka kulikata papai hili. – Unataka kisu ..., kirefu au kifupi?

26. Переведите:

1. Они встречались на берегу реки каждое утро. 2. Если не хочешь потолстеть, не ешь много сахара и конфет. 3. Давайте нарвем полевых цветов и поставим их в нашу красивую вазу. 4. Если вы не умеете хорошо плавать, не пытайтесь переплыть эту быструю реку. 5. Многие африканские женщины носят своих детей за спиной. 6. В вашей аптеке есть лекарство от малярии? 7. Почему ты заранее не сказал, что эти обезьяны настоящие воришки? 8. Украв наши бананы через открытое окно автомобиля, мартышка прыгнула на дерево и уселась на ветке.

Kusikiliza hadithi

- Прослушайте текст полностью.
- Повторите в паузах фразы вслед за диктором.
- Закончите предложения вместо диктора.
- Задайте друг другу вопросы на суахили по содержанию прослушанного текста и дайте на них ответы.
- Ответьте на суахили на вопросы диктора.
- Изложите письменно на суахили содержание текста.

* * *

Mazoezi

27. Запомните следующие слова и выражения:

-pangusa вытирать, протирать
-pata pancha получить прокол (*шины*)
gurudumu la spea/akiba запасное колесо
spea (-) запчасти
mpira (mi-) резина; шина
usukani (sukani) руль, рулевой механизм
-funga safari отправиться в путешествие

28. Переведите следующий текст и перескажите его на суахили:

Kutunza motokaa

Kila dereva lazima aitunze motokaa yake. Kwanza, ukizoea kupangusa gari lako, utajua sehemu zake na pakiwa na makosa fulani utayatambua upesi. Hakuna haja ya kufundishwa kutengeneza sehemu za injini zilizoharibika. Hiyo ni kazi ya fundi wa kutengeneza injini. Jambo lifaalo kwa dereva ni kujua jinsi ya kutengeneza au kubadili sehemu zinazoharibika mara kwa mara, kwa mfano:

Gari lipatapo pancha, ajue kutia gurudumu la spea.

Gari lisipowaka, awaombe wenzake kumsukuma.

Gari lipunguzapo mwendo wake, aangalie kama lina mafuta au maji ya kutosha.

Gari litoapo sauti ambayo si yake ya kawaida asiendelee na mwendo mpaka amegundua sehemu inayotoa sauti hiyo.

Gari litoapo moshi mwingi au harufu ambayo si ya kawaida, asiendelee na safari yake mpaka agundue sehemu inayoungua au kutoa harufu.

Na bila ya shaka kabla ya kufunga safari dereva lazima aangalie kama kuna haja ya kuipuliza mipira hewa, akague usukani na breki. Jambo la maana sana ni kuona kuwa wakati wote gari lako linatunzwa vizuri.

Ni furaha iliyoje kushika usukani ukifahamu kuwa motokaa yako haina hitilafu zo zote!

29. Переведите диалог:

Maneno ya kusaidia tafsiri

Будьте добры!	**Kwa hisani yako!**
скажем (*вводное слово*)	**tuseme**
подбросить (*кого-л. на автомобиле*)	**kumpa mtu lifti**
Как хотите!	**Hiari yako!**

Водитель: Будьте добры, посмотрите мою машину. Она немного дымит, а я собираюсь отправиться в путешествие.

Мастер: Хорошо. Вы можете оставить машину и забрать ее через несколько часов, скажем, после обеда.

Водитель: Да, конечно. Вот ключи ... Да! Чуть не забыл! Я недавно менял колесо. В моей запаске прокол. Так что отремонтируйте, пожалуйста.

Мастер: Обязательно. Я вижу, что и шины надо подкачать. А машину вам помыть?

Водитель: Пока не надо, протрите только окна. А главное – проверьте двигатель и тормоза.

Мастер: Не волнуйтесь, мы все сделаем. Ваша машина будет, как новая! Наш шофер может подбросить вас, куда скажете.

Водитель: Спасибо, но я лучше пройдусь пешком.

Мастер: Как хотите!

30. Подберите соответствующие окончания пословиц и вспомните их значения:

Lenye mwanzo ...	... ndio mwendo
Kupoteza njia ...	... kabla ya hatari
Njia ya mwongo ...	... lina mwisho
Pole pole ...	... [ni] hasara
Si kila mwenye makucha ...	... pana njia
Akiba ...	... ni fupi
Tahadhari ...	... hukatika pembamba
Kamba ...	... haiozi
Hasira ...	... ndiko kujua njia
Penye nia ...	... huwa simba

31. Напишите сочинение на тему “Kazi ninazozifanya mwenyewe kwa mikono yangu”.

SOMO LA KUMI NA TATU
(marudio)

Mazoezi

1. Tafsiri hadithi ifuatayo:

sisimizi (-) маленький черный муравей
mzinga (mi-) улей
nyuki (-) пчела
asali (-) мед
mwitu (mi-) лес
sifa (-) слава, известность
tikiti maji (ma-) арбуз
asilani никогда
-hisi чувствовать, ощущать
-jadili обсуждать
-angamiza уничтожать
shujaa (ma-) герой; храбрый человек
-bembeleza уговаривать, упрашивать
-angua kicheko заливаться смехом
-dharau презирать
dharau (-) презрение, неуважение

Sisimizi alivyomwangamiza Tembo!

Ni ajabu na kweli, lakini ndivyo ilivyokuwa kwa kijana Sisimizi, mdudu mdogo lakini shujaa na ambaye baadaye aliweza kujipatia sifa nyingi kutoka kwa wanyama na hata wadudu wenzake!

Ilikuwa siku moja ambapo mnyama Tembo ambaye anaaminika kuwa mkubwa kuliko wote mwituni alipokuwa akitishia uhai wa wanyama na wadudu wa mwituni kwa fujo zake za ajabu.

Tembo kwa ukubwa wake akajenga ujeuri na majivuno makubwa kiasi cha kudharau kila kiumbe kilichopita mbele yake, hali iliyowaudhi wenzake kupita kiasi.

Ingawa viongozi wa mwituni walifanya juhudi za kumbembeleza tembo aache fujo, dharau na kujitapa kwake, hali hiyo haikusaidia kitu, kwani alikuwa akiambiwa leo, kesho yake anaongeza fujo na uhalifu wake mara mbili.

Kutokana na hali hiyo, wanyama na wadudu wa mwituni walikusanyika na kufanya mkutano mkubwa kuzungumzia dharau na ujeuri wa Tembo. Mkutano huo ulivuta wanyama na wadudu wa kila aina ukijadili njia mbalimbali za kumwangamiza Tembo

ambaye kwa kweli wanyama na wadudu hao walikuwa wamekwishasumbuka kiasi cha kutosha kwa ajili yake.

Hata hivyo bado hakuna aliyeweza kutoa jibu la kufaa kuhusu jinsi ya kumwangamiza Tembo bila ya kuleta madhara mwituni. Mzee Simba ambaye ndiye aliyekuwa mwenyekiti wa mkutano ule wa wanyama akatoa shauri la kuundwa kwa jeshi la wanyama ili kupambana na Tembo, lakini shauri hilo lilikataliwa kabisa na wenzake, hasa kwa kutambua ugumu wa kupambana naye.

Hiyo ilitokana na ukweli kwamba tembo alikuwa amekwishaharibu ekari nyingi za mashamba ya mazao mbalimbali ya wanyama na hata mizinga ya nyuki iliyotengenezwa na wadudu. Alitumia ukubwa wake, hasa miguu na mgongo wake kuharibu mazao mashambani kwa wanyama waliopanda mboga na matikiti maji, kwani hayo yalikuwa ndiyo chakula chake.

Mbaya zaidi, alipofika kwenye mashamba hayo hakuomba ruhusa kutoka kwa wenye mashamba hayo, bali aliingia na kuanza kushambulia mazao ya shambani kama kwamba amelima yeye. Kwa wadudu waliokuwa wametundika mizinga ya nyuki kwenye miti, alitumia ujanja wa kuiangusha miti hiyo kisha kuila asali yote.

Kwa kweli hali hiyo iliwatia wasiwasi mkubwa na hata umaskini wanyama na wadudu, hasa ikitiwa maanani kuwa kijiji kile cha wanyama kilikuwa cha wakulima waliokuwa wakitegemea zaidi shughuli za kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula na biashara na ufugaji wa nyuki kuendesha maisha yao.

Hali hiyo ya kuharibiwa mashamba na mizinga ya nyuki iliwafanya wanyama wengi kufikiria kuhama kijiji hicho waende kujitafutia nafasi ya kuishi sehemu nyingine, kwani hata uongozi wa kijiji ulikuwa umeshindwa kumsimamia na kumzuia Tembo huyo. Kwa maneno mengine, hali ya hasara aliyokuwa akisababisha Tembo ilionekana wazi machoni pa kila mmoja, kiasi cha wengine kuanza kusema kwamba labda Tembo yuko juu ya sheria kutokana na jinsi alivyokuwa akijitapa na kudharau wote.

Hata hivyo hali hiyo ilimsumbua sana kijana Sisimizi, ambaye kwa kushirikiana na uongozi wa kijiji alimtaka mwenyekiti Mzee Simba afanye mkutano ili Sisimizi aelezee lengo lake la kutaka kumwangamiza Tembo.

Habari za kwamba Sisimizi ametaka kumwangamiza Tembo zilipowafikia wanakijiji wengine ziliwafanya wengine kuangua vicheko na kumtaka mwenyekiti wao asijisumbue hata kidogo kwa sababu ati kijana Sisimizi alikuwa anatania tu.

Lakini kwa kufikiria uzito wa tatizo lenyewe pale kijijini, Mzee Simba akafanya mkutano uliovuta wanyama na wadudu wa kila aina, ambapo siku hiyo Sisimizi alitoa ahadi kumwangamiza Tembo hata bila ya msaada wa mnyama mwingine. Ingawa wanyama wengine walimcheka sana kijana Sisimizi na kudai kuwa asingemweza tembo asilani, yeye alisema mbele ya mkutano ule, hasa wazee wa kijiji, kuwa kwa hakika atafanya kama alivyoahidi.

Basi siku moja Tembo akiwa amesinzia baada ya kushiba mboga alizoiba kutoka shamba la mkulima mmoja pale kijijini, Sisimizi alimsogea kimya kimya na kisha kuingia sikioni mwake. Alikwenda moja kwa moja hadi ndani kabisa ya sikio na kujificha katika sehemu ambayo Tembo asingeweza kujua hata kidogo ni kitu gani kimo ndani yake, na akaanza kumchokoza.

Tembo alipohisi kwamba kuna kitu sikioni mwake, alishtuka na kuanza kupiga makelele ya kumtaka yule aliyekaa ndani yake atoke kabla hajakasirika. Lakini kelele zile hazikusaidia kitu!

Kwa hasira Tembo alinyanyuka kutoka alipokuwa na kuanza kujipiga huku na kule akijitahidi kumwondoa Sisimizi sikioni mwake, lakini hiyo haikusaidia kitu. Hali hiyo ilimwumiza sana Tembo, lakini kila alipojaribu kumwondoa, ndivyo alivyozidi kujiumiza zaidi.

Alifanya hivyo kuanzia asubuhi mpaka jioni akipita kwenye miti mikubwa na kujigonga ovyo, lakini wapi, kwani Sisimizi alikuwa amemshikilia vizuri, hali ilimfanya Tembo aanze kuchoka na kukosa nguvu, huku akiumizwa vibaya mno. Kwa kuwa Tembo alikuwa ametokwa damu nyingi mwilini katika juhudi zake za kujigonga huku na kule, hali yake ilidhoofika na baada ya saa chache kupita alikufa.

Habari za kijana mdogo Sisimizi kumwangamiza Tembo, mnyama aliyekuwa anasumbua mji mzima zilienea kama moto wa kiangazi na kukifanya kijiji kizima kitulie kwa furaha ya kutoamini kile kilichotokea. Lakini ndio uliokuwa ukweli wenyewe.

2. Jibu maswali kuhusu hadithi hiyo:
1. Jinsi gani Tembo alikuwa akiwaudhi wanyama wote wa mwituni? 2. Viongozi wa wanyama waliamua kuufanya mkutano kwa ajili gani? 3. Tembo alileta hasara gani kwa wakulima? 4. Sisimizi alitumia hila gani kumwangamiza Tembo?

3. Eleza kwa Kiswahili hadithi juu ya sisimizi aliyemwangamiza tembo.

4. Tafsiri hadithi ifuatayo:

aibu (-) позор; стыд
-kwaruza царапать
-nyamaza молчать, замолкать

Jogoo wa ajabu

Zamani Pazi alikuwa mtoto mwenye tabia mbaya. Alikuwa hana huruma, aliwapiga mbwa, ng'ombe, mbuzi na hata kuku bila sababu. Kila alipotumwa kuwapeleka kuku mahali, aliwachukua vibaya, yaani kichwa chini miguu juu. Baba yake alimwonya mara nyingi lakini Pazi hakusikia.

Siku moja Pazi aliitwa na baba yake akamwambia, "Kamata kuku wawili ukawauze sokoni." Pazi akamwuliza, "Kuku yupi na yupi?" Baba yake akajibu, "Wakamate Nihurumie na Naumia." Pazi akawafukuza na kuwapiga. Baba yake akamwambia, "Usiwatupie kuku mawe. Wafukuze tu." Pazi akaendelea kuwafukuza kuku. Kuku walipochoka aliwakamata, akawafunga miguu. Pazi alipoaga baba yake akamwambia, "Haya, nenda, lakini kumbuka, uwachukue vizuri na usiwapige. Pia usichelewe kurudi." Pazi aliitikia, "Haya baba, nimesikia."

Pazi akaondoka kwenda sokoni. Alipokwenda mbali kidogo na nyumbani kwao, aliwapiga kuku na kuwachukua vibaya. Kuku wakawa wanalia. Mmoja alilia, "Nihurumie! Nihurumie!" Mwingine akalia, "Naumia! Naumia!" Pazi hakujali. Aliendelea na safari yake.

Njiani Pazi alimkuta jogoo wa ajabu akitafuta chakula chini ya mwembe. Alisikia wale kuku wakilia, "Nihurumie! Naumia!" Aliwaangalia akaona jinsi wanavyopata taabu.

Yule jogoo aliwahurumia wale kuku na kumkasirikia Pazi. Mara jogoo akageuka akawa mkubwa sana. Akamwendea Pazi. Akasimama mbele yake na kuwika kwa sauti kubwa, "Kokorikoo!" Mara Pazi alisimama huku akitetemeka. Jogoo akamwuliza Pazi, "Kwa nini unafanya mambo haya?" Pazi hakujibu. Alizidi kutetemeka. Jogoo akaendelea kumwuliza, "Husikii?" Pazi akajibu, "Nasikia!" Jogoo akamwuliza, "Sasa?" Pazi akajibu kwa woga, "Sielewi!" Jogoo akamwuliza, "Huelewi nini?" Jogoo akarudia, "Nasema kwa nini unafanya mambo haya?" Pazi akauliza, "Mambo gani?" Jogoo akasema, "Mambo unayafanya mwenyewe na halafu unajidai huelewi. Kwanza unawapiga hao kuku, halafu unawachukua vibaya. Unafanya makosa!"

Pazi akanyamaza. Aliona aibu. Jogoo akasema, "Basi leo utanitambua." Mara akamrukia Pazi usoni. Akamkwaruza, akamshika, akamnyanyua, akampinduapindua kichwa chini miguu juu. Pazi akalia kama wale kuku, "Nihurumie! Nihurumie! Naumia! Naumia! Nakuomba sana. Tafadhali niachie! Sitawachukua tena kuku vibaya." Jogoo akajibu, "Hapana. Wewe mwongo. Husemi ukweli. Tena humtii baba yako. Leo utafika sokoni, kichwa chini miguu juu." Pazi akajibu, "Lakini ukinichukua vibaya nitakufa." Jogoo akamwuliza, "Hawa kuku hawakuwa wakiumia?" Pazi akajibu, "Tafadhali nimekosa. Nimekosa sana sitarudia."

Jogoo akajibu, "Hapana. Leo ni leo. Nikisema utafika sokoni kichwa chini miguu juu, jua utafika sokoni ukiwa hivyo." Jogoo akaendelea kumchukua Pazi kichwa chini miguu juu. Pazi akazidi kulia. Akasema, "Kweli sitafanya tena. Sitawachukua tena vibaya." Jogoo akamwuliza, "Sasa utawachukua namna gani?" Pazi akajibu, "Nitawachukua na kuwashika vizuri. Miguu itatazama chini na kichwa juu kama kawaida. Tena sitawapiga." Jogoo akazidi kuuliza, "Na wale mbwa na ng'ombe je?" Pazi akajibu, "Hata hao pia sitawapiga. Nitawapa maji na chakula."

Jogoo akasema, "Vizuri. Ni lazima uwe mwema kwa wanyama wote. Tangu sasa inakubidi kuwa mtii kwa wakubwa wako."

Jogoo alimwachia Pazi. Pazi akarudi akawachukua kuku wale vizuri. Akaenda sokoni. Tangu siku ile Pazi akawa rafiki wa wanyama.

5. Eleza hadithi juu ya jogoo wa ajabu kama kwamba wewe ni Pazi.

6. Uibadilishe matini ifuatayo iwe mazungumzo:

Vijana na simba

Magembe, Kalukwa, Luhala na Busara (Разумный) walikwenda kuwinda. Huko porini walimwona simba mzee amelala. Simba huyo alionekana kama aliyekufa. Vijana watatu walisema kwamba watachukua mkia, kucha na kichwa cha yule simba. Lakini Busara aliwaonya wasicheze na hatari. Alisema kwamba simba huyo hakufa na hivyo akiguswa anaweza kuwaua vijana wote. Hata hivyo wenzake walimcheka wakamwita mwoga. Wakamsogelea simba na Busara akapanda juu ya mti.

Magembe, Kalukwa na Luhala walimkaribia simba. Kalukwa alimshika simba mkia kwani alisema kwamba anataka mkia wa kuchezea ngoma. Magembe alimshika simba mguu. Alitaka kuchukua kucha zake. Luhala alimshika shingo. Lakini alipoanza kumkata, simba aliamka ghafula, akamkamata Luhala na kumla. Magembe na Kalukwa walikimbia, kila mtu njia yake.

Simba alipomshiba aliondoka. Busara aliteremka mtini, akarudi nyumbani haraka. Naam, si vizuri kucheza na hatari.

7. Soma kisa kifuatacho ukakieleze kwa Kiswahili. Jaribu mwenyewe kutambua maana ya maneno usiyoyafahamu:

Dada Alyonushka na kaka Ivanushka
(Imetafsiriwa na Mbigili Marcus)

Hapo zamani palikuwa na wazee wawili mke na mume, walikuwa na binti aliyeitwa Alyonushka na kijana wa kiume aliyeitwa Ivanushka.

Baada ya muda wale wazee walifariki, na wale watoto, Alyonushka na Ivanushka waliachwa peke yao.

Siku moja yule Alyonushka aliondoka nyumbani kwenda kufanya kazi, alimchukua pia mdogo wake Ivanushka.

Kwa kweli walikuwa na safari ndefu sana kupita mbuga pana iliyokuwa mbele yao. Baada ya kutembea kwa kitambo kirefu Ivanushka alianza kujisikia kiu. "Dada Alyonushka, najisikia kiu," alisema Ivanushka. Dada yake akamwambia, "Kuwa mvumilivu mdogo wangu, baada ya muda mfupi tutafika kisima kilipo."

Walitembea, wakatembea, na wakati huo jua lilikuwa juu ya utosi katika anga. Hali ilikuwa ya joto sana na wale watoto wakaudhika sana.

Waliona kwato ya ng'ombe iliyokuwa imejaa maji, na Ivanushka akasema, "Naweza kunywa maji haya kwenye kwato, dada Alyonushka?" Alyonushka akasema, "Hapana, mdogo wangu, kama utakunywa utageuka na kuwa ndama." Ivanushka alikubaliana, na wakatembea kitambo kirefu tena. Jua lilikuwa kali sana angani, joto lilikuwa baya sana na wakawa na huzuni sana.

Aidha waliona tena kwato ya farasi iliyokuwa imejaa maji, Ivanushka akasema, "Naweza kunywa maji haya kwenye kwato, dada Alyonushka?" – "Hapana, mdogo wangu, kama utakunywa utageuka na kuwa mwanafarasi."

Ivanushka alihema kwa majonzi, wakaendelea tena kutembea mbele. Walitembea, wakatembea, na jua lilikuwa bado kali sana angani, na hewa ilikuwa kavu sana wakajisikia kama kwamba wanataka kufa. Wakaona pia kwato ya mbuzi iliyokuwa imejaa maji, na Ivanushka akasema, "Ninakufa kwa kiu, dada Alyonushka. Naweza kunywa maji kwenye kwato?" – "Hapana, mdogo wangu, kama utafanya hivyo utageuka na kuwa mwanambuzi."

Lakini Ivanushka hakumsikiliza dada yake na akayanywa yale maji kwenye kwato ya mbuzi. Baada ya kufanya hivyo, muda huo huo akageuka na kuwa kimbuzi kidogo cheupe.

Alyonushka akamwita kaka yake, badala ya Ivanushka, kimbuzi kile kidogo cheupe kilikwenda kwake. Alyonushka alitoa machozi. Alikaa akiwa analia, wakati kile kimbuzi kidogo cheupe kikirukaruka karibu naye kwa michezo yake.

Muda huo huo mfanyabiashara mmoja alikuja akiwa kwenye farasi wake. Akamwuliza Alyonushka, "Unalilia nini mwanamwali mzuri?" Alyonushka alimwambia yule mfanyabiashara shida zake. Mfanyabiashara akasema, "Nikuoe, mwanamwali mzuri.

Nitakuvalisha dhahabu na nguo za hariri na huyu mbuzi mdogo ataishi pamoja na sisi."

Alyonushka alifikiria kwa muda na mwishowe alikubaliana kuolewa na yule mfanyabiashara.

Waliishi pamoja wakiwa na furaha, na yule mbuzi mdogo aliishi pamoja nao wakila na kunywa kikombe kimoja na Alyonushka.

Siku moja yule mfanyabiashara aliondoka nyumbani kwa ajili ya safari zake, na ghafla pale nyumbani alitokea mchawi kutoka mahali pasipojulikana. Huyo mchawi alisimama chini ya dirisha la Alyonushka akamwomba kwa upole na ukarimu kwenda kuoga naye katika mto.

Alyonushka alimfuata yule mchawi hadi mtoni. Walipofika kule, yule mchawi alimwangusha Alyonushka na kumfungilizia jiwe shingoni na kumtupa ndani ya maji, yule mchawi akachukua umbile la Alyonushka. Halafu akavaa nguo zake na kwenda nyumbani. Hakuna mtu aliyegundua kuwa hakuwa Alyonushka, watu walidhani ndiye Alyonushka, kumbe alikuwa ni yule mchawi.

Mfanyabiashara aliporudi nyumbani, na yeye hakuweza kukisia. Ni yule mbuzi mdogo tu ndiye aliyeelewa kilichotokea. Alikwenda karibu na mto ule akawa anachungulia kwa kichwa bila kuyagusa maji yale wala kunywa. Asubuhi na jioni.

"Dada, mpendwa dada Alyonushka!

Ogelea nje, ogelea uje kwangu."

Yule mchawi alijua hayo na kumwomba yule mume wake amwue yule mbuzi mdogo. Mfanyabiashara yule alimhurumia sana yule mbuzi mdogo na alikuwa na upendo naye. Lakini yule mchawi aliendelea kumbembeleza na kumshawishi na hapakuwa na la kufanya ila kumkubalia. "Vizuri, umwue", alisema.

Yule mchawi alikuwa tayari na moto mkubwa jikoni, chungu kikubwa kilichokuwa kikichemka na kisu kikubwa ambacho kilikuwa kimenolewa.

Mbuzi mdogo akagundua kwamba atauawa, akamwambia yule mfanyabiashara, "Niruhusu niende mtoni kabla sijafa, nikanywe maji ya mwisho." – "Nenda", alisema mfanyabiashara.

Mbuzi mdogo alikimbia kuelekea mtoni na kusimama juu ya ukingo wa mto, na alilia kwa huruma,

"Dada, dada mpendwa Alyonushka!
Ogelea nje, toka uje kwangu,
Moto unawaka kwa nguvu,
Chungu kinachemka,
Visu vinanolewa,
Na ninakwenda kufa."

Na Alyonushka alijibu akiwa kwenye mto,

"Kaka, kaka mpendwa Ivanushka!
Jiwe zito limenilalia mabegani!
Kamba za hariri zimeitega miguu yangu.
Mchanga wa njano unagandamiza kifua changu."

Yule mchawi alianza kumtafuta yule mbuzi mdogo, na hakuweza kumpata, hivyo alimwita mtumishi na kumwambia, "Nenda kamtafute mbuzi yule na umlete kwangu." Mtumishi yule alikwenda mtoni, alimwona yule mbuzi akikimbiakimbia juu na chini ya ukingo wa mto na kuita kwa huzuni,

"Dada, mpendwa dada Alyonushka!
Uogelee utoke, uje kwangu,
Moto unawaka kwa nguvu,
Vyungu vinachemshwa,
Visu vinanolewa,
Ninakwenda kufa."

Kutoka ndani ya mto sauti ya mtu ilitoka ikisema,

"Kaka, kaka mpendwa Ivanushka,
Jiwe zito limelalia mabegani,
Kamba za hariri zimetega miguu yangu,
Mchanga wa njano unagandamiza kifua changu."

Mtumishi yule alikimbia kwenda nyumbani na kumwambia mkubwa wake yote aliyoyasikia na kuyaona. Mfanyabiashara yule aliwaita watu wengine wakaenda wote kule mtoni na kutupa nyavu za hariri ndani ya mto, na kumkokota Alyonushka nje kwenye ukingo wa mto. Walimfungua lile jiwe ambalo lilikuwa shingoni mwake, walimzamisha katika chemchemi kwa ajili ya kumwogesha na baada ya kumwogesha walimvalisha nguo zenye mng'aro mzuri. Alyonushka alirudia tena uhai wake na alikuwa mzuri zaidi ya wakati wa mwanzo.

Mbuzi yule mdogo alikuwa kama mwenda wazimu kwa furaha. Alijigeuza kichwangomba mara tatu, na bila kutegemea aligeuka na kuwa na umbile la kawaida tena.

Na yule mchawi mwovu alifungwa kwenye mkia wa farasi na kuburuzwa kwenye mbuga iliyo wazi.

8. Jifunza kwa moyo kisa kifuatacho:

Palikuwa na mwanamume mmoja jina lake Hasani, alikuwa na kasuku (попугай), na kasuku yule akawa hodari sana akajua sana kutamka (произносить) maneno ya kibinadamu. Kila siku Hasani huenda shambani kulima, lakini mke wake Fatuma hukaa nyumbani mwao apike chakula. Jioni Hasani hurudi nyumbani, humwuliza kasuku habari za nyumba, na kasuku yule akamwambia habari za makosa yote ya mke wake Fatuma. Kwa sababu hii, Fatuma akakasirika sana akamchukia (ненавидеть) kasuku yule.

Usiku mmoja Fatuma alifanya hila amdanganye kasuku. Mume wake Hasani alipokwisha kwenda shambani alinde mavuno yake, Fatuma akagongagonga vyombo, akapiga kelele nyingi. Lo! Yule kasuku akafikiri inapiga radi. Halafu aliporudi bwana wake, kasuku alimwambia habari za radi. Aliposikia habari hizi, Hasani alishangaa sana, kwa sababu alijua radi haikupiga, akaona kasuku wake anataka kumdanganya, amesema uwongo. Tena, akafikiri maneno yote aliyoyasema kumlaumu Fatuma ni ya uwongo pia. Hasani akakasirika sana, akamkamata yule kasuku akamwua.

SOMO LA KUMI NA NNE
(Kusikiliza hadithi)

1. Sikiliza hadithi "**Chatu na mbwa**".

chatu (-) питон, удав **-kasirisha** сердить

2. Jibu maswali ya msomaji.

3. Usikilize tena hadithi hiyo na uieleze kwa Kiswahili.

4. Sikiliza hadithi "**Sungura alivyopata mkia mfupi**".

-chafua загрязнять, пачкать

5. Jibu maswali ya msomaji.

6. Usikilize tena hadithi hiyo uitafsiri kwa Kirusi.

7. Sikiliza hadithi "**Sisimizi shujaa**".

8. Usikilize hadithi hiyo kwa mara ya pili ukayaibu maswali ya msomaji.

9. Uieleze hadithi hiyo kama kwamba **wewe** ndiye sisimizi huyo.

10. Sikiliza hadithi "**Mbu na tembo**".

-nyonya сосать, высасывать

11. Jibu maswali ya msomaji.

12. Usikilize tena hadithi hiyo uitafsiri kwa Kirusi.

13. Sikiliza hadithi "**Paka na panya**".

jembe (ma-) мотыга **-fyeka** корчевать; вырубать
-komaa достигать зрелости

14. Jibu maswali ya msomaji.

15. Usikilize tena hadithi hiyo uiandike kwa Kiswahili.

16. Sikiliza hadithi "**Ndege walivyopata manyoya**".

17. Jibu maswali ya msomaji.

18. Sikiliza tena hadithi hiyo uitafsiri kwa Kirusi kwa kuandika.

* * *

Словарь активной лексики

Урок 1

nyota (-) звезда
mbingu (-) небо; небеса
usingizi (ед.) сон
uji (ед.) жидкая каша
zana (-) инструмент, прибор; орудие
sahani (-) тарелка; блюдо
bakuli (-; ma-) глубокая чашка, миска, таз
sufuria (-) кастрюля
kikaango (vi-) сковорода
birika (ma-) чайник
uchovu (ед.) усталость, изнеможение
kisima (vi-) колодец
pipa (ma-) 1)бочка 2)бак
giza, kiza (-; ma-) темнота, сумерки
mkeka (mi-) циновка
ajali (-) 1)несчастный случай, происшествие 2)авария, катастрофа
paa (ma-) крыша, кровля
wivu (ед.) 1)зависть 2)ревность
bati (ma-;-) жестяной лист; жесть
kitoweo (vi-) приправа (*из мяса, рыбы, курицы или овощей*)
kibarua (vi-) поденный рабочий
vuno (ma-) 1)урожай 2)сбор урожая
binadamu (-) человек
kale (-) древность, старина
hapo kale когда-то давно
kimya (-) 1)молчание 2)тишина
msumeno (mi-) пила
nyundo (-) молот, молоток
kekee (-) сверло, бур
msumari (mi-) гвоздь
mkutano (mi-) 1)встреча 2)собрание, совещание
-oa жениться, брать жену
-olewa выходить замуж, быть замужем
-kaanga жарить, поджаривать
-nong'oneza шептать
-loa/ -lowa промокать
-paramia [быстро] влезать, взбираться, вскарабкиваться
-simulia повествовать, рассказывать
-chinja резать, забивать (*скот*)
-fum[u]ka рваться, расходиться по шву
-jaa наполняться, быть полным /наполненным
-zidi 1) увеличиваться, возрастать 2)превосходить
-palilia полоть, пропалывать
-zito 1)тяжелый 2)трудный
-tamu 1)сладкий 2)вкусный
-nono толстый, жирный, упитанный (*о животных*)
-wivu 1)завистливый 2)ревнивый
mbona почему?, для чего?
usiku kucha всю ночь
kimyakimya 1)молча 2)тихо, бесшумно
ghala (-; ma-) склад; кладовая
kisha впоследствии; затем, потом

Урок 2

asili (-) источник; происхождение
adhuhuri (-) полдень (*от 12 до 14 часов*)
alasiri (-) время после полудня (*от 14 до 18 часов*)
daraja (-; ma-) 1)мост 2)ступень
taabu (-) трудность, затруднение
umoja (ед.) единство
shimo (ma-) яма; нора; отверстие
huruma (-) сочувствие, сострадание
doadoa (ma-) пятно; крапинка
mwili (mi-) тело, туловище
mdomo (mi-) 1)губа 2)рот
pipi (-) конфета (*карамель*)
umri (ед.) возраст
sumu (-) яд, отрава
ng'ambo (-) 1)одна из двух противоположных сторон (*реки, улицы и т.п.*) 2)заграница
uchokozi (ед.) 1)провокация 2)агрессия
mlinzi (wa-) 1)сторож, охранник 2)защитник
mate (мн.) слюна
mbizi (-) прыжок в воду, ныряние
harufu (-) запах, аромат
risasi (-) пуля; патрон
tone (ma-) капля
kenge (-) варан
jeraha (ma-) 1)рана 2)болячка
punde вскоре, через некоторое время
punde si punde вскоре, мгновенно, моментально
-hesabu считать, подсчитывать
-keti садиться
-patikana быть в наличии
-fanana быть похожим
-tupa бросать, кидать
-vuka переходить, пересекать
-ondoa удалять, устранять
-okoa спасать, избавлять
-rudisha возвращать, отдавать назад
-vuta тянуть, тащить
-amsha будить
-vua раздеваться, снимать одежду
-zama тонуть, погружаться в воду
-bweka лаять, гавкать
-tambaa ползать, ползти
-nyanyua поднимать
-kumbatia обнимать
-shtuka поражаться, удивляться
-tambua узнавать, распознавать; догадываться
-poteza терять, утрачивать
-umiza причинять боль,

uamuzi/ uwamuzi (ед.) решение
kishindo (vi-) шум; стук; удар
mbio (-) бег; гонки
adui (-; ma-) враг, противник
bunduki (-; ma-) ружье; винтовка
sikitiko (ma-) огорчение, сожаление
siafu (-) муравей
mwewe (-; wewe) коршун
ovyo зря, напрасно
-sikitika 1)горевать 2)сожалеть
-shuka спускаться, опускаться
-ororo мягкий, нежный
-bivu спелый, зрелый
-bichi 1)неспелый, незрелый 2)свежий
maskini бедный, нищий

Урок 3

moshi (ед.) 1)дым 2)пар
honi (-) гудок, сирена
motokaa (-) автомобиль
mafuta (мн.) 1)масло, жир 2)нефть; топливо
injini (-) двигатель, мотор
kifuniko (vi-) крышка
mjinga (wa-) глупец, дурак
kofi (ma-) 1)ладонь 2)аплодисменты
alfajiri (-) рассвет, утренняя заря (*≈в 4-5 часов*)
ukanda (kanda) ремень, пояс, лента
mlafi (wa-) обжора, чревоугодник
woga (ед.) страх, боязнь
mwiko (miiko) половник
ruhusa/ ruhsa (-) разрешение, позволение
rubani (ma-) пилот, летчик
ukungu (ед.) туман
chungu (vy-) горшок (для варки пищи)
blanketi (ma-) одеяло
-kanyaga наступать (*ногой*), наезжать
-gonga 1)ударять, бить 2)ударяться, сталкиваться
-tangaza объявлять, сообщать
-jali обращать внимание, придавать значение
-shangaa удивляться, изумляться
-funika покрывать, накрывать
-chemka кипеть, бурлить
-shangilia/-shangiria устраивать овацию, приветствовать (*криками*)
-tayarisha приготавливать, готовить
-simamisha останавливать, прекращать
-fungamana сплетаться, переплетаться
-jikaza брать себя в руки, собираться с силами
-sinzia дремать; засыпать

kibiriti/ kiberiti (vi-) спичка
mafuta ya taa керосин
jirani (ma-; -) сосед
[-a] jirani соседний; близкий
ila за исключением; кроме как; только
-bonyea сплющиваться
-nukia хорошо пахнуть, благоухать
-kagua осматривать, обследовать; инспектировать
-songa ugali готовить кашу
-zima гасить, тушить; глушить
-hifadhi 1)хранить, беречь 2)защищать
-pakua перекладывать пищу из кастрюли на тарелку, подавать пищу на стол
-inua поднимать
-ota ndoto 1)видеть сон 2)мечтать
-dhani думать, считать
-mwaga выливать, разливать, проливать
-kwea восходить, взбираться

Урок 4

mfugaji (wa-) фермер, скотовод
ufugaji (ед.) животноводство, разведение (животных)
mchungaji (wa-) пастух
maana (-) 1)смысл, значение, суть 2)потому что
mwiba (mi-) шип, колючка
malisho (мн.) пастбище, выпас
ndama (-) детеныш домашнего животного; молодняк
mkuki (mi-) копье
upinde (pinde) 1)лук 2)дуга, изгиб
mshale (mi-) стрела
jike (ma-) самка
dume (ma-) самец
chuma (vy-) железо, металл
siagi (-) сливочное масло
samli (-) топленое масло
mhandisi (wa-) инженер
ubaguzi (ед.) неравенство, дискриминация
hasara (-) 1)ущерб, убыток 2)вред
ngozi (-) кожа, шкура
mali (-) 1)имущество, собственность 2)богатства
uhuru (ед.) независимость, свобода
ghafula/ ghafla неожиданно, вдруг
wino (ед.) чернила
-kama выдавливать; доить
-himiza торопить, поторапливать
-karipia ругать; упрекать
-udhi беспокоить, докучать
-tisha пугать, устрашать
-donoa клевать
-chuna сдирать, снимать (*кожу, шкуру*)
-kauka сохнуть, высыхать
-kausha высушивать, сушить

ubishi (ед.) спор, разногласия
kasi (-) быстрота, скорость
maiti (-) умерший человек, труп
mbayuwayu (-) ласточка
mwanahewa (w-) летчик, пилот
mgongo (mi-) спина, спинной хребет
uti wa mgongo позвоночник; основа, стержень
akina, kina (-) родня, семья
kanga (-) цесарка
majivuno (мн.) гордость, высокомерие
ugomvi (ед.) спор, ссора, конфликт
jamaa (-) 1)родственник, член семьи 2)товарищ, приятель
-sitawi 1)успешно произрастать 2)процветать, преуспевать
-tegemea 1)зависеть 2)надеяться, рассчитывать
-hitimu заканчивать, завершать
-kimbiza 1)обращать в бегство 2)гнать, гнаться
-zuka возникать, появляться
-tuma посылать, отправлять
-choka уставать, утомляться
-dondoka выливаться по капле
-dondosha капать, выливать по капле

Урок 5

faida (-) выгода, польза
mganga (wa-) 1)врач, доктор 2)знахарь
akili (-) ум, рассудок
mwenzi (wenzi) 1) товарищ, друг, приятель 2)коллега
maarifa (мн.) 1)знания 2)умение, опыт
ujuzi (ед.) 1)знание 2)мастерство, квалификация
uwezo (ед.) 1)возможность 2)способность
zahanati (-) медпункт, поликлиника
adhabu (-) наказание
unadhifu (ед.) чистота, аккуратность
darubini (-) микроскоп; телескоп, бинокль
bingwa (ma-) знаток, специалист
msaidizi (wa-) помощник, ассистент
matibabu (мн.) лечение
moyo (mioyo, nyoyo) сердце, душа
huduma (-) услуга; обслуживание
-hudumu служить, обслуживать
shughuli (-) деятельность, занятие
-shughulika заниматься (*каким-л. делом*)
-geuka превращаться
-bahatisha рисковать; действовать наугад

kichaka (vi-) кустарник; заросли
maradhi (мн.) заболевание, болезнь
ubwabwa (ед.) жидкая [рисовая] каша (*для детей или больных*)
haja (-) потребность, нужда, необходимость
balaa (-; ma-) беда; бедствие
sharti (ma-) 1)обязательность 2)условие, требование
hiari (-) воля, желание
mzizi (mi-) корень, корешок; корнеплод
harag[w]e (ma-) фасоль
mwanakijiji (w-) деревенский житель, крестьянин
jumbe (ma-) староста
msamaha (mi-) прощение, извинение
kiboko (vi-) 1)плеть (*из кожи бегемота*) 2)удар плетью
koo (ma-) горло, гортань
Heko bwana!
-pasua 1)разрезать, рассекать 2)оперировать, делать операцию
-zoea привыкать; приобретать навык
-bana жать, давить
-dhoofu слабеть, терять силы
-lazimisha заставлять, вынуждать
-tamani страстно желать, жаждать
-chapa ударять, наносить удар
-am[u]ru приказывать, предписывать
fulani какой-то; некоторый
-aminifu надежный, заслуживающий доверия
bali но, однако, напротив
ikiwa [в случае] если
ingawa хотя; несмотря на то что
japo хотя бы
Поздравляю! (Молодец!)

Урок 6

mwandishi (wa-) писатель; автор
msomaji (wa-) читатель
jalada (-; ma-) переплет, обложка
idadi (-) число, количество
alama (-) знак; указатель
mfupa (mi-) кость
mbao (-) древесина
ganda (ma-) 1)кора, корка 2)кожура 3)скорлупа, шелуха
udongo (ед.) 1)почва 2)глина
katani/ kitani (-) сизаль (*волокно*)
pamba (-) 1)хлопок 2)вата
risasi (-) свинец
shukrani (-) благодарность
maktaba (-) библиотека
kiwanda (vi-) предприятие, завод, фабрика
mnofu (mi-) мякоть, филе
-waza думать, размышлять

pango (ma-) 1)пещера 2)нора, берлога
kaburi (ma-) могила, склеп, гробница
hekalu (-) храм, молитвеный дом
Mmisri (wa-) египтянин
Mchina (wa-) китаец
Mwarabu (wa-) араб
Mungu (miungu) Бог, божество
uso (nyuso) лицо
sura (-) внешность, облик
mtindo (mi-) метод, способ; образец
herufi (-) буква
mtego (mi-) ловушка, капкан, западня
-vumbua 1)изобретать 2)находить, обнаруживать
-itikia отзываться, откликаться
-gusa трогать, [при]касаться притрагиваться,
-tunga 1)сочинять 2)собирать; составлять
-sogea приближаться, придвигаться
-shiriki участвовать
-papasa трогать, ощупывать
badala ya вместо (*кого-л., чего-л.; того чтобы*)
-kuukuu старый, изношенный

Урок 7

maendeleo (мн.) развитие, прогресс
madhumuni (мн.) цель, намерение
makubaliano (мн.) 1)согласие 2)соглашение, договоренность
biashara (-) торговля, бизнес
hamu (-) желание, страсть
mahitaji (мн.) нужда, потребность
shaba (-) медь
dhahabu (-) золото
thamani (-) 1)цена, стоимость 2)ценность
utumiaji (мн.) использование, применение
tokeo (ma-) результат, итог; следствие
mpango (mi-) план, программа
juhudi (-) 1)усилие 2)усердие, старание
noti (-; ma-) бумажные деньги
-amini верить, доверять
-hangaika суетиться; заниматься (*чем-л.*)
-rahisisha упрощать, облегчать
-jitapa хвастать[ся], хвалиться
-changanya 1)соединять 2)смешивать
-badilisha заменять, обменивать
-dondosha ронять; сбрасывать
-wamba обтягивать, натягивать (*что-л. на что-л.*)

mwongo (wa-) лгун, обманщик
uongo, uwongo (ед.) ложь, неправда
pembe (-) угол; уголок
mkia (mi-) хвост
bawa (ma-) крыло (*птицы, насекомого*)
tawi (ma-) ветвь, ветка
-danganya обманывать
-panga 1)расставлять, размещать 2)планировать
baina ya между; среди
kando (-), kandokando 1)край, сторона 2)берег
kando ya сбоку, скраю, у
-tupu пустой, порожний

Урок 8

mashua (-) лодка; шлюпка
mtumbwi (mi-) лодка (*долбленка*)
merikebu (-) корабль; теплоход
chombo (vy-) судно; корабль
kasia (ma-) весло
bidhaa (-) товар
poromoko (ma-) лавина; поток
poromoko la maji водопад
gogo (ma-) ствол срубленного дерева; пень; бревно
dizeli (-) 1)дизельный двигатель 2)дизельное топливо
[kwa] taratibu 1)осторожно, осмотрительно 2)постепенно
mviringo (mi-) 1)круг, окружность 2)шар
gharika (-) потоп, наводнение
mzee (wa-) старый человек, старик
-zee старый; пожилой
mwananchi (w-) житель, гражданин (*страны*)
kipepeo (vi-) бабочка; мотылек
nungunungu (-) дикобраз
kucha (ma-) коготь
kijia (vi-) дорожка, тропинка
karne (-) век, столетие
kapteni (ma-) капитан
tanga (ma-; -) парус
baharia (ma-) моряк, матрос
-simamisha ставить прямо; выпрямлять; устанавливать
-thibitisha подтверждать, уточнять
-furika переливаться через край, выходить из берегов (*о реке*)
-enea распространяться
-unda строить, сооружать, конструировать
-sokota 1)крутить, скручивать 2)плести
-jivuna 1)хвастать[ся] 2)важничать, кичиться
-tafuna 1)жевать 2)есть
-chonga строгать, обтесывать
-tabiri предсказывать, прогнозировать
-vuja протекать; пропускать воду
-ng'oa вырывать, выдергивать; корчевать
hafifu слабый, хилый;

hekima (-) мудрость; знание
umeme (ед.) 1)молния 2)электричество
anasa (-) роскошь, комфорт
dobi (ma-) прачка

Урок 9

usalama (ед.) безопасность
mjenzi (wa-) строитель
ujenzi (ед,) стройка, строительство
uchumi (ед.) экономика; хозяйство
roho (-) 1)душа, жизнь 2)нрав, характер
ngamia (-) верблюд
farasi (-) лошадь, конь
kobe (ma-) черепаха
pundamilia/ punda milia зебра
kivuko (vi-) 1)переправа 2)переход 3)паром
leseni (-) лицензия, удостоверение; права (*водительские и т.п.*)
mtaa (mi-) 1)район (*города*) 2)улица
msururu, msululu (mi-) цепь, ряд; серия
tukio (ma-) случай, событие
uhalifu (ед.) правонарушение, преступление
tabia (-) 1)характер, натура 2)привычка
hitilafu (-) дефект, недостаток; неисправность
tope (ma-) грязь; трясина, болото
скудный
-bovu плохой, негодный; неисправный
-epesi 1)легкий (*по весу*) 2)быстрый, скорый
-onya предостерегать, предупреждать
-chubuka слезать (*о коже, шкуре*); получать ссадину
-dumu 1)продолжаться, длиться 2)быть прочным, постоянным
-laumu 1)упрекать, критиковать 2)обвинять
-babaika теряться; мешкать
-egesha ставить на стоянку, парковать
-jitokeza появляться, показываться
-hakikisha 1)убеждать[ся], удостоверять[ся] 2)обеспечивать, гарантировать
-wasiliana общаться, контактировать, связываться
-ponda 1)раздавливать, разминать 2)переехать (*кого-л.*)
-elemisha учить, обучать, давать образование
-sababisha/ -sabibisha становиться причиной, вызывать

bima (-) страхование
fidia (-) [денежное] возмещение, компенсация
kitendo (vi-) действие, поступок
gereji (ma-;-) гараж
tanki, tangi (ma-;-) бак
mzunguko (mi-) оборот; поворот
brashi, burashi (-) кисть, кисточка, щетка
teke (ma-) удар ногой; пинок; лягание
tahadhari (-) предосторожность
-tahadhari быть осторожным, остерегаться
utelezi (ед.) 1)скольжение 2)скользкое место
-teleza 1)быть скользким 2)скользить, поскальзываться
-jeruhi ранить
-kwama застревать, завязать
-kwepa/ -epa избегать, уклоняться
-twanga толочь; молотить
-pisha давать дорогу, пропускать; уступать (*место*)
-paka накладывать (краску), мазать
-angalifu внимательный, бдительный
imara крепкий, прочный, устойчивый
wazi 1)открытый 2)ясный, понятный
-a kijani зеленый

Урок 10

mfalme (wa-) правитель, царь
mkubwa (wa-) 1)начальник, директор 2)предводитель
ukarimu (ед.) радушие, гостеприимство
kito (vi-) драгоценный камень
upole (ед.) 1)доброта 2)жалость, сострадание
mkasa (mi-) случай, приключение; просшествие
upenzi, upendo (ед.) любовь, расположение
jahazi (-; ma-) парусное судно
unga (ед.) 1)мука 2)порошок
jinsi (-) способ; метод, манера
tamaa(-) страстное желание, страсть
kamba (-) веревка, канат
kundi (ma-) группа; отряд
jeshi (ma-) армия; войско
mkonga (mi-) хобот
-husu относиться, иметь отношение, касаться
-simamia 1)наблюдать, контролировать 2)управлять
-lisha кормить, давать пищу
-saga молоть, размалывать, толочь
-tangulia идти впереди; опережать (*кого-л., что-л.*)
-ng'aa/ -ng'ara блестеть, сверкать
-pindua переворачивать, опрокидывать

hatima (-) конец; результат; заключение
yowe (ma-) крик, вопль
swala (-) импала (*антилопа*)
kisa (vi-) история, рассказ, сказка
jamii (-) 1)общество, коллектив 2)род, семейство
ncha (-) 1)остриё 2)оконечность
desturi (-) 1)обычай, традиция 2)привычка, обыкновение
mfuko (mi-) 1)карман 2)сумка, портфель, кошель
sarafu (-) 1)монета, мелочь 2)валюта
mjanja (wa-) 1)обманщик, плут 2)хитрец, ловкач
fujo (-) путаница, неразбериха; беспорядок
-dai 1)требовать 2)утверждать, заявлять
-kirimu 1)угощать 2)оказывать гостеприимство
-eneza распространять; разносить
-jidai притворяться, прикидываться
-tania 1)шутить, подшучивать 2)дразнить
kuhusu о[б], относительно
isipokuwa исключая, кроме, за исключением
bure 1)даром, бесплатно 2)напрасно, зря 3)бесплатный
chungu chungu в большом количестве, во множестве

Урок 11

kikosi (vi-) 1)отряд, группа 2)часть (военная), подразделение
zimamoto (-) 1)тушение пожара 2)пожарная команда
mzimamoto (wa-) пожарник
mwanadamu (w-) человек
madhara (мн.) вред, ущерб
makini (-) 1)внимательность, тщательность 2)внимательный
maskani, masikani (мн.) жилье, жилище
gharama (-) 1)трата, расходы 2)цена, стоимость
fukara (-; ma-) бедняк, нищий
kitambulisho (vi-) удостоверение, свидетельство, документ
mkokoteni (mi-) тачка, тележка
shoka (ma-) топор
pampu (-) насос, помпа
kurunzi (-) 1)прожектор, большая лампа 2)фонарь
agizo (ma-) заказ; распоряжение
-agiza заказывать; давать указания
-fikisha привозить, доставлять
-bishana спорить
-pumua дышать
-ungua гореть, пылать; сгорать, обгорать
-ajiri нанимать, брать на работу
-andikisha регистрировать

mkataba (mi-) договор, соглашение; контракт
kampuni (ma; -) компания, фирма
funzo (ma-) урок, наставление
sare (-) униформа
ndoo (-) ведро
ndoana (-) крючок (*рыболовный*)
jogoo (ma-) петух
kifungo (vi-) застежка (пуговица, крючок и т.п.)
nguzo (-) 1)опора 2)столб, колонна
tundu (ma-) 1)дыра, отверстие 2)впадина, углубление
jasho (ma-) пот; испарина
hila (-) 1)хитрость, уловка 2)коварство, обман
zamu (-) очередь, очередность; смена
oksijeni (-) кислород
orodha (-) список; перечень
menyu (-) меню
bili(-) счет; чек
heri, kheri (-) 1)счастье; удача, успех 2)лучше, предпочтительнее
-tundika вешать, подвешивать; прикреплять
-maanisha значить, означать
-angusha 1)ронять 2)бросать 3)сбивать, валить
-mudu 1)мочь 2)справляться 3)овладевать
-wika петь (*о петухе*)
-chungulia наблюдать, выглядывать (*украдкой*), подглядывать
-konyeza подмигивать
-okota 1)подбирать 2)[случайно] находить
-jipepea обмахиваться
-shikilia удерживать, поддерживать
-zoa подбирать; сгребать, сметать
kimoyomoyo в сердце, про себя, в душе
iwapo [в том случае] если
yaani 1)а именно; то есть 2)так сказать

Урок 12

hai живой
uhai (ед.) 1)жизнь 2)существование
kiumbe (vi-) создание, творение; существо
mmomonyoko (mi-) 1)эрозия 2)оползень
korongo (ma-) 1)овраг 2)канава, кювет
samadi (-) навоз
kima (-) обезьяна
rutuba (-) плодородие, плодородность
-rutubisha удобрять
-unga соединять, присоединять
-jiunga na 1)присоединяться 2) поступать, вступать (*в организацию*)
-oza портиться, гнить

kadiri/ kadri (-) величина; степень, мера
kunde (-) бобы
vumbi (ma-) пыль
spea (-) запчасти
wajibu (ед.) долг, обязанность
lengo (ma-) цель, задача
mfereji (mi-) канал; траншея
bwawa (ma-) запруда, плотина
mwanasesere (w-) кукла
sanamu (-) скульптура; статуя; памятник
sanaa (-) 1)искусство, вид искусства 2)ремесло, мастерство
stadi (ma-) мастер своего дела, умелец
stadi искусный, умелый
ustadi (ед.) искусство, мастерство
mashine (-) машина, механизм; агрегат
mfinyanzi (wa-) гончар
seremala (ma-) 1)плотник 2)столяр
samani (-) мебель, предметы обстановки
panga (ma-) длинный широкий нож; меч
mpira (mi-) резина; шина
fahari (-) гордость
usukani (sukani) руль, рулевой механизм
-hama переселяться, переезжать
-hamahama переезжать с места на место, кочевать, мигрировать
-chimba копать, рыть; выкапывать
-elekeza 1)показывать, указывать 2)направлять, наставлять
-linga ставить преграду; предохранять, оберегать
-nenepa жиреть, толстеть
-zalisha 1)производить, создавать 2)выращивать
-pangusa вытирать, протирать
-chuma собирать, рвать (*цветы, плоды и т.п.*)
-finyanga лепить из глины
-puliza 1)дуть (*с силой*) 2)надувать, накачивать
-tokana na происходить, брать начало
kutokana na из-за; исходя из, в соответствии с
kadha wa kadha некоторые, кое-какие
laini 1)гладкий, ровный 2)мягкий

Урок 13

sisimizi (-) маленький черный муравей
mzinga (mi-) улей
nyuki (-) пчела
dharau (-) презрение, неуважение
-dharau презирать
-jadili обсуждать

asali (-) мед
mwitu (mi-) лес
sifa (-) слава, известность
tikiti maji (ma-) арбуз
aibu (-) позор; стыд
shujaa (ma-) герой; храбрый человек
asilani никогда
-bembeleza уговаривать, упрашивать
-nyamaza молчать, замолкать
-angamiza уничтожать
-kwaruza царапать
-hisi чувствовать, ощущать

Урок 14

chatu (-) питон, удав
jembe (ma-) мотыга
-komaa достигать зрелости
-fyeka корчевать; вырубать
-kasirisha сердить
-chafua загрязнять, пачкать
-nyonya сосать, высасывать

СОДЕРЖАНИЕ

Часть I

Предисловие 3

Введение 5

УРОК 1 (Somo la kwanza)

Лексическая тема: **Приветствия. Знакомство (Salamu)** 8

1. Фонетика. Алфавит. Гласные и согласные звуки Слогоделение. Ударение. 8
2. Интонация. Вопросительные слова **nani, wapi, gani**. 17
3. Личные местоимения ед. числа **mimi, wewe, yeye**. 17
4. Притяжательные местоимения ед. числа **-angu, -ako, -ake**. 18
5. Приглагольные согласователи ед. числа **ni-, u-, a-**. 18
6. Настоящее время **-na-**. Глаголы бантуские и арабские. 18

УРОК 2 (Somo la pili)

Лексическая тема: **Чем вы занимаетесь?**

(Unafanya nini?) 24

1. Инфинитивная форма глагола. 24
2. Простое предложение. Связка **ni/si**. 25
3. Вопросительное слово **nini**. 25
4. Имя прилагательное. Прилагательные согласованные и несогласованные. 25
5. Односложные глаголы. 26
6. Императив (повелительное наклонение). 32
7. Предлоги **katika; kutoka**. Локативный суффикс **-ni**. 32
8. Предложения по типу **kuna – hakuna**. 33
9. Числительные **1 – 20**. 34

УРОК 3 (Somo la tatu)

Лексическая тема: **В гостях у друга**

(Nyumbani kwa rafiki) 40

1. Прошедшее время **-li-**, будущее время **-ta-**, показатель **-ka-** 40
2. Вопросительные слова **lini, -ngapi, vipi**. 41
3. Предлоги **baada ya, kabla ya, kwa**. 42
4. Спряжение глагола **-wa.** 48
5. Числительные **30 – 900**. 48

УРОК 4 (Somo la nne)

Лексическая тема: **Семья (Ukoo)** 54

1. Личные местоимения мн. числа **sisi, nyinyi, wao**. 54
2. Приглагольные согласователи мн. числа **tu-, m-, wa-.** 54
3. Спряжение глагола "иметь". 54
4. Отрицание глагола "иметь" (настоящее время). 55

УРОК 5 (Somo la tano)

Лексическая тема: **Дата и дни недели**
(Tarehe na siku za wiki) 67

1. Дни недели, число, месяц. 67
2. **-me-** как показатель перфектности. 68
3. Числительные **1000 – 100 000**. 79
4. Вопросительные слова **kwa nini** и **kwa sababu gani.** 74
5. Вопросительные слово **je** и частица **-je**. 74

УРОК 6 (Somo la sita)

Лексическая тема: **Мой день (Siku yangu)** 81

1. Отрицание глагола в настоящем времени. 81
2. Показатель **-me-** с глаголами состояния. 81
3. Счет времени. 88

УРОК 7 (Somo la saba)

Лексическая тема: **На рынке и в магазине**
(Sokoni na dukani) 97

1. Именные классы **m-/wa-** и **ji-/ma-.** 97
2. Указательные местоимения близости. 99
3. Согласование с притяжательными местоимениями. 100
4. Обобщительное местоимение **-ote.** 105
5. Посессивный формант **-a.** 105
6. Порядковые числительные. 106
7. Числительные **100 000 – 1 000 000.** 106

УРОК 8 (Somo la nane)

Лексическая тема: **В ресторане (Hotelini)** 114

1. Именной класс **ki-/vi-.** 114
2. Служебные слова **kwamba, kuwa, kama**. 115
3. Именной класс **m-/mi-.** 121
4. Названия суахилийских месяцев. 123
5. Определительные конструкции с поссесивом. 123
6. Видовой показатель **hu-**. 124

УРОК 9 (Somo la tisa)

Лексическая тема: **У врача (Hospitali)** 131

1. Отрицательные формы глаголов в прошедшем времени (1-ый класс). 131
2. Пассивный залог. 131
3. Отрицательные формы глаголов в будущем времени 141
4. Общее настоящее время **-a-.** 142

УРОК 10 (Somo la kumi)

Лексическая тема: **На почте и в банке (Posta na benki)** 149

1. Объектные приглагольные согласователи. 149
2. Возвратный залог. 149
3. Направительная форма глагола. 149
4. Инфикс **-ро-** во временном придаточном предложении. 158
5. Инфинитив в предложении с однородными сказуемыми. 159

УРОК 11 (Somo la kumi na moja)

Лексическая тема: **Мой дом (Nyumba yangu)** 165

1. Именной класс **n-/n-**. 165
2. Выражение модальных значений со словом **budi**. 167
3. Именной класс **u-/n-**. 173
4. Предлоги с пространственным значением. 174

УРОК 12 (Somo la kumi na mbili)

Лексическая тема: **Карта Восточной Африки (Ramani ya Afrika ya Mashariki)** 183

1. Приглагольные субъектные и объектные согласователи неодушевленных классов. 183
2. Именной класс **mahali.** 192
3. Глагол "**находиться**" 192

УРОК 13 (Somo la kumi na tatu)

Лексическая тема: **Животный мир Африки (Wanyama wa Afrika)** 201

1. Согласование прилагательных и количественных числительных. 201
2. Слова **-ingi, -ingine**. 204
3. Указательное местоимение дальности **-le**. 213
4. Степени сравнения прилагательных. 213
5. Посессивные конструкции с существительным, оформленным префиксом **ki-**. 214

УРОК 14 (Somo la kumi na nne)

Лексическая тема: **Отдых и развлечения (Burudani)** 220

1. Относительный союз **amba-**. 220
2. Релятив в глаголе. 221
3. Желательно-побудительное наклонение. 228

УРОК 15 (Somo la kumi na tano)

Лексическая тема: **Погода и климат (Hali ya hewa)** 238

1. Согласовательные модели имен существительных в локативной форме. 238
2. Сослагательное наклонение. 246
3. Взаимный залог. 247

УРОК 16 (Somo la kumi na sita)

Лексическая тема: **Транспорт (Usafiri)** 256

1. Условное наклонение. 256
2. Показатели **-mesha-** и **-ja-**. 257
3. Вопросительное слово **-pi**. 264
4. Стативная форма глагола. 265

Словарь активной лексики

Часть II 291
SOMO LA KWANZA "Встреча на улице" 291
Текст для аудирования: **Paka na binadamu**
Класс ku-
Тексты/диалоги: 295
Maisha ya nyumbani 300
Kumkaribisha mgeni

307

SOMO LA PILI "Домашние животные"
Текст для аудирования: **Siafu na nyoka** 307
Формант -ki- в функции причастия и деепричастия
Тексты/диалоги: 309
Asili yake Simu 314
Fikiri kabla ya kutenda

321

SOMO LA TATU "Путешествие"
Текст для аудирования: **Kibo na Mawenzi** 321
Местоимение -o -ote
Тексты/диалоги: 323
Kuvunja safari 328
Kupanda mlima Kilimanjaro 332
Ajali ya ndege

334

SOMO LA NNE "Выбор профессии"
Текст для аудирования: **Kanga na kuku** 334
Выделительная связка ndi-
Местоимения hivi, hivyo, vile в функции наречий образа действия 335
Тексты/диалоги: 338
Kazi ya mjomba 342
Kazi nzuri ni ipi? 347
Maana ya kazi

349

SOMO LA TANO "На приеме у врача"
Текст для аудирования: **Nyani** 349
Служебные слова -enye, -enyewe 350
Определительные конструкции -enye + инфинитив
Тексты/диалоги: 352

Faida ya hospitali 356
Bi Rehema anaumwa

364

SOMO LA SITA "Разговор по телефону"
Текст для аудирования: **Pepe huna masikio** 364
Безвременной релятив
Тексты/диалоги: 367
Asili ya kitabu 372
Vitabu kwa ajili ya vipofu 377
Mazungumzo ya simu

379

SOMO LA SABA "У лжи короткие ноги"
Текст для аудирования: **Safari ya mti** 379
Безличная форма глагола
Тексты/диалоги: 381
Fedha si msingi wa maendeleo 385
Juma na Saidi 392
Chenga na Selina

395

SOMO LA NANE "Стихийные бедствия"
Текст для аудирования: **Chui na nungunungu** 395
Аналитические глагольные временные конструкции
Тексты/диалоги: 398
Safari za baharini 403
Gharika 408
Njaa

410

SOMO LA TISA "Аренда автомобиля"
Текст для аудирования: **Punda na pundamilia** 410
Выражение модальных значений
Тексты/диалоги: 414
Usalama barabarani 419
Ajali barabarani 425
Kukodi gari

SOMO LA KUMI "Досуг и развлечения" 426
Текст для аудирования: **Uwongo wa nyoka**
Глаголы -zuia, -kataza 426

Недостаточный глагол **-ngali** 426
Тексты/диалоги:
Namna bahari ilivyotiwa chumvi 430
Tembo barabarani 435
Sungura mjanja 440

SOMO LA KUMI NA MOJA "В гостинице" 443
Текст для аудирования: **Jua na upepo**
Словообразование имен существительных 443
Тексты/диалоги:
Kikosi cha zimamoto 448
Sarafu yenye thamani 453
Hotelini 459

SOMO LA KUMI NA MBILI "Своими руками" 461
Текст для аудирования: **Mamba na kima**
Сложно-подчиненное предложение 461
Тексты/диалоги:
Udongo ni uhai 466
Shule za sanaa 472
Kutunza motokaa 477

SOMO LA KUMI NA TATU (marudio) 480
Тексты/диалоги:
Sisimizi alivyomwangamiza Tembo! 480
Jogoo wa ajabu 483
Vijana na simba 485
Dada Alyonushka na kaka Ivanushka 485

SOMO LA KUMI NA NNE (Kusikiliza hadithi) 490

Словарь активной лексики 492